BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 8 Juni, 2016

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae. Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI: Hati za kuwasilisha Mezani.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Waliondoka Ukumbini)

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

NAIBU SPIKA: Tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):

Taarifa ya mwaka ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii Nchini *(SSRA)* kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na mwaka wa fedha 2014/2015 *(The Annual Report of The Social Security Regulatory Authority for the Financial Year 2013/2014 and 2014/2015)*.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017.

Taarifa ya Sera za Fedha kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 na Mwelekeo wa Sera za Fedha kwa mwaka 2016/2017.

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 324

Hitaji la Ofisi na Nyumba za Watumishi Wilaya Mpya ya Nyang'hwale

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA aliuliza:-

Wilaya ya Nyang'hwale ni moja kati ya Wilaya mpya zilizoanzishwa hivi karibuni ili kuharakisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuwezesha kujenga ofisi na nyumba za watumishi katika Makao Makuu ya Wilaya eneo la Karumwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Halmashauri mpya ya Nyang'hwale ilipokea shilingi milioni 450 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ofisi katka Makao Makuu ya Wilaya iliyoko Karumwa. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 177.7 zimetumika kumlipa Mtaalam Mshauri ambaye ni *BJ Amili Limited* kwa ajili ya kuandaa michoro, upembuzi yakinifu na usanifu wa eneo lote zinalojengwa ofisi. Kiasi kilichobaki kinajumuishwa katika fedha zilizoombwa mwaka 2016/2017 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Halmashauri hiyo imetengewa shilingi milioni 850 kwa ajili ya kuendela na ujenzi majengo ya Makao Makuu ya Halmashauri katika eneo la Karumwa. Azma ya Serikali ni

kuhakikisha ofisi na nyumba za watumishi zinajenwa katika Wilaya na Mikoa mipya kwa awamu ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Josephine Chagula, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimuulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukosefu wa nyumba za kuishi watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale ni kubwa sana; watumishi hawa hulazimika kutembea umbali wa kilometa 50 mpaka 80, lakini wengine wanaishi Mkoani kabisa Geita ambako ni umbali wa kilometa 100. *(Makofi)*

Je, Serikali haioni kuna haja sasa ya kuharakisha majengo haya ili watumishi hawa waweze kuishi karibu na ofisi zao? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, tumekisikia kilio hiki, ndiyo maana mwaka huu tumetenga bajeti ya shilingi milioni 850.

Nawapongeza kwa sababu mshauri ameshaanza zile kazi za awali; ramani imeshapatikana na bajeti iliyolipwa pale kwa shilingi milioni 177, pesa iliyobakia inaonekana mkandarasi aliyepatikana hawezi kuanza kufanya kazi. Ndiyo maana tumesema kwamba mwaka huu tumetenga shilingi milioni 850, lengo letu kubwa ni kwamba tukichanganya na zile za mwanzo sasa, mkandarasi aweze kuingia *site* na hii kazi iende kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mchakato huu wa bajeti tutaharakisha fedha hizi ziende mapema ili mradi ujenzi uweze kuanza kwa wakati ili kuondoa kero kwa watumishi hawa ambao wanasafiri katika umbali mrefu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Makilagi.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tatizo la nyumba na ofisi katika Halmashauri mpya ya Wilaya ya Nyang'hwale ni sambamba na matatizo katika Halmashauri nyingi zilizoanzishwa hapa nchini ambazo ni mpya. Sasa napenda kujua, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga ofisi mpya na nyumba mpya katika Halmashauri zote nchini zilizoanzishwa ikiwemo na Halmashuri ya Butiama ambako ndiko alikotoka Baba wa Taifa? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa mama yangu na wamama wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Amina Makilagi kama ifuatavyo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili ni lazima nilijibu taratibu sana kwanza. Kweli hoja aliyoitoa Mheshimiwa Mama Makilagi ni ya msingi sana, ndiyo maana siku tulipokuwa tukihitimisha bajeti yetu ya TAMISEMI nilisema kwamba Halmashauri zile mpya lazima tuhakikishe tunaweka miundombinu na ni lazima nyumba zijengwe. Ndiyo maana katika kipaumbele chetu sisi cha TAMISEMI katika bajeti yetu ya mwaka huu, tuliziorodhesha zile Halmashauri ambazo ujenzi unaanza, lakini Halmashauri nyingine mpya hata ujenzi haujaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu swali hili ni kubwa na zito na limetolewa na Mbunge mzito, niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuliona hili tunaweka kipaumbele; kuna Halmashuri mpya zipatazo 20 tumezitengea kila moja shilingi bilioni 2,140,000,000 kila Halmashuri moja! Halmashauri hizo ni Buchosa, *Bunda TC, Chalinze DC, Handeni TC, Ifakara TC, Itigi DC, Kasulu TC, Kibiti DC, Kondoa TC, Madaba DC, Mafinga TC, Malinyi DC, Mbinga TC, Mbulu TC, Mpimwa TC, Nanyamba TC, Newala TC, Nzega TC, Songwe DC na Tunduma TC*. Hizi kila moja tumezitengea shilingi bilioni 2,140,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kuna Halmashauri zipatazo 44 tumezitengea kati ya shilingi milioni 500 na shilingi milioni 850. Hii maana yake ni nini? Wajumbe mbalimbali inawezekana wakasimama hapa kutaka kujua juu ya hoja hiyo.

Nakala hii iko hapa, mtu anaweza akafanya *reference* katika Halmashauri yoyote ambapo mwaka huu tumeweka kipaumbele, lazima Ofisi ya Rais, TAMISEMI ihakikishe inajenga miundombinu katika maeneo hayo, ili mradi wafanyakazi waweze kupata huduma bora na waweze kupata mazingira rafiki ya kufanyia kazi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge hapo pembeni ya Mheshimiwa Masele, naomba ujitaje jina, nimesahau kidogo.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Naibu Waziri wa TAMISEMI kwa majibu yake mazuri ya kwamba tumetengewa shilingi milioni 850 katika

Halmashauri ya Nyang'hwale. Namuomba Mheshimiwa Waziri kwamba kwa kuwa kuna pesa ambayo imetengwa, shilingi milioni 80 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wenye eneo lile. Naomba amuagize Mkurugenzi zoezi hilo la kuwalipa wananchi lifanyike haraka ili ujenzi huo uanze kujengwa mara moja. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, anayezungumza hapa ni Mbunge wa Jimbo hilo, maana yake yeye anayajua ya huko yalivyo na hizo pesa wameshatenga tayari. Hizo pesa kama zipo sasa, nadhani tusifanye ajizi. Namuomba Mkurugenzi haraka sana, kama vigezo vyote vimetimia, hakuna sababu kuwacheleweshea ulipaji wa fidia. Tunachotaka ni kwamba fidia ilipwe, ujenzi uendelee.

Mheshimiwa Naibu spika, kwa hiyo, moja kwa moja Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tunamwelekeza Mkurugenzi wa Nyang'hwale ahakikishe kwamba kama kuna hiyo fedha imetengwa na ipo, watu walipwe fedha zao ili mradi hii kazi hii isiendelee kuchelewa tena kwa sababu ina maslahi mapana kwa wananchi wa Nyang'hwale. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tunaendelea, Mheshimiwa Susane Peter Maselle, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Susanne Peter Maselle, Mbunge wa Viti Maalum, UKAWA, naomba sasa swali lake namba 325 lijibiwe.

Na. 325

Kuhusu fidia kwa wananchi wa Luchelele - Nyamafana

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y. MHE. SUSANNE P. MASELLE) aliuliza:-

Mwaka 2007 Serikali ilipima viwanja vya Luchelele Wilayani Nyamagana, Mwanza na iliendelea na mpango huo ambapo mwaka 2012 ilifanya tathmini na uhakiki kwa ajili ya kulipa fidia lakini hadi leo wananchi hao hawajawahi kulipwa fidia zao.

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi hao wa Luchelele kuhusu hatma yao hasa ikizingatiwa kuwa Waziri wa Ardhi alitoa ahadi mwaka 2015 kuwa atalitatua tatizo hili ndani ya mwezi mmoja?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chegeni hatuna UKAWA. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susanne Peter Maselle, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Luchelele lilipimwa mwaka 2008 likiwa na ukubwa wa hekta 873.38 ambapo viwanja vilivyopimwa ni 3,583. Katika zoezi hilo wapo wananchi waliokuwa ni wamiliki wa asili wa eneo hilo wapatao 683 ambao kwa makubaliano maalum yaliyofanyika tarehe 27/01/2013 chini ya Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, wamemilikishwa viwanja badala ya fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaodai fidia katika eneo la Luchelele ni wale ambao walikutwa katika maeneo yao lakini baada ya upimaji, maeneo hayo ni kwa ajili ya Taasisi au barabara na idadi yao ni 671. Wananachi hao wanadai fidia ya shilingi bilioni sita. Kauli ya Serikali ni kwamba wananchi hao watalipwa fidia na tayari Halmashauri imeomba mkopo kutoka Benki ya *CRDB* ambao wamekubali kutoa mkopo huo ili wananchi hao waweze kulipwa fidia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Chegeni, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Napenda nishukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa muuliza swali ametoka Bungeni humu na ameliacha swali hili, mimi naomba niulize kama ifuatavyo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa wananchi wa Luchelele wamekuwa kwa muda mrefu sana wakiahidiwa kuhusu suala la fidia; na pale Luchelele kulikuwa na mpango mpaka kujenga kiwanja cha *golf* ambacho mpaka leo hii imekuwa ni hadithi; na hii mara kwa mara tunaambiwa kuna fidia italipwa, imechukua muda mrefu. Sasa Serikali imefikia wapi kwa suala la fidia ili kweli wananchi wa Luchelele walipwe fidia yao na Serikali iendelee na mpango wake wa Luchelele kama ilivyopangilia?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Wilaya ya Nyamagana inapanuka kuelekea sehemu za Luchelele na kwa kuwa mipango mingi kule inafanyika. Je, Serikali kupitia Wizara yako, ina mkakati gani kuhakikisha kwamba ile Luchelele na *St. Augustine* yote inaendelezwa kwa mpango na masharti ya Mpango Mji wa Jiji la Mwanza? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu yangu ya awali nilisema kwamba wananchi hawa watalipwa fidia na taarifa zilizopo kama nilivyosema ni kwamba kuna mkopo kutoka *CRDB. Status* ya mkopo huo ni nini na tumefikia wapi mpaka sasa? Ni kwamba walipoleta ile *request,* katika ile shilingi bilioni sita, *CRDB* walikuwa wameweka *commitment* yao kuwakopesha shilingi bilioni 5.5. Kwa hiyo, ilivyokuja ile *request* TAMISEMI, ikaonekana kwamba deni linalodaiwa ni tofauti na mkopo watakaoweza kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ikatakiwa *clarification,* ni jinsi gani pesa nyingine itaweza kupatikana hapo? Wakaandikiwa tena barua, Mkurugenzi wa Nyamagana ambayo ni barua ya tarehe 5 Mei, 2016 kumwambia kwamba alete mchanganuo huo sasa, ile tofauti ya shilingi bilioni 2.5 ambayo inatakiwa ku-*top up* na ile ambayo inatoka *CRDB,* kuona italipwa vipi na utaratibu wake utakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakaleta hiyo *feedback* tena katika Ofisi ya TAMISEMI lakini hawakuambatanisha ule muhtasari wa vikao vilivyokubaliana hilo. Kwa hiyo, ofisi yetu imepeleka hiyo barua tena. Lengo ni kuleta zile *attachments* za makubaliano ya kikao ili mradi ofisi ya Rais, TAMISEMI iendelee na *process* ya kuhakikisha jambo hili linakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili kuhusu mikakati ya kuendeleza Wilaya ya Nyamagana; kama nilivyosema watu wa Nyamagana mpango wao mkubwa ni kuhakikisha maeneo hayo yanapimwa. Tunajua wazi kwamba Jiji la Mwanza ni kubwa sana, ndiyo maana katika suala zima la uendelezaji wake, tunaelekeza hizi Halmashauri na Manispaa zetu ziweze kuweka utaratibu mzuri wa mipango miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana watu wa Jiji la Mwanza, kwa sasabu kwa utashi wao mzuri na mawasiliano mazuri wamesababisha Jiji la Mwanza libadilike. Kwa kushirikiana na *LAPF* wametengeneza *center* nzuri sana ya kibiashara. Ni imani yangu kubwa sana kwamba mpango ule walioufanya *LAPF* na mikakati yao ya upimaji katika eneo la Nyamagana kuelekea maeneo haya ya Luchelele itaendelea. Lengo kubwa ni kulibadilisha Jiji la Mwanza liendelee kuwa bora, katika suala zima la kuendeleza Kanda ya Ziwa ya nchi yetu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Stanslaus. Oh, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nilitaka kuongezea tu katika majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la uendelezaji wa Mji wa Mwanza kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameuliza, Jiji la Mwanza pamoja na Majiji mengine kama 14 yako kwenye utaratibu wa kupanga Miji yao kwa maana ya kuwa na *master plan*; na Jiji la Mwanza ni mojawapo na *master plan* yake inaandaliwa na wameshirikishwa vizuri. Kwa hiyo, hata hawa ambao wako Luchelele wamekuwa *considered* katika ile *master plan* ambayo iko katika *process* ambayo inaandaliwa. Baada ya muda mfupi nadhani kwenye mwezi Juni hii itakuwa imekamilika na watakuwa katika utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika suala la fidia siyo Luchelele peke yake, ni maeneo mengi labda kwa kutumia fursa hii pia niseme Wizara imejipanga katika kuhakikisha tunawakumbusha wale wote ambao Mashirika na Taasisi mbalimbali ambazo zinadaiwa wakimewo wenzetu wa *Airport* Dar es Salaam na maeneo mengine na hata yale yaliyochukuliwa na Jeshi. Tunawaandikia ili kuwakumbusha zile fidia waweze kuzilipa kwa sababu zimekuwa za muda mrefu na kadri zinavyokaa ndivyo jinsi gharama ya Serikali inavyokuwa kubwa hasa katika kupitia katika Mashirika yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutalizingatia na tutaendelea kulifuatilia na watu wa Mwanza, Luchelele na maeneo mengine watafidiwa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Stanslaus Mabula, nilikuwa nimekutaja lakini naona Naibu Waziri ameongelea sana Mwanza. Bado swali lako lipo?

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimwa Naibu Spika, hoja yangu bado iko pale pale kwamba pamoja na majibu mazuri ya Serikali na utaratibu mzima ambao Jiji la Mwanza unao sasa wa *master plan* ya miaka 20 ijayo lakini kama tunavyofahamu, pamoja na *master plan* bado kuna suala la fidia. Luchelele sasa ni takriban miaka kumi tangu wamethaminishwa na fidia wanaambiwa kila leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika hatua sehemu wananchi wanachoka. Sasa ukopaji wa fedha hizi umeanza muda mrefu; ulianzia *TIB* ukashindikana; umehamia *CRDB;* lakini ili fedha ziweze kupatikana *CRDB* ni lazima kibali cha Serikali kutoka TAMISEMI kipatikane. Sasa lazima tuliweke vizuri, ni lini Serikali itakuwa tayari kutoa kibali cha fedha ili Halmashauri ipate fedha iende kulipa fidia na mipango inayotarajiwa hata ya *master plan* ifikie kwenye wakati wake na ikubalike vizuri na wananchi? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninayo barua ya tarehe 5 Mei, 2016. Barua hii inataka ufafanuzi kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Nyamagana. Lengo kubwa ni kwamba akisha-*meet* haya maelezo ambayo yameandikwa humu, tofauti yake ni nini? *CRDB* kama nilivyosema awali, walikuwa na uwezo wa kutoa mkopo wa shilingi bilioni 5.5. Kulikuwa na tofauti pale kidogo ambapo kulikuwa na maelezo ambayo yalitaka ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya TAMISEMI tarehe 5 Mei ikaandika barua kwa ajili ya hayo maelezo, ambapo kwa mujibu wa barua hii, yenye kumbukumbu Na. CE.214/237/01/31 imani yangu kwamba Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza ataweza ku-*meet* hivi vigezo vya barua hiyo. Halafu mwisho wa siku ni kwamba Waziri mwenye dhamana ataipitia ile *document*. Lengo ni kwamba wananchi wa eneo hili ambao wanadai fidia, fidia yao iweze kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua ni kweli jambo hili la muda mrefu, lakini naamini kwamba vigezo hivi vikipita na vikifika kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, basi atalitolea maamuzi sahihi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi name niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la Mwanza linafanana na tatizo la Tabora Manispaa, Kata ya Malolo na mpaka sasa hawajalipwa fidia ya aina yoyote na wakati huo huo Mheshimiwa Waziri wa Ardhi aliwahi kufika na kutoa agizo. Je, Serikali inasemaje kuhusu kulipa fidia ya hawa wakazi wa Kata ya Malolo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kama nilivyosema katika majibu ya awali ambayo nilikuwa naongezea kwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais (TAMISEMI), nimesema Wizara imejipanga katika kupitia; kwa sababu tumekusanya madai haya au migororo na fidia anazozisema mengi yako katika ile orodha tuliyoichukua. Kwa hiyo, tutakachofanya sisi ni kukumbusha taasisi zinazohusika na fidia hiyo ili waweze kulipa, kwa sababu ni nyingi kweli zimekaa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna namna nyingine ya kufanya kwa sababu Serikali haiwezi kulipa fidia ambayo inadaiwa taasisi au maeneo mengine tofauti. Kwa hiyo, tutakachofanya sisi ni kupeleka kumbukumbu za kuwakumbusha wahusika na pale ambapo Serikali inahusika yenyewe basi itajipanga namna ya kuweza kuilipa.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge Manyoni Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 326

Ujenzi wa Barabara ya Kuingia Itigi

MHE. YAHAYA O. MASSARE aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano katika kampeni zake za uchaguzi alipokuwa Itigi aliombwa na wananchi wa Itigi kuwajengea barabara ya kuingia Mji wa Itigi yenye urefu wa kilometa 8.3 na akakubali.

Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kama ilivyoahidiwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kuingia Mji wa Itigi *(Itigi access road)* yenye urefu wa kilometa 8.3 iko chini ya Halmashauri ya Mji wa Itigi. Hata hivyo, ujenzi wa barabara hii utatekelezwa wakati wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara kuu ya Makongorosi - Rungwa - Itigi hadi Mkiwa yenye urefu wa kilometa 413.

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Makongolosi -Rungwa - Itigi hadi Mkiwa umekamilika na kwa sasa Serikali inatafuta fedha za kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Massare swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mkiwa - Itigi, Rungwa - Makongorosi aliyoitaja Mheshimiwa Waziri ni barabara inayopita katikati ya Mji wa Itigi wenye vijiji vya Songambele, Majengo na Itigi Mjini na kwa majibu haya, maana yake barabara hii imeshushwa daraja. *(Makofi)*

Swali, wakati sheria inabadilika kutoka mita 45 kuja mita 60, wananchi hawa waliwekewa alama za "X" kwamba wasiendeleze maeneo yale. Sasa kwa majibu haya; je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutamka kwamba wale wananchi waendelee na ujenzi? *(Makofi)*

Pili, Naibu Waziri anaweza kuthibitishia wananchi wa Itigi kwamba itakapoanza kujengwa kilometa 35 za kwanza na kipande kile kitakajengwa pamoja nacho? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimechanganyikiwa nimechanganyikiwa kidogo kwa sababu swali la pili linapingana au linakinzana na swali la kwanza; kwa sababu swali la kwanza tumemwambia tunajenga hiyo barabara wakati tunajenga hiyo ya kutoka Rungwa - Makongorosi hadi Mkiwa. Kwa maana nyingine, lile eneo ambalo limewekewa "X" ni lazima liendelee kubakiwa kuwekewa "X". Sasa tumemaliza kufanya upembuzi yakinifu, hatua zinazofuata ni za kulipa fidia na kuanza ujenzi baada ya kutafuta hizi fedha na kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili sijui nijibu vipi kwa sababu nadhani la pili linajibu kwa hili la kwanza, kwa sababu tunajenga hili eneo na tutajenga. Tunachokifanya ni tunatafuta fedha.

Kwa hiyo, naomba sana asiwaambie watu wajenge hilo eneo. Maeneo ambayo yamewekewa "X" maana yake ni kwamba katika upembezi yakinifu imeonekana hapo ndiyo barabara itapita. Tafadhali sana, usiwahimize wakajenga, hilo eneo libakie ili tutakapopata fedha tuweze kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, siyo kwamba tutajenga na hiyo, tunajenga kupitia hapo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwambalaswa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona na kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa ahadi aliyotoa Mheshimiwa Rais kwenye Mji wa Itigi inafanana kabisa na ahadi aliyotoa kwenye Mji mdogo wa Makongorosi ambapo alisema kwamba wakati inajengwa barabara ya kutoka Chunya kwenda Makangorosi na kuelekea Itigi na Mkiwa, Serikali itawajengea wananchi wa Makongolosi lami kilometa nne; je, ahadi hiyo itatekelezwa wakati barabara hiyo inajengwa? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni ahadi ya viongozi wetu, ni wajibu wetu na dhamana yetu kutekeleza ahadi za viongozi wetu pamoja na ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia kwamba ahadi hii itakamilika na hasa wakati ujenzi huu wa barabara ya kutoka Mkiwa hadi Makongorosi itakapofikia hilo eneo, kwa vyovyote na hizo kilometa nne ambazo zimeahidiwa, zitajengwa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Barabara ya Bigwa – Kisaki, Wilaya ya Morogoro Vijijini ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Awamu ya Tano kujengwa kwa lami. Mpaka sasa hivi hata kwenye bajeti iliyopita sikuona kitu chochote kinachoelezea kuwa itajengwa. Je, barabara hii kwa niaba ya wananchi wa Morogoro Vijijini itajegwa lini kwa kiwango cha lami? Ahsante *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumeongea na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo, ni kwamba hii barabara tutaijenga. Mheshimiwa Ishengoma anafahamu na tulishaongea kwamba hii barabara ambayo ni ahadi ya kiongozi wetu wa Kitaifa, tutaitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba kiwango kilichowekwa katika bajeti ya mwaka huu ni ya matengenezo peke yake, ujenzi tumeshindwa kuuweka safari hii kwa sababu tumetoa vipaumbele kwa zile barabara ambazo makandarasi wako *site* na tunataka tuwamalizie hawa makandarasi wasiendelee kulipwa fedha bila kufanya kazi. Kwanza, tuwalipe fedha ili wakamilishe barabara ambazo zilishaanza muda mrefu. Tukishamaliza hiyo, sisi

baaada ya hapo, sina uhakika kama ni lugha nzuri, lakini sisi ni mwendo mdundo kutekeleza ahadi zote za viongozi wetu na ahadi zote zilizomo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuanzia mwaka wa pili wa Awamu hii ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa naomba tupeni fursa ili tumalize kwanza hizi barabara ambazo zilikuwa zimeanza vipindi vya nyuma na wakandarasi wengi wako *site* wanapokea hela, *interest* na vitu vingine wakati hawafanyi kazi kwa sababu tulikuwa hatuna uwezo wa kuwalipa. Sasa tunafanya hilo, tukimaliza mwaka huu unaokuja hawa wote tutakuwa tumewamaliza na sasa tutaanza kutekeleza kwa kasi maeneo mengine yote ambayo viongozi wetu wakuu wameahidi na Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imeongea. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tunaendelea. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Namanyamba, sasa aulize swali lake.

Na. 327

Huduma ya Mawasiliano ya Simu Kata za Jimbo la Nanyamba

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka huduma ya mawasiliano ya simu ya mkononi kwenye Kata za Mbembaleo, Nyuundo, Mnima na Kiyanga?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Mbambakofi, Mwamko na Mwang'anga kutoka katika Kata ya Mbembaleo, vijiji vya Namahukula, Namambi na Namgogoli kutoka katika Kata ya Mnima na vijiji vya Mkahara, Mnongodi, Mwamko na Tulia kutoka katika Kata ya Kiyanga vimo katika orodha ya vijiji vitakavyopata huduma ya mawasiliano kupitia utekelezaji wa awamu ya pili na awamu ya tatu ya mradi wa mawasiliano ya *Viettel (Halotel)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa awamu ya pili na awamu ya tatu ulioanza Novemba, 2015 na unategemewa kukamilika Novemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Kata ya Nyuundo vimeainishwa na Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na vitaingizwa katika miradi ya siku za usoni kwa kadri ya upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi zitakavyopatikana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chikota hukuniambia kwamba kuna kijiji kinaitwa jina langu huko kwako. Swali la nyongeza. *(Kicheko)*

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, kipo! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza kwa kuwa Mfuko wa Mawasiliano umenufaisha Kata chache sana katika Jimbo la Nanyamba; je, Serikali ipo tayari sasa kuingiza Kata ya Nyuundo na Kata nyingine ambazo hazina mawasiliano katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 badala ya kutuambia siku za usoni ambazo hatujui itakuwa ni lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kuna Makampuni ya Simu yamefunga minara katika baadhi ya kata zetu lakini upatikanaji wa mitandao bado ni hafifu kama vile Kata ya Njengwa na Milangominne.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari sasa kuyaagiza sasa makampuni hayo kutuma wataalamu ili wakaangalie matatizo ya minara hiyo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu mafupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vijiji vya Kata vya Nyuundo ambavyo vimeainishwa katika awamu itakayofuata nimelichukua na tutaliangalia kama linaweza likatekelezeka kwa namna ambavyo ameeleza kwa sababu anafahamu kwamba bajeti imeshapita na tutaliangalia kwa namna itakavyowezekana. Naomba tu nimhakikishie kwamba Kata hii ya Nyuundo kwa vyovyote vile tutaishughulikia na mawasiliano tutayapeleka. Suala ni lini, itategemeana na fedha kama zitapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la maeneo Njengwa na Milangominne, minara kutofanya kazi, nimelichukua tutalifanyia kazi. Nitawafuatilia wahusika nione hasa kuna tatizo gani. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kafumu.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kule Wilaya ya Igunga Jimbo la Igunga kulikuwa na Kata za Kiningila, Sakamaliwa na Kinungu, zilikuwa zimewekwa kwenye Mpango wa Mawasiliano kwa Wote, lakini pia Jimbo la Manonga Kata ya Goweko na Kata ya Mwanshiku. Ni lini sasa mradi huu utatekelezwa kwa maana yake tulitegemea mwaka 2015 na mwaka 2014 yafanyike? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mila zetu, ukiulizwa swali na bosi wako huruhusiwi kujibu kwenye hadhara. Namuomba Mheshimiwa Dalaly Peter Kafumu tukutane ofisini ili tuweze kuwatendea haki wananchi wa Jimbo hili la Igunga pamoja na Jimbo jirani ambalo ameliulizia. Nakuomba sana tuonane ofisini ili tuweze kukutana na wataalam halafu tuliweke sawa, tuone ni namna gani ya kufanya. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kutupa kipaumbele sisi Kambi mbadala.

Kwa kuwa matatizo ya mawasiliano yaliyoko katika Jimbo la Nanyamba yanafanana na Jimbo la Ulanga, Kati ya Kata ya Ruaha, Chilombola, Ilagula, Ketaketa na Ilonga; je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu za mkononi katika Kata hizi ili na wananchi hawa wafaidi mawasiliano ya simu za mkononi? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maswali yako tutayashughulikia, tumeyachukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate ufafanuzi zaidi wa hayo maeneo aliyoyaeleza ili tuweze kuyafanyia kazi na kuwatendea wananchi wake kwa namna inavyotakiwa. Naomba tukutane ofisini tuelezane kwa undani zaidi kuhusu hilo eneo ili hatimaye tutende kile ambacho wananchi wanakihitaji. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Mtwara Vijijini, maeneo ya Moma na Dihimba kote, usikivu wa simu za mikononi siyo mzuri.

Je, ni lini atakwenda kufuatilia yale makampuni ambayo yalipewa kazi ya kuweka minara huko ambapo mpaka sasa hivi kwa kweli kwingine wamejenga, haisikiki na kwengine hawajafika kabisa? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, CHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hawa Ghasia kama Mwenyekiti wa Kamati, vilevile amemwona Waziri wangu kutetea maslahi ya watu wa Jimbo lake. Namshukuru sana kwa juhudi kubwa anazozifanya, kwanza kutusaidia sisi wote kama nchi kupitia Kamati ya Bajeti, lakini vilevile kuwatetea wananchi wa Wilaya ya Mtwara, Jimbo la Mtwara Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia nitafika kukakagua hilo eneo na baada ya hapo tutampa majibu sahihi, siyo majibu tu, lakini vilevile kujibu kwa vitendo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tunaendelea. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile na swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Kakunda.

Na. 328

Ajali Zilizotokea Nchini – Januari 2015 Hadi Sasa

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA (K.n.y. MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM) aliuliza:-

Kumekuwepo na ajali nyingi zinazosababisha vifo na majeruhi barabarani, baharini na kwenye maziwa.

Je, ni ajali ngapi zimetokea barabarani, baharini na kwenye maziwa kuanzia Januari, 2015 hadi sasa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile, lililoulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Kakunda Joseph, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha Januari, 2015 hadi Februari, 2016 jumla ya ajali zilizotokea ni 9,864 ambazo zimesababisha vifo 3,936 na majeruhi 9,868 katika Mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi kama hicho jumla ya ajali 15 za baharini na kwenye maziwa zilizotokea, ambapo tisa zilitokea baharini na sita zilitokea katika maziwa. Katika ajali hizo, jumla ya watu 24 walipoteza maisha na watano walijeruhiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kakunda, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kuhusu masuala ya ajali barabarani. Sasa nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, Tarafa ya Kitunda ambayo iko umbali wa kilometa 180 kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Sikonge ina Kituo cha Polisi kidogo ambacho kina polisi wanne ambao hawatoshi kuhudumia wakazi zaidi ya 80,000 kwenye Tarafa hiyo. Maana kuna majengo chakavu, polisi wenyewe ni wachache na hawana gari hata moja; lini Serikali itawasaidia polisi hao ili wafanye kazi yao vizuri? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mwezi Machi, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Nyahwa alichinjwa kama kuku na hadi leo wauaji wale hawajakamatwa. Ni lini Serikali itafanya kazi yake kikamilifu ili wauaji hao wakamatwe na kuondoa hofu Kijiji cha Nyahwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu, maswali ya nyongeza yanatokana na swali la msingi. Swali la msingi lilikuwa linahusu vifo vinavyosababishwa na ajali. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri tusimuulize maswali ambayo hayahusiki na lile swali la msingi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani unaweza kujibu swali la nyongeza la kwanza, la pili unaweza ukaliacha kwa sababu halitokani na swali la msingi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kakunda kwamba *concern* yake ambayo amei-*raise* hapa tutaifanyia kazi ya kwa maana ya kwamba tutaongeza idadi

ya askari katika kituo hicho. Kwa hiyo, nachukua fursa hii kuwaelekeza Jeshi la Polisi wale askari ambao wako *depot,* tunaotarajia kuwa-*deploy* karibuni, basi tuangalie uwezekano wa kuwapeleka Sikonge kuongeza ile idadi ya askari waliopungua pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pale ambapo magari ambayo tunatarajia yataingia wakati wowote, nayo tuone uwezekano wa kufanya hivyo kwa kuzingatia changamoto eneo hilo baada ya kulifanyia utafiti wa kina pamoja na mahitaji ya nchi nzima. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mboni Mhita.

MHE. MBONI M. MHITA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba Jimbo la Handeni Vijijini ambalo kwa upande mmoja ni barabara kubwa ya Mkata kupitia Korogwe kuja mpaka Misima; ila askari wa Jimbo la Handeni ama Wilaya nzima ya Handeni hawana usafiri wa ku-*patrol,* jambo ambalo naamini kama wangeweza kuwa na usafiri huo kwa namna moja ama nyingine wangeweza kupunguza idadi ya ajali ambazo zinatokea. Lakini pia, swali langu la pili…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mboni, swali la nyongeza huwa ni moja.

MHE. MBONI M. MHITA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili nalo vilevile tumelichukua. Tutaangalia vilevile utaratibu na hali halisi ilivyo na changamoto ya eneo la Handeni na changamoto za maeneo mengine na idadi ya magari ambayo tutayaingiza kwa awamu inayokuja. Pia tutalipa uzito kwa kutilia maanani changamoto ambazo ametueleza Mheshimiwa Mbunge.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Molel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Naomba niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa ajali nyingi zinasababishwa na baadhi ya madereva walio wazembe na mfano mzuri ni katika Jiji la Dar es Salaam katika utaratibu mpya ulioanzishwa kwa jitihada za Serikali wa mabasi yaendayo kasi; hadi sasa zaidi ya mabasi 30 yamepata ajali na gharama za matengenezo hayo ni zaidi ya shilingi milioni 90. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhakikisha kwamba kama ni

sheria, zinawabana madereva wazembe wanaoisababishia Serikali hasara? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baadhi ya madereva wakiwemo madereva wa pikipiki, bodaboda na magari binafsi na hata magari mengine tu kwa ujumla, bado sharti na sheria inayotaka wasitumie barabara ya mabasi yaendayo kasi inakuwa ngumu sana kwao na hivyo kusababisha ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba barabara ile ni kwa ajili ya mabasi yaendayo kasi na siyo vinginevyo. Kwa hiyo, mtumiaji mwingine yeyote anayetumia barabara zile anakuwa amevunja sheria na hivyo, yeye ndiye amegonga yale mabasi na kusababishia hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli takwimu zinaonesha kwamba ajali ni nyingi, na sisi tunasema tutaendelea kusimamia sheria ili kuhakikisha wananchi wanapata elimu, lakini pia watambue kwamba kwa kufanya hivyo wanafanya makosa makubwa na kusababisha hasara. Hawaruhusiwi kutumia barabara za mabasi yaendayo kasi zinazotumika sasa kwa Dar es Salaam.

Kwa hiyo, nawaomba sana wakazi na watumiaji wa barabara Dar es Salaam, kuheshimu barabara za mabasi yaendayo kasi ili kuipunguzia Serikali hasara zinazojitokeza.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa aulize swali lake.

Na. 329

Hitaji la Benki – Jimbo la Mlalo

MHE. RASHID A. SHANGAZI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itashawishi Benki za Biashara kuwekeza katika Jimbo la Mlalo ambalo mzunguko wa fedha ni mkubwa sana kutokana na magulio ya mboga mboga na matunda?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo huduma za kibenki katika sehemu zenye shughuli za kiuchumi kama kilimo cha mboga mboga na matunda kama Jimbo la Mlalo. Kwa sababu hiyo, Serikali imekuwa ikijitahidi kuboresha mazingira ya utoaji huduma za kibenki ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara na miundombinu ya umeme ili kuchochea zaidi shughuli za uzalishaji na hatimaye kuvutia mabenki kufungua matawi sehemu hizo. Ikumbukwe kuwa uanzishaji wa huduma za kibenki hutegemea upembuzi yakinifu ambao unazingatia uwezo wa kupata faida pande zote mbili yaani benki na wananchi. Hii pia hutegemea na uchumi wa eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko ya kuendesha mfumo wa kifedha nchini unaotekelezwa kuanzia mwaka 1991, Serikali imekuwa ikitekeleza azma ya kujitoa katika kuhusika moja kwa moja na biashara ya mabenki. Kwa hiyo, Serikali imebaki na jukumu la kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ili kuiwezesha sekta binafsi kuanzisha benki na kutoa huduma bora za kifedha kwa wananchi wetu, hususan pale ambapo huduma hizo zitaweza kujiendesha. Serikali inaendelea na ushauwishi wake wa Benki za Biashara na taasisi nyingine za fedha kuanzisha huduma za kibenki na kifedha popote ambapo kuna mzunguko mkubwa wa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ushawishi wa Serikali, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Serikali yetu, kuwashauri wananchi wa Mlalo kujiunga na kuanzisha Benki za Kijamii *(Community Banks)* na taasisi ndogo za kifedha *(Micro Finance Institutions)* zinazozingatia mazingira ya mahali husika ili kukidhi mahitaji ya kibenki ya Jimboni Mlalo.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kwa kuwa iliyokuwa *NBC*, Benki iliyokuwa inamilikiwa na Serikali ilikuwa na tawi pale mlalo na ilikuwa inahudumia wakazi wa Mlalo, Mbaramo, Mtae mpaka Mlola; je, kwa nini *NMB* iliyochukua nafasi ya *NBC* isitekeleze wajibu huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amesema sehemu ambazo zina mzunguko mkubwa wanaweza wakaongeza ushawishi wa kutengeneza *Community Bank;* na Jimbo la Mlalo lina mzunguko mkubwa wa fedha; je, ni lini kwa kushirikiana na *SACCOS* ya *Kumekucha Mwamko SACCOS Ltd.* wanaweza wakawajengea uwezo ili tuweze kuanzisha hiyo *Community Bank?* Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba Serikali ilijitoa moja kwa moja kuendesha shughuli hizi, lakini Serikali kupitia Wizara yangu itaendelea kuhimiza mabenki kuendelea kusambaza huduma zao kwa wananchi wa vijijini likiwepo na Jimbo la Mlalo. Pia nitalifikisha ombi hili katika Benki yetu ya *NMB* na kuwashauri kuhusu ombi hili la Mheshimiwa Rashid Shangazi ili tuone sasa *NMB* inaweza kurejesha huduma ambayo mwanzo ilikuwa ikiendeshwa na Benki yetu ya *NBC*. Kwa hiyo, nitakaa nao, nitaongea nao na namwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane naye ili tuweze kuongea na Menejimenti ya *NMB* ili kurejesha huduma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ipo tayari kabisa kutoa ushauri wa kitaalamu na namna ya kuanzisha benki za kijamii. Ninafahamu pale Mlalo hasa maeneo ya Lukozi, maeneo ya Rangwi, Mlalo yenyewe, Shume na Mlola kuna huduma nyingi za kiuchumi, hivyo niko tayari kabisa kuishauri Benki Kuu kwamba sasa tukatoe huduma hizi za kitaalamu kwa wajasiriamali wetu hawa ili waweze kuanzisha Benki ya Kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, kuna *society* nzuri pale ambayo tukishirikiana nao na mtaji unaotakiwa kuanzisha *Community Bank* ni shilingi bilioni mbili tu, kwa taarifa nilizonazo, taasisi hii iliyopo pale ina zaidi ya shilingi bilioni moja sasa. Kwa hiyo, wamebakiza sehemu ndogo tu waweze kuanzisha *Community Bank*. Mheshimiwa Rashid Shangazi tushirikiane ili tuweze kuanzisha *Community Bank* pale Mlalo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mhagama.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba niulize swali lingine la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile huduma hizi za kibenki ni suala la kisera; na kwa vile ni haki ya kila Mtanzania kupata huduma hizi; na kwa vile imebainika kwamba mabenki yetu ya kibiashara hayawezi kufika yale maeneo ambayo hayana tija sana kibiashara; ni lini sasa Serikali itahakikisha kwamba Benki ya Kilimo inayafikia maeneo hayo ambayo hayana tija kwa wafanyabiashara wa kibenki likiwemo Jimbo la Madaba na Jimbo la Mlalo kama ilivyoulizwa? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mhagama kama ulivyosikia wakati tunaweka Mezani bajeti yetu ya Wizara ya Fedha, moja katika benki ambazo tunategemea kwamba zitafungua

matawi yake zaidi, ni hiyo Benki yetu ya Kilimo. Kwa hiyo, tunaendelea kuijengea uwezo na muda siyo mrefu Benki hii itafungua matawi yake katika maeneo yenye wakulima wetu ili waweze kufaidika na huduma za Benki yetu ya Kilimo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shally Raymond, swali fupi.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa kuna mtazamo kwamba kila kundi kufungua benki ndiyo jibu la huduma ya benki, siyo jema; na kwa kuwa hapa tulipofikia, huko nyuma tulikuwa na Benki ya Posta ambayo iko kila mahali na watumiaji wa benki ni hao hao wananchi wa eneo lile; je, ni kwa nini sasa Serikali isiipe uzito Benki ya Posta ikasambaa kote? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, katika benki ambazo zinakuja juu sasa ni Benki yetu ya Posta. Tumeiwezesha vizuri, Menejimenti yake imekaa vizuri sasa, imezindua huduma nyingi ambazo hata benki nyingine kubwa za kibiashara zimeshindwa kuanzisha huduma hizo. Kwa hiyo, ni imani yangu kubwa Benki ya Posta ndani ya muda mfupi ujao itarejesha hadhi yake ndani ya nchi yetu ya Tanzania.

Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kuiunga mkono Benki yetu ya Posta, tufungue akaunti kule, tuiwezeshe sisi kama *shareholders* muhimu ili Benki ya Posta iweze sasa kurejea. Tuko vizuri na inakimbia Mheshimiwa Shally, itafungua matawi yake sehemu zote nchini. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Albert Ntabaliba Obama, Mbunge wa Buhigwe sasa aulize swali lake.

Na. 330

Mradi wa Maji Mnanila

MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

(a) Je, ni lini Mradi wa Maji wa Mnanila, Mwayaya na Mkatanga utaanza kutoa maji kwa kuzingatia ahadi za Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli?

(b) Je, kwa nini Serikali haitoi fedha ili kumaliza miradi ya maji ya Munzenze, Kirungu na Nyamugali ambayo sasa imekuwa kero kwa wananchi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Albert Ntabaliba Obama, Mbunge, wa Jimbo la Buhigwe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Mnanila, Mwayaya na Mkatanga ni mradi wa zamani uliyotekelezwa katika miaka 1970. Mradi huu kwa sasa umechakaa, na haufanyi kazi. Kutokana na ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Serikali ilituma fedha kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe kiasi cha shilingi 10,000,000 kwa ajili ya kufanya usanifu wa mradi na kuhamasisha jamii kushiriki katika ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha andiko la ukurabati la mradi huu linaonesha mradi utagharimu shilingi bilioni moja nukta sifuri nane. Utekelezaji wa mradi huu utaanza katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji ya Munzenze, Kirungu, na Nyamugali ni miongoni mwa miradi ya vijiji kumi inayotekelezwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Vijijini ambapo utekelezaji umefikia asilimia 86 kwa mradi wa Munzenze, asilimia 65 kwa mradi wa Kirungu na asilimia 50 kwa mradi wa Nyamugali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika, Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017, imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.28 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe. Serikali itaendelea kutuma fedha ili kukamilisha miradi kwa kadri zinavyopatikana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Albert Obama swali la nyongeza.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwanza naomba nipongeze juhudi za Serikali katika kutatua tatizo la maji nchini, lakini namba mbili naomba niendelee kuipongeza Wizara ya maji kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kata ya Mnanila, wananchi wa Kata ya Mwayaya na Kata Mkatanga katika majibu ya Waziri anasema utekelezaji wa maradi huu utaanza katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Maji, watu wale hawaelewi programu ya pili, ya tatu hawaelewi. Swali lao, je, mradi huu unaanza kutekelezwa lini?

Swali la pili Jimbo letu la Buhigwe bado lina vijiji na Kata ambazo kwa kweli bado tuna matatizo makubwa ya maji. Je, Waziri anaweza akatuma wataalamu wake kwenda kwenye Kata ya Rusaba Kibande, Kilelema, Mgera, Kibigwa na Nyaruboza ili kufanya tathimini ya gharama za kupeleka maji katika vijiji vile ili navyo tuweze kuviingiza kwenye programu hapa baadaye?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ameuliza hii Programu ya Pili ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Kwanza ya Maendeleo ya Sekta ya Maji tuliianza katika bajeti ya mwaka wa fedha 2006/2007 ambayo imekamilika mwaka 2015 Disemba na katika programu hiyo tulikuwa na wadau wanaotuchangia fedha pamoja na Serikali yenyewe nayo imekuwa inatoa fedha kwa ajili ya utekelezajiwa miradi ya maji. Katika programu hiyo Mheshimiwa Mbunge mwenyewe ni shahidi kwamba miradi ya Munzenze, Kirungu na Nyamgali, ilianza kutekelezwa na sasa hivi ina maendeleo mazuri tu katika hiyo programu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa programu ya pili tumeianza mwezi Januari, 2016, inaendelea, nayo itadumu kwa muda wa miaka mitano na katika programu hiyo wadau wa maendeleo tayari wameshatoa ahadi ya kutuchangia dola bilioni tatu na nukta tatu. Lakini hiyo ni pamoja na Serikali nayo itaendelea kukusanya fedha na kuchangia kwenye utekelezaji wa miradi kwenye vijiji ambavyo bado havijapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuna vijiji ambavyo bado havijafikiwa na hii programu na Mheshimiwa Mbunge ameomba kwamba je, tutatuma wataalam lini? Mheshimiwa Mbunge natambua kwamba unayo Halmashauri ya Buhigwe, lakini Halmashauri ya Buhigwe bado ni changa, tutakachofanya na ambacho tumeshaanza kufanya sasa hivi ni kwamba Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji, inaendelea kuajiri wataalam na kuwapeka katika Halmashauri yako na Halmashauri nyingine zote ambazo zina upungufu wa wataalam. Ili tuwe na wataalam maeneo husika kuliko kuwachukua wataalam kutoka Wizarani. Lakini pale inapohitajika kama utaalamu unahitajika zaidi basi tutakuwa tuko tayari Mheshimiwa Mbunge kuja kutoa utaalamu zaidi kwenye eneo lako.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Getere, swali fupi tafadhali.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujua tu katika Wizara ya Maji kuna miradi sugu katika Jimbo langu la Bunda, kuna mradi wa maji Mgeta Nyang'alanga, Nyamswa Salama na kuna mradi wa maji Kiloreli na fedha zinazodaiwa Mgeta ni milioni 119 na Nyamswa ni milioni

229 na Kiloreli milioni 400. Naomba kujua tu hizi fedha zitaenda lini ili miradi hii ikamilike? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu mafupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa katika Halmashauri ya Bunda Vijijini kiasi kumekuwa na matatizo na kuna miradi ambayo haijakamilika lakini pili, katika utekelezaji Halmashauri haijatuletea hati ili tuweze kulipa hiyo fedha. Kwa hiyo, nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi na yeye tutasaidiana kufuatilia kuangalia kuna tatizo gani kwenye hii Halmashauri. Kwa nini hii miradi imechelewa sana utekelezaji, kuna tatizo gani? Je, ni ni tatizo la kiutaalam au ni uzembe? Mimi pamoja na yeye tutalifuatilia hili kuweza kuhakikisha miradi hii inakamilika.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa Mradi wa Maji wa Nyamugali unafanana na Mradi wa Maji wa Mvomero hususani katika eneo la Dihinda, Kanga, Mzia na Lubungo; na kwa kuwa katika maeneo hayo kuna visima virefu vilichimbwa na Wizara mwaka jana. Visima vile vimeachwa kama maandaki na Serikali imetumia mamilioni ya fedha.

Je, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wako tayari kufuatana na mimi kwenda kuangalia visima vile na kutoa kauli ni lini miradi ile itapata fedha ili ikamilike na wananchi wapate maji safi na salama?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu mafupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imeshachimba visima, kilichobaki sasa hivi ni kuweka mtandao wa mabomba ili maji sasa yaweze kuchukuliwa kutoka kwenye visima kuwafikia wananchi. Mheshimiwa Mbunge wewe mwenyewe ni shahidi kwamba mwaka huu tayari tumeweka fedha kwenye Halmashauri zote ili kuhakikisha kwamba sasa fedha hizo zitumike kuweka mtandao huo wa maji ili wananchi waweze kupata maji kwa sababu uwekezaji wa visima tayari umeshafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufuatana naye, tusubiiri tumalize Bunge, Mheshimiwa Mbunge hiyo ni kazi yetu tutapita kila eneo ili kwenda kuangalia matatizo yaliyopo na kushauriana jinsi ya kuyatekeleza.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la kutopeleka fedha kwenye miradi ya maji ambalo kwa mujibu wa swali la msingi liko pia katika miradi mbalimbali inayotekelezwa Mkoa wa Pwani. Mfano mradi wa Ujenzi wa Bwawa Kata ya Chole, Wilaya ya Kisarawe, lilitengewa kiasi cha

shilingi 1,500,000,000 lakini zilipelekwa 500,000,000 na bwawa lilipojengwa pamoja na mvua bwawa lile limeharibika.

Je, Naibu Waziri yupo tayari kufanya ziara Wilaya ya Kisarawe kwa kuwa ipo karibu na Dar es salaam ili kuona namna gani watakavyofanya na Wizara ili bwawa lile likamilike kwa wakati na wakazi wa Chole wapate maji kama ilivyokusudiwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimwambie kwamba niko tayari kuongozana naye baada ya Bunge kwenda kuangalia hilo bwawa. Lakini pili nimuhakikishie kwamba tayari tunayo tume ambayo kazi yake itashughulikia masuala ya kujenga mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji. Tume hiyo sasa hivi iko tayari na tutahakikisha kwamba tunapeleka fedha na tatizo hili kwamba ilipelekwa fedha lakini nyingine haijaenda nafikiri tatizo kubwa ni huu utaratibu tuliouweka kwamba kama ujaleta hati sasa na sisi tutashindwa kuomba fedha kutoka Hazina. Tunachataka kwanza utuletee hati ili ile hata tuipeleke Hazina na Hazina wapate ushahidi kwamba kazi imefanyika waweze kutupa fedha ili tuweze kuzileta.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo sasa aulize swali lake.

Na. 331

Uhaba wa Maji Wilaya ya Urambo

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza:-

Serikali ina mkakati wake wa kupata maji kutoka Mto Ugala ili kukabiliana na uhaba mkubwa wa maji katika Wilaya ya Urambo.

(a) Je, ni hatua gani zimechukuliwa hadi sasa katika kutekeleza ahadi hiyo na kiasi gani cha fedha kitatumika?

(b) Je, kiasi gani kimetengewa kwa mwaka mpya wa fedha?

(c) Je, ni lini mradi huu utafikisha maji Urambo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margatet Simwanza Sitta Mbunge wa Jimbo la Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze wananchi wa Urambo kwamba wamechagua jembe. Mila za Kiafrika tunajua kwamba akina mama ndio wanaochota maji na huyu mama anahangaika sana na hadi leo asubuhi amekuja ofisini, hakunikuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua tatizo la maji kwa Mji wa Urambo Serikali ilipanga kupatia mji huu maji kutoka chanzo cha Mto Ugala. Katika hatua za awali za upembuzi yakinifu wa mradi, ulionekana Mto Ugala hukauka wakati wa kiangazi kati ya Juni na Oktoba. Kutokana na changamoto zilizotajwa, mpango wa Serikali wa kupeleka maji Urambo ni kutoka Mto Malagarasi na siyo Mto Ugala. Mradi huu unatarajiwa kugharimu kiasi cha dola za Marekeni 332.91.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imetenga kiasi cha shilingi 500,000,000 kwa ajili ya kukamilisha usanifu wa mradi. Aidha, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na Shirika la Maendeleo la Ufaransa *AfD* kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huo mkubwa utagawanywa katika *lot* nne ili kuharakisha utekelezaji wake. Kwa kufanya hivyo mradi unatarajiwa kufikisha maji Urambo katika kipindi cha Miaka miwili mara baada ya fedha kupatikana.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwanza naipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu, lakini kutokana na uhaba mkubwa wa maji unaowakabili wananchi wa Urambo, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza la nyongeza, kwa kuwa mradi huu ndio kwanza mradi wa maji ya kutoka Malagarasi uko katika awamu ya upembuzi yakinifu; na kutokana na umbali wa Mto Malagarasi kutoka Urambo, na shida iliyopo pale Urambo. Nilikuwa nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba hivi Serikali haioni wakati huu wanapoendela na upembuzi yakinifu wakachimba bwawa la maji Mto Ugala ili bwawa hilo lipate maji kutoka Mto Ugala, pia na maji ya mvua ambayo yanapotea bure ili yawasaidie wananchi kupata maji wakati bado huu mradi ambao utachukua muda mrefu unaendelea kushughulikiwa.

Swali la pili la nyongeza, ningependa kujua hizo *lot,* au awamu ambazo zitatekelezwa katika upatikanaji wa maji kutoka Malagarasi na kuhakikishiwa kwamba Tarafa ya Usoke imo pia?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati tunashughulikia huu mradi mkubwa tumetenga fedha kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo kwa ajili ya kuweza kuhakikisha wananchi wa Wilaya ya Urambo kwa ajili ya kuweza kuhakikisha wananchi wa Urambo wana endelea kupata maji wakati tunasubiri huu mradi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika kufanya usanifu wa Miradi hii tunaangalia kitu kinaitwa *cost* na *benefit*. Yaani kuchukua maji Mto Malagarasi itafaidisha vijiji 68 katika Wilaya ya Uvinza, Uyui, Kaliua, kwa hiyo ni mradi ambao una-*benefit* watu wengi zaidi na ndio maana Serikali ikaona kwamba tuweke, badala ya kuchukua Mto Ugala ambao kiangazi unakauka tuweze kuuchukua huu mradi mkubwa ambao wananchi wengi watapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu suala la bwawa, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwanza tutatembelea eneo lile ili tuone uwezekano kwamba bwawa hili lifanyiwe usanifu kwa ajili ya maji ya umwagiliaji kwa ajili ya wananchi wanaoishi maeneo yale.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona, kwa kuwa tatizo la maji lililopo Urambo linafanana kwa ukaribu kabisa na tatizo la maji lililopo katika mji wangu mdogo wa Mlowo, na kwa vile katika Mji huo kuna mto uitwao Mto Mlowo.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuchimba mabwawa katika mto huo ili kuhakikisha kwamba wananchi wa mji mdogo wa Mlowo, hususani wanawake ambao Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba ndio wachotamaji wakubwa wanaondokana na adha hiyo ya mji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ametuomba kwamba tuna Mto Mlowo na akinamama wanakwenda kuchota maji Mto Mlowo, sasa haoni kwamba kuna umuhimu wa kuchimba mabwawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaagiza tayari kwamba Halmashauri zote zifanye utafiti na zilete mapendekezo ili Serikali iweze kutenga fedha kuhakikisha kwamba kila Halmashauri na tumeomba kwamba kila Halmashauri kila mwaka ihakikishe inachimba bwawa moja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Shonza naomba na wewe ni Diwani, tusaidiane kwenye vikao vyetu tuelekeze kwamba Wakurugenzi na wahandisi wa maji wa Halmashauri zetu wafanye utafiti ili tuweze kupata maeneo ya kuchimba mabwawa tuweze kuondoa hii kero ya maji.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mwaka 2013 Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya kuchimba visima vinane katika vijiji vinane, lakini hadi sasa shilingi milioni 184 tu zilizopelekwa.

Naiuliza Serikali ni lini sasa kwa sababu azma ya Serikali ilikuwa ni kuchimba visima vinane; ni lini sasa Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya visima hivyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ujasikia vizuri swali? Mheshimiwa Ndassa sehemu ya mwisho ya swali ni lini?

MHE. RICHARD M. NDASSA: Katika Jimbo la Sumve na Jimbo la Kwimba Serikali ilipanga kuchimba visima vinane katika vijiji vinane vya Isunga, Kadashi, Gumangubo, Shilima, Mande na Izimba A. Fedha zilizotengwa ni shilingi bilioni 3.6 lakini hadi juzi ni shilingi milioni 185 tu ndizo zilizopelekwa, kwa hiyo, miradi hii imekwama, ni lini sasa Serikali imepeleka fedha hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, tumeishaelekeza tayari, kwamba ukishapata bajeti, Halmashauri ikipata bajeti, kitu cha kwanza ni kufanya taratibu za manunuzi. Kuhakikisha kwamba mkandarasi anaanza kazi, na akishatekeleza kazi utuletee hati, ya madai ya mkandarasi tuweze kuipeleka kwa Waziri wa Fedha aweze kutupatia fedha.

Nina wasiwasi lakini tutashirikiana na Mheshimiwa Ndassa kuangalia ni kazi ipi imeishafanyika tangu kupeleka hiyo hela, inawezekana kwa sababu hata wakati wa ziara yangu niliona hiyo. Unakuta mtu ametengewa bajeti lakini hajafanya kazi yoyote, anasubiri kwamba kwanza aletewe hela, utaratibu huo kwa sasa hatunao. Ukishapata bajeti basi fanya taratibu za manunuzi na mkandarasi afanye kazi akifanya kazi ndio tutampatia hela. *(Makofi)*

MHE. ISSA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona, aliyoyazungumza Mheshimiwa Ndassa yanafanana na Jimboni kwangu Mbagala. Kuna mradi ule wa maji, Mpera na Kimbiji, ambao sasa hivi unafika miaka nane, haujatekelezwa na wala maji hakuna. Lakini vilevile kulikuwa na mpango wa kuchimba visima virefu katika Jimbo langu, mpaka leo mpango ule haujatekelezwa kwa kukosa fedha.

Je, Waziri anatupa jibu gani wakazi wa Mbagala, na wananchi wa Mbagala kwa ujumla, lini visima vile vitaanza kuhudumia Jimbo la Mbagala na Dar es Salaam kwa ujumla na je, ule mpango wa visima virefu upo au umekufa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maji inaendelea na mradi wa kuchimba visima vya Mpera na Kimbiji; na mpaka sasa tunavyoendelea tayari tumeishafikia asilimia 60, na mradi huo unakamilika mwezi Disemba mwaka huu. Baada ya hapo tutaanza na mradi mwingine sasa wa kuweka mabomba, ambayo sasa yatatoa maji kwenye visima na kuyasambaza mpaka kwenye maeneo yake, ya Mheshimiwa Mbunge ya Mbagala. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba hakuna wasiwasi ule mradi unaendelea, na mwaka huu unakamilika. Lakini pia ameomba kwamba je, Serikali ina mpango gani wa kuchimba visima virefu? Ni kwamba tunaendelea kulingana na bajeti tunavyotenga, tutaendelea na kama maji yanapatikana tutaendelea kuchimba visima virefu.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Nditiye, Mbunge wa Muhambwe, sasa aulize swali lake.

Na. 332

Marekebisho ya Mpaka wa Hifadhi ya Moyowosi na Wananchi

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE aliuliza:-

Mwezi Septemba, 2015 Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, aliwaahidi wananchi wa Kata za Busonzu, Busagara na Murungu ambao wamepakana na Hifadhi ya Taifa ya Muyowosi kwamba mpaka kati ya wananchi hao na hifadhi hiyo, utarekebishwa ili wananchi wapate eneo kwa ajili ya kilimo.

Je, utekelezaji wa ahadi hiyo utaanza lini?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia uongozi wa Serikali ya Wilaya ya Kibondo inayo taarifa ya maombi kutoka kwa wananchi wa Kata za Busonzu, Busagara na Murungu kuongezewa maeneo kutoka Pori la Akiba la Moyowosi kwa matumizi ya shughuli za kibinadamu, ikiwa ni pamoja na shughuli za kiuchumi na kijamii katika vijiji vya kata hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itayaorodhesha maombi haya katika orodha ya maeneo yanayopakana na hifadhi, yatakayoshughulikiwa kimkakati na Serikali; kwa kushirikisha wadau wote muhimu, zikiwemo Wizara za Maliasili na Utalii, Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, TAMISEMI, Maji,

Nishati na Madini na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, kwa nchi nzima. Utaratibu huu unaotarajiwa kuanza baada ya Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Moja kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaendelea kusisitiza kwamba utekelezaji wa azma ya Serikali ya kujibu kero za wananchi kuhusu changamoto za mahitaji ya ardhi, utazingatia uwepo wa sheria, kanuni na taratibu na pia kuweka mbele maslahi ya Taifa. Aidha Hifadhi ya Pori la Akiba la Moyowosi lilianzishwa kisheria, kwa Tangazo la Serikali namba moja, la mwaka 1981 baada ya kukidhi vigezo vyote, ikiwemo ushirikishwaji wa wananchi katika hatua za Vijiji, Kata, Mkoa hadi Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kuhifadhi Pori la Akiba la Moyowosi Kitaifa, unazingatia bioanuwai katika mfumo wa ikolojia ya Moyowosi Malagarasi. Inayotoa mchango mkubwa wa viumbe mbali mbali wanaopatikana katika maeneo hayo, pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji kwa matumizi ya binadamu. Eneo hilli pia ni sehemu ya ardhi ya owevu, yenye hadhi ya kimataifa yaani *Ramsar Site*.

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa miaka mingi sana hadi mwaka jana mwanzoni, wananchi waliruhusiwa kufanya shughuli za uvuvi ndani ya hifadhi pamoja na ufugaji nyuki. Lakini toka mwaka jana mwanzoni Serikali ilipiga marufuku na wananchi wakiingia kule wananyanyaswa sana ikiwa ni pamoja na kupigwa na wafanyakazi wa Idara ya Wanyamapori na Wahifadhi.

Je, ni lini Serikali itaruhusu wananchi, waendelee kufanya shughuli za uvuvi na ufugaji nyuki, kwa kuwa kwa kufanya hivyo, itajenga mahusiano mazuri kati ya Serikali na wananchi?

Swali la pili, sehemu kubwa ya hifadhi hiyo ya Moyowosi haina alama kwenye mipaka yake na kwa kuwa wananchi wanakuwa wakinyanyaswa sana kwa ajili ya kufanya shughuli zao ambazo walikuwa wamekwisharuhusiwa na Serikali, ni lini sasa Serikali itakuwa tayari kuweka alama hizo za mipaka? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza wakati Serikali imetoa ruhusa ya kufanya shughuli zile za uvuvi na ufugaji nyuki, ruhusa ile ilizingatia masharti ya kitaalam kwamba shughuli hizi za kibinadamu kwa kiwango hicho ambacho kiliruhusiwa kilikuwa hakiathiri shughuli za uhifadhi katika eneo linalohusika na kwamba utaratibu huo, utaendelea kutumika pale

itakapoonekana kwamba kuna umuhimu wa kufanya hivyo kwa ushauri wa wataalam.

Hivyo basi, ningeweza kusema kwamba tutakwenda kuangalia eneo hili *specifically* sasa hivi, mahsusi lakini kwa kuwa nimeishatangulia kusema kwamba Serikali tayari inao mpango wa kushughulikia masuala haya kimkakati zaidi, basi nimuombe Mheshimiwa Mbunge avute subira kidogo, twende tukayaangalie yote hayo kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya swali lake, kuhusiana na kwamba eneo kubwa au sehemu kubwa haina alama, hii ni mojawapo ya changamoto ambayo inasumbua masuala ya uhifadhi kwenye maeneo yetu kwamba maeneo mengi alama zake ziko kwenye kumbukumbu za kitaalam, unazungumzia *coordinates* kwa mfano. *Coordinates* kwa mtumiaji wa kawaida mwanakijiji ambaye anapakana na eneo hilo si alama ya kutosha kuweza kumfanya mwananchi huyo aweze kutii Sheria vizuri zaidi.

Kwa hiyo, tunaposema tunakwenda kushughulikia kimkakati zaidi, ni pamoja na kwenda kuweka alama za kudumu lakini zinazoonekana vile vile. Lakini pia zitakazoshirikisha wananchi wanaoishi au jamii zinazoishi kwenye maeneo hayo, ili tukubaliane kwamba kuanzia hapo sasa huo ndio mpaka, na mpaka huo utakuwa unaonekana vizuri, na kila mmoja atalazimika kuuheshimu.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Tumekuwa tukiona mapori mengi ya hifadhi yakiingiliana na makazi ya watu katika jamii na mapori hayo yamekuwa yametengwa kwa muda mrefu sana.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kugawa mapori haya ya hifadhi yaliyotengwa kwa muda mrefu kwa wananchi, ili waweze kufanya shughuli za kijamii kama kilimo, na mifugo na hii itaweza kuwaondolea adha ya migogoro ya wafugaji na wakulima? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali inayo taarifa na inatambua kwamba iko kiu kubwa ya wananchi wanaoishi kwenye maeneo yanayopakana na hifadhi kwamba pengine wangechukua maeneo yale ili waweze kuyatumia katika shughuli zingine za kibinadamu, ikiwemo kilimo, ufugaji, pamoja na shughuli zingine. Lakini ni kweli pia sisi sote ni wananchi na nchi ni moja na kwamba sababu za kuifadhi maeneo hayo zilizingatia pia uhitaji wa mahitaji yetu ambayo ni ya kudumu ya muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu utaratibu ule, wa kuweza kuyatwaa maeneo haya na kuyatumia kama Hifadhi, yalikuwa ni maamuzi yetu

sisi sote pamoja, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, tulishirikisha Vijiji, Wilaya pamoja na Mikoa ili kuweza kukubaliana kwamba maeneo hayo yahifadhiwe kwa sababu ambazo zina maslahi mapana zaidi, si kwa Taifa tu, lakini pia hata kwa wananchi ambao ni wa nchi nzima na sio wale wanaoishi kwenye maeneo yale tu pale walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, narejea tena kusema kwamba kwa sababu umepita muda mrefu tangu maeneo hayo yalipotwaliwa kuwa kama hifadhi, pengine mazingira yamebadilika, pengine kuna sababu ambazo zinaweza zikaonekana kwamba zina uzito zaidi hivi sasa, ndio maana nimesema Serikali inakwenda kulishughulikia suala hili kimkakati, itakuwa ni pamoja na kushirikisha wananchi upya, wote twende tukaangalie na tupime kwamba je, sasa tuseme nchi hii isiwe na hifadhi kabisa? Maeneo yote tutwae kwa ajili ya shughuli zingine za kibinadamu? Pengine hiyo itakuwa ni upande mmoja haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tukisema kwamba kinyume chake kwamba maeneo yale ya hifadhi yote yabaki kama yalivyo, pengine kuna maeneo tunatakiwa kufanya marekebisho kidogo. Sasa tukatae kwa sababu kuna Sheria, hata kama kuna ukweli kwamba kwa sasa hivi kuna sababu za msingi, pengine na yenyewe itakuwa si sahihi. Ndio maana tunasema kwamba sasa Serikali pamoja na wananchi wanaoishi kwenye maeneo hayo, na pengine wananchi kwa nchi nzima wakitoa maoni tutakwenda kufika mahali sasa tukubaliane kwamba maeneno yapi tunahifadhi, kwa sababu zipi ambazo zitakuwa ni kwa maslahi ya taifa. Niwakumbushe sio kwa maslahi tu ya Taifa, sisi kama nchi tumesaini pia mikataba ya kimataifa, kuhusu masuala ya uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda hautoshi ningeweza kusema zaidi lakini napenda kuishia hapa, tunakwenda kufanya zoezi hili kwa pamoja, kutatua kero hizi kwa namna ambayo itakuwa ni endelevu, na ya kudumu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, sasa aulize swali lake.

Na. 333

Mbuga ya Akiba ya Uwanda Katika Wilaya ya Sumbawanga Vijijini

MHE. IGNAS A. MALOCHA aliuliza:-

Mbuga ya Akiba ya Uwanda katika Wilaya ya Sumbawanga Vijijini ilitengwa miaka ya nyuma wakati idadi ya watu ikiwa ndogo sana ikilinganishwa na sasa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulipunguza pori hilo ili kunusuru shida inayowapata wananchi wanaozunguka eneo hilo ya kukosa maeneo ya kilimo na ufugaji?

(b) Je, kwa nini wananchi wa maeneo hayo wanapigwa na Askari wa Wanyamapori na kunyang'anywa mali zao, wakati hakuna alama yoyote inayoonyesha mpaka katika mbuga hiyo?

(c) Je, wananchi wa vijiji vinavyozunguka pori hilo wamenufaika na nini zaidi ya vipigo wanavyovipata?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori la Akiba Uwanda lenye ukubwa wa kilometa za mraba 5,000 lilianzishwa mwaka 1959 na kutangazwa upya kwa Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Namba 12 ya mwaka 1974, kwa tangazo la Serikali namba 275 la tarehe 8 Novemba, 1974. Kati ya mwaka 1974 na 2013 pori hilo lilikuwa chini ya usimamizi ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ambapo lilikabidhiwa rasmi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii tarehe 20 Januari, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, pori hili linazungukwa na jumla ya vijiji tisa ambapo asilimia kubwa ya wakazi wake wanajihusisha na shughuli za kilimo, uvuvi na ufugaji. Umuhimu wa pori hili umejikita katika uhifadhi wa rasilimali wanyamapori, mimea na mazalia ya samaki katika Ziwa Rukwa ambayo ni mojawapo ya vyanzo vikuu vya kiuchumi kwa wananchi wa eneo hilo. Pamoja na umuhimu huo, Pori la Akiba Uwanda kama yalivyo maeneo mengine ya hifadhi, linakabiliwa na changamoto ya ongezeko la shughuli za kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, eneo kubwa la pori hili ni sehemu ya Ziwa Rukwa, na sehemu iliyobaki yenye eneo la kilometa za mraba 400 ni nchi kavu. Kutokana na umuhimu huo Wizara yangu inaona ni mapema kupunguza ukubwa wa pori hilo kwa sababu uamuzi huo utaathiri sababu na malengo ya kuanzishwa kwake. Hata hivyo, Serikali kwa upana wake itajumuisha eneo hili la Pori la Akiba la Uwanda, kuwa miongoni mwa maeneo yanayotarajiwa kushughulikiwa kimkakati zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu haikubaliani na vitendo vya baadhi ya watumishi wake, wakiwemo Askari Wanyamapori kujichukulia sheria mkononi kwa kuwapiga, kuwanyang'anya mali, kuwatoza faini kinyume cha

utaratibu, kuwachomea moto nyumba zao, na kuwanyanyasa kwa namna yoyote ile, kwa kisingizio cha kutekeleza matakwa ya sheria. Wizara yangu inasisiza msimamo wa Serikali wa kuendelea kusimamia utawala wa sheria, na hivyo kujipanga zaidi, ili kuchukua hatua kali dhidi ya watumishi watakaodhibitika kukiuka, kwa mujibu wa sheria, kanuni, na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaombwa, kutoa ushirikiano katika kuwabaini watumishi wa aina hii, na pia wachukue hatua stahiki kabla, wakati na baada ya matukio ya aina hiyo ili kuirahisishia Serikali kuchukua hatua sahihi kwa wakati sahihi. Hata hivyo Wizara yangu inasisitiza kuwa wananchi wanaoishi katika maeneo yanayopakana na hifadhi, wazingatie na kutii sheria bila shuruti. Ili hifadhi hizo ziendelee kuleta manufaa kwa taifa wakiwemo wananchi hao kwa tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba ni kipindi kifupi tu, takribani miaka miwili na nusu tangu usimamizi wa Pori la Akiba Uwanda, ukabidhiwe kwa Wizara yangu. Tayari tumeanza mkakati wa kuwekeza kwa kuboresha miundombinu na vivutio ili kuhakikisha kwamba pori hilo linarudi kwenye hadhi yake ya awali. Kabla ya kufanyika kwa shughuli za utalii zitakazoiwezesha Serikali kushughulikia ipasavyo changamoto za maendeleo ya wananchi. Azma hii inaendana na mipango ya Serikali ya muda mrefu ya kuboresha shughuli za utalii Ukanda wa Kusini.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanzishwa kwa pori hilo mwaka 1959 hadi sasa ni miaka 57; je, Serikali inaweza kusema kwa kipindi hicho, imepata faida gani zaidi ya Askari Wanyamapori kukodishia wafugaji na wakulima wasio na uwezo kuruhusiwa kulima halafu baadae wanagawana mazao?

Swali la pili, kwa majibu yaliyotolewa ninapata imani kuwa, Mheshimiwa Waziri anadanganywa na wataalam wa chini yake. Je, yuko tayari kuongozana na mimi kwenda kwenye Mbuga hiyo, ili akajionee changamoto zilizopo na baadae asiweze kudanganywa na watumishi wake?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza pori lina faida gani na zaidi ya miaka 50 iliyopita anataka kujua kuna faida gani imepatikana kutokana na uhifadhi huo?

Kwanza niseme tu kwamba faida za uhifadhi ziko zile ambazo unaweza ukazitazama kwa macho au ukazikamata mkononi ambazo ni za kifedha na pengine ni za kiuchumi moja kwa moja. Lakini uhifadhi hasa wa mapori wakati

mwingine faida zake unaweza usizione kwa macho au ukakamata kwa mikono kwa sababu faida zake ni za kiikolojia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida zake zinakwenda kuambukiza hata uwekezaji, hata shughuli zingine za kiuchumi, lakini pia hata uwepo wa dunia tunayoishi na nchi tunayoishi yakiwemo masuala ya hali ya hewa, upatikanaji wa maji, na mambo mengine ya namna kama hiyo. Kwa hiyo, faida zipo na ni nyingi, lakini kama alikuwa anakusudia za kiuchumi zinazohusiana na fedha, hilo ni suala la takwimu na kwa hiyo basi anaweza kutafuta fursa tukaonana na kwa kutumia wataalam ambao na wenyewe nitawasemea kwenye swali la pili basi tunaweza tukapata takwimu, kujibu vizuri zaidi kuhusiana na suala la faida za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili la kuongozana, kwanza niweke sawa juu ya suala hili ambalo linajirudia mara nyingi sana la kwamba kuna kupata taarifa ambazo ni za uongo au za kudanganywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna jambo niko makini nalo ni hilo na naomba Waheshimiwa Wabunge mnisaidie ili kwa upande wangu lakini nafikiri kwa Serikali nzima; ikiwa kuna majibu ambayo yanakuwa yanatia mashaka na pengine ni ya uongo; kwa sababu majibu ya uongo ni kama vile yamedhamiliwa. Kama kunajitokeza mazingira kama hayo, basi tuanze sasa kukataa namna hiyo ya kufanya kazi, kwa sababu hiyo ni namna ambayo haifai.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa upande wangu anayetoa jibu ninamfahamu, na anapotoa jibu namuambia anaweka saini kabisa kwenye jibu hilo analonipatia. Sasa baada ya hili kwa sababu tayari umeishanipa hiyo *indication* baada ya hapa, mimi na yeye tutakwenda kutafuta jibu sahihi ni lipi kulinganisha na hili ili yule aliyelitoa sasa kama kweli amedanganya, kwa sababu kudanganya ni dhamira, basi atachukuliwa hatua kwa mujibu wa kanuni na taratibu, lakini kwa kawaida kila mmoja kila mtumishi wa Serikali, anao wajibu wa kutenda kazi zake sawa sawa na anao wajibu kwenye masuala ya kujibu maswali, anao wajibu wa kujibu maswali kwa niaba ya Serikali na kwa hiyo, anawajibika kutoa majibu ambayo ni sahihi.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nilikuwa naomba niulize Serikali na niulize Wizara ya Maliasili na Utalii, je, ni lini sasa italipa fidia au italipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi katika hifadhi zote ambazo zinapakana na wanyamapori, leo ni mwaka wa tano fedha ambazo wananchi wamelipwa ukizingatia vijiji 16 Wilaya ya Babati Vijijini bado hawajalipwa wamelipwa shilingi milioni 12 tu kati ya shilingi milioni 100 na, na nikifuta jasho na wala siyo fidia.

Je, ni lini na ni lini sasa Serikali itakuja tulipendekeza hapa kwamba hifadhi husika ndiyo ziwe zinalipa hizo fidia badala ya Wizara ya Maliasili na Utalii ili iwe rahisi sasa hifadhi ambazo ziko jirani na hivyo vijiji waweze kulipa mara moja ili wananchi hao sasa wapate unafuu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii maswali yamekuwa mengi hapo naomba ujibu moja tafadhali kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na naomba nijibu swali la nyongeza moja au mawili pengine inaweza kuwa moja kwa mawili kadri alivyouliza Mheshimiwa Mbunge.

NAIBU SPIKA: Ujibu moja tafadhali kwa sababu ndiyo kanuni zinavyosema kwa hiyo, chagua moja.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Ahsante, suala la ulipaji wa kifuta jasho na kifuta machozi, yapo mambo mawili jambo la kwanza ni utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa kanuni kwamba ule ni lazima utimie ukamilike na ambao unaanzia kwenye ngazi ya kitongoji au kijiji kwenda wilaya kwenda mkoa halafu kwenda hifadhi inayohusika na mpaka kwenye Wizara. Yale maombi au madai yanayopata sifa za kuweza kulipwa sasa yataingia kwenye kikwazo kingine cha pili ambacho si kikwazo lakini ni utaratibu kwamba kuna suala pia la bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna suala la kutimiza vigezo halafu kuna suala la uwepo wa fedha. Sasa yale yanayohusiana na utaratibu kwa sababu unahusisha pia Wizara kama kuna madai ambayo yamekidhi vigezo lakini pengine yanachelewa kwa sababu tu ya *procedure* za kiofisi hayo tunakwenda kuongeza kasi kuharakisha ili yakae *pending* kusubiri uwepo wa fedha na fedha zitakapokuwa zimepatikana madai yote yanayohusiana na kifuta jasho, na kifuta machozi yatalipwa mara moja.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa wananchi wa Kasulu wengi wao kwa kutokujua mipaka inaishia wapi; wamekuwa wakilima mpakani mwa pori la Kagera Nkani na kwa sasa mazao yao yako tayari wanahitaji kuvuna.

Je, Serikali iko tayari kumuagiza Mkuu wa Wilaya awaruhusu wananchi waweze kuvuna mazao yao huku utaratibu mwingine ukiwa unaendelea?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, maagizo yametolewa mahususi kabisa kuhusu suala hilo kwamba Wizara pamoja na Wakuu wa Wilaya wawaruhusu wananchi ambao wamelima ndani ya hifadhi zetu waweze kuvuna mazao yao kabla hawajaondoka katika maeneo hayo.

Kwa hiyo, nimkumbushe tu Mkuu wa Wilaya juu maagizo hayo na awaruhusu wananchi wachukue mazao yao.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona swali langu ni dogo tu ambalo linafanana na swali la msingi la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, utamaduni uliokuwepo wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa miaka ya nyuma uliruhusu wananchi wanaoishi kando kando mwa maeneo ya hifadhi waliruhusiwa kuvua samaki kwenye mabwawa hususan wananchi wa Jimbo langu la Rufiji wa maeneo ya Luwingo na utaratibu huu ulienda sambamba na kata zote; kata ya Mwasenimloka, kata ya Ngolongo pamoja Kagira, naomba kufahamu Wizara ya Maliasili na Utalii inaweka utaratibu gani sasa ili kuweza kuwasaidia wananchi wa maeneo haya katika kuchimba mabwawa ya samaki ili wananchi hawa wawekeza kuuza samaki hizo kuwasaidia kwa ajili ya kuwapeleka watoto wao shuleni? Ahsante.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri alielezea kuhusu masuala ya kimkakati ambayo ni lazima tuyashughulikie katika kuendesha hifadhi hizi na kutokana na mabadiliko ambayo yametokea katika maeneo ya mipaka ya hifadhi zetu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala hili ni moja ya masuala ya mkakati na tutajadiliana na wananchi na hasa kwenda kabisa katika maeneo hayo ili tukubaliane na wananchi namna ya kutumia maeneo hayo ya kuvua na pale inapowezekana tuwasaidie wananchi kuwa na mabwawa yao wenyewe ili kusiwe na sababu yao kwenda ndani ya hifadhi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu nitaleta kwenu matangazo kadhaa kabla hatujaendelea na ratiba. Tangazo la kwanza linahusu wageni wapo wageni ambao wako jukwaa la Spika na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango wakiongozwa na Dkt. Likwelile, Katibu Mkuu Hazina, karibu sana shemeji huyu ni mume wa Mheshimiwa Vicky Kamata. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Dorothy Mwanyika ambaye ni Kaimu Katibu Mkuu Hazina, sasa ambalo tangazo hili linasema Kaimu lakini naona Katibu Mkuu keshatangazwa nadhani ni Naibu ama namna hiyo. Lakini tunaye pia Ndugu James Dotto, Naibu Katibu Mkuu Hazina, Ndugu Amina Shaban, Naibu Katibu Mkuu Hazina. Tunaye pia Ndugu Florence Mwanri Kaimu Katibu Mtendaji Tume ya Mipango. Wapo pia Manaibu Katibu Watendaji kutoka Tume ya Mipango, Makamishina kutoka Wizarani, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wakurugenzi na watumishi wengine wa Wizara ya Fedha wasimame wote kwa pamoja. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge na kundi la kwanza ni wageni wawili wa Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Ndugu Tausi Likokola, ambaye ni mwanamitindo wa Kimataifa. Karibu sana Tausi Likokola pia nimepewa taarifa hapa na Mheshimiwa Nape kwamba mwanamitindo huyu ameamua kurudi kufanyia kazi zake nyumbani. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kwa sababu huko alikokuwa ameshafahamiana na wanamitindo wengi wa Tanzania na wa nje awataarifu tu kwamba Mheshimiwa Nape anawakaribisha hapa nchi wa nje na Watanzania pia warudi nyumbani. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wengine Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni sita kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakiongozwa na Profesa Mussa Asaad ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Profesa Mussa Asaad ameongoza na Ndugu Ketiness Msongwe ambaye ni Kaimu Afisa Masuuli, ameongoza pia na Ndugu Jasper Mero ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu. Hawa wameambatana pia na maafisa wake wengine watatu nadhani tumewaona pale walisimama. *(Makofi)*

Pia wageni watano wa Mheshimiwa Mussa Rashid Ntimizi ambao ni viongozi wa TALGWU kutoka Mkoa wa Tabora ambao ni Ndugu Beatus Mlolwa ambaye ni m-NEC wa CCM Uyui, yupo pia Ndugu Razaki Irumba - Mwenyekiti TALGWU Wilaya ya Uyui, yupo pia Ndugu Haruna Msoga - Mwenyekiti TALGWU Tabora, yuko pia Ndugu Njaa Kibwana - Naibu Katibu Mkuu TALGWU Taifa, yupo pia Ndugu Kongoni Wandimba - Afisa Utumishi TALGWU Taifa, karibuni sana.

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Allan Kiula ambao ni marafiki zake kutoka mjini Dar es Salaam, Ndugu Shizya Sineda na Ndugu Alphonce Thobias, karibuni sana. Pia wageni 28 wa Mheshimiwa Mary Chatanda ambao ni walimu kutoka shule ya msingi Kilimani kutoka Korogwe wakiongozana na Ndugu Elias Mavoo, ambaye ni Afisa Elimu Taaluma, karibuni sana walimu wetu wote tumepita katika mikono yenu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Rita Kabati ambao ni wahadhiri na wanachuo kutoka Chuo Kikuu cha Iringa wakiongozwa na Ndugu Neema Mwamoto ambaye ni Mhadhiri Chuo Kikuu cha Iringa, karibuni sana. Tunao pia wageni 11 wa Mheshimiwa Doto Biteko ambao ni viongozi wa Chama cha Wafanyakazi Migodini kutoka Mgodi wa Geita yaani *GGM* kutoka Mkoa wa Geita wakiongozwa na Ndugu Gideon Kangolo ambao ni Mwenyekiti wa *TAMICO* na Ndugu Hassan Ameir ambaye ni Katibu Mkuu *TAMICO* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula anayetokea Nyamagana, Mkoani Mwanza ambaye ni Ndugu Halid Mashashi karibu sana. Pia wageni watatu wa Mheshimiwa Amina Makilagi ambao ni watoto wake wanaotokea Kahama, Mkoani Shinyanga na hawa ni Ndugu Tatu Said, Amina Said na Leila Said, karibuni sana mabinti zetu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 84 wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni wachungaji na waimbaji wa KKKT kutoka Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Mchungaji Thadei Kiwaga ambaye ni Mchungaji Kiongozi na Mchungaji Shukuru Stephen ambaye pia ni Mchungaji Kiongozi hawa wameongozana na mwalimu Lupiyana Samweli, karibuni sana wageni wetu. Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Abdallah Chikota ambao ni wajumbe wa Umoja wa Banguaji Wadogo wa Korosho Tanzania wanaotokea Mkoani Mtwara wakiongozwa na Mama Tumpale Magehema ambaye ni Mwenyekiti wao, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 26 wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni wana maombi kutoka Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Mchungaji Barikieli Joel ambaye ni Mchungaji Kiongozi karibu sana viongozi wetu. Pia wageni 26 wa Mheshimiwa Pascal Haonga wanaotokea Mbozi, Mkoani Mbeya wakiongozwa na Mchungaji Sanga, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na kundi la kwanza ni wanafunzi 48 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma kilichopo Mkoani Dodoma, karibuni sana wageni wetu. Tunao pia wanafunzi wanne kutoka shule ya msingi Martin Luther iliyopo mjini Dodoma, karibuni sana, pia wapo wanafunzi sita ambao ni wahitimu wa kidato cha sita kutoka shule mbalimbali zilizopo Mkoani Dodoma wakiongozwa na Bi. Aisha Msantu, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia Mwalimu Ndugu Iddi Kutua, kutoka shule ya msingi Sua - Handeni ambao ameambatana na wanakijiji wawili kutoka Kijiji cha Mwembe Wilaya ya Same, Kilimanjaro ambao ni Ndugu Hadia Kutua na Ndugu Mwanaidi Kutua, karibuni sana wageni wetu. Yupo pia mgeni wa Desderius John Mipata, huyu ni Mbunge wa Nkasi Kusini na anaitwa Joshua Mwimazi nadhani jina lake lilichelewa, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo ya wageni yapo matangazo mengine hapa ya kazi. Kamati ya Katiba na Sheria leo tarehe 8 Juni wanatarajiwa ama wanapaswa kukutana hapa tangazo linasema ukumbi wa Msekwa kuanzia saa tano, lakini hii saa tano nadhani tutakuwa tunasikiliza hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango. Kwa hiyo, nadhani muda Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii uwasiliane na Wajumbe wako mkutane saa ngapi kwa sababu saa tano inabidi ibaki mbaki humu ndani. Kuna tangazo lingine la

kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji *(PIC),* tangazo linasema kesho tarehe 9 Juni, 2016 kutakuwa na kikao kuanzia saa tano ukumbi wa Hazina mnaombwa mfike bila kukosa tangazo limeletwa na Mwenyekiti wenu hili ni la kesho.

Tangazo lingine Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ambaye ni Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkao wa Morogoro anawatangazia Wabunge wote wa Mkoa wa Morogoro baada ya kusitisha shughuli za Bunge leo, mkutane, hajasema mkutane wapi, lakini nadhani mkimuona yeye mahali aliposimama hapo nje mtaweza mkutane wapi ama urahisi ni kusimama mbele ya Ukumbi wa Pius Msekwa pale mtapata chumba cha mkutano.

Tangazo lingine ni Wabunge wote wanaotoka Mkoa wa Njombe wanaombwa kukutana na Mwenyekiti wao na yeye amesema pale hotelini nadhani alimaanisha kantini, mara baada ya kusitishwa shughuli za Bunge mchana huu. Kwa hiyo, Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Njombe anahitaji kukutana na Wabunge wote kutoka Mkoa huo kantini.

Waheshimiwa Wabunge, yapo matangazo mengine mnatangaziwa kutoka Ofisi ya Bunge kwamba leo kuanzia saa kumi jioni kutakuwa na uwasilishwaji wa hotuba ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kutokana na tukio hilo mialiko ya wageni watakaohudhuria itazingatia orodha ya wageni walioalikwa. Hivyo basi, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kuwasihi wageni wenu ambao hawana mwaliko kuwa hawatashiriki tukio hilo kwa kuingia Bungeni leo jioni. Hata hivyo fursa ya wao kutembelea Bunge ipo asubuhi hii na watatakiwa kuondoka maeneo ya Bunge ifikapo saa sita mchana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho linatoka kwa Mheshimiwa Leonidance Tutubert Gama ambaye huyu ni kocha maarufu wa timu ya kuvuta kamba, yeye anawatangazia Wabunge wote wanaotaka kuingia kwenye mchezo wa kuvuta kamba waanze kujiorodhesha kwa ajili ya mazoezi yanayotegemewa kuanza mwishoni mwa wiki hii na watajiorodhesha kwake, anakaa pale nyuma nadhani wote tunajua anakaa wapi. Kwa hiyo, tafadhali mchezo huu unahitaji wachezaji kama Mheshimiwa Gama, kwa hiyo tafadhali mkajiandikishe ili tuweze kushinda vizuri. *(Makofi)*

La mwisho, Waheshimiwa Wabunge nimepata taarifa kwamba jana wakati Mheshimiwa Oliver Semuguruka alipouliza swali lake la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swali hilo alisema yeye ni Mbunge wa Viti Maalum, Mwanza, sasa naagiza kwamba Taarifa Rasmi za Bunge zibadilishe kwa sababu yeye anatoka Kagera na siyo Mwanza. Kwa hiyo, Taarifa Rasmi za Bunge zirekebishe kwa kufuata marekebisho hayo, badala ya Mwanza iandikwe Kagera. Tunaendelea, Katibu.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbogo Mwongozo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) sina haja ya kusoma kwa ajili ya kuokoa muda. Lakini vilevile naomba nirejee na Kanuni ya 44(4), Kanuni ya 45(3), Kanuni ya 46(3) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(3)(a).

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Kiti kilitunyima fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza kwa sababu ambayo haikuwa na uzito sana na wananchi wetu walishindwa kujua sisi Wabunge tunafanya nini. Lilikuwa ni swali Na. 320 la Mheshimiwa Rhoda Kunchela liliulizwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa lakini tuliomba nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza tukanyimwa na sababu iliyotolewa tuliona kwamba haina uzito kwamba Naibu Waziri alikuwa anajibu kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa maana siyo mhusika wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirejea kwenye hizi Kanuni na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulikuwa na fursa pia ya Mawaziri wengine kuweza kusaidia kujibu maswali ambayo yamejitokeza. Wakati huo huo siku za nyuma kama nne zilizopita Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo aliweza kujibu maswali ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo Waziri na Naibu Waziri hawakuwepo na maswali ya nyongeza yaliulizwa na alijibu kiufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwamba kwa kuwa ilitokea hivyo, je, ni halali kwa swali hilo kurudiwa na vilevile tuweze kuuliza maswali ya nyongeza ili tuwatendee haki wananchi ambao tumekuja kuwawakilisha katika hili Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza niseme hivi, huwa tunajaribu kurudia hili jambo kila wakati inapojitokeza fursa. Niwakumbushe mwongozo unaombwa kwa jambo lililotokea siku hiyo, siyo jana yake ama sehemu nyingine, litokee siku hiyo Bungeni, hilo ni la kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, la pili kuhusu maswali, Kanuni ya 44 inaongelea maswali ya nyongeza na nitakapomalizia nitawapa ushauri. Maswali ya nyongeza Kanuni zimeweka utaratibu kwamba hayatakiwi kuzidi mangapi lakini

haijasema ni lazima yaulizwe, tuelewane. Kanuni ya 44 imeweka ukomo wa maswali ya nyongeza lakini haijasema ni lazima kila swali la msingi liwe na maswali ya nyongeza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, kwa sababu nimeshaeleza kuhusu hilo jambo la kwanza, maswali ya nyongeza ni kweli yanatoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kuuliza mambo yanayohusu Majimbo yao ama wakati mwingine ya Taifa zima. Hata hivyo, kwa kadri inavyowezekana tujitahidi kuwa na maswali ya msingi kwa sababu ya nyongeza hutegemea muda, Waziri anatoa majibu marefu kiasi gani na pia mwenye swali la nyongeza anauliza maswali marefu kiasi gani, kwa sababu yule ndiyo ana haki ya kwanza ya msingi ya kuuliza swali la nyongeza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo niseme hivi, maswali yaliyojibiwa jana yaliyokuwa ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ndiye aliyejibu kwa niaba ya Waziri. Nirudi na nyuma kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ameshawahi kujibu maswali ya Wizara ya Elimu kwa niaba.

Tuwe tunakumbuka sawasawa, maswali ya nyongeza aliyoulizwa yalikuwa ni yale yanayotoka kwa yule aliyeuliza swali la msingi. Kwa hiyo, hutegemea kama Kiti kinaona ni busara Waziri huyo kuongezewa maswali mengine, huyo ambaye anajibu swali ambalo siyo la Wizara yake. Hizi Kanuni tuziangalie vizuri maswali yanaweza kujibiwa aidha na Waziri mwenye dhamana au Waziri mwingine yoyote. Kwa hiyo, suala la kwanza ni yule Waziri mwenye dhamana na ndiyo maana Naibu Waziri anapojibu anasema anajibu kwa niaba ya Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tuzielewe tu vizuri hizi Kanuni wala tusione kwamba Kiti kinataka kubana Wabunge wasiulize maswali, hapana. Unaangalia uhalisia wa swali lenyewe na yule anayehusika kutakiwa kujibu. Mtakumbuka siku zilizopita kumekuwa na mazingira ambayo Kiti kinaombwa mwongozo swali lisipojibiwa kikamilifu. Itakuwa siyo busara kuomba mwongozo kwa swali kutojibiwa kikamilifu kwa Waziri ambaye alikuwa anajibu kwa niaba ya Waziri. Kwa hiyo, tufike mahali tuwekane tu vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini niseme hata baada ya haya maelezo, katika mazingira haya sasa kwa sababu mimi ndiye niliyetoa hayo maelezo jana, ikiwa hujakubaliana na maamuzi ya Kiti, Kanuni ya tano (5) na wote tunazo hizi nakala, inakupa fursa ya kufuata utaratibu ambao upo kikanuni kwamba hukuridhika na maamuzi ya Kiti kwa mujibu wa Kanuni ili usijikute unaomba mwongozo unaambiwa huwezi kuomba mwongozo jambo ni la jana ama vipi.

Nimeamua tu nitoe haya maelezo lakini kama hukuridhika au Mbunge yeyote hakuridhika na maamuzi ya Kiti Kanuni ya tano (5) inakupa fursa ya wewe kuweza kulalamika kuhusu maamuzi ya Kiti ikiwa ni pamoja na hayo aliyoyasema Mheshimiwa Mbogo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea, Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/2017. Pamoja na hotuba hii nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017. Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango ninayowasilisha ndiyo msingi wa Bajeti ya Serikali itakayowasilishwa mchana huu kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuendelea kushiriki Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukiwa na afya njema, amani na utulivu. Napenda kutumia nafasi hii pia kukushukuru wewe pamoja na Spika mwenyewe lakini pia Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha majadiliano ya Mpango wa Maendeleo kwa umakini na umahiri mkubwa tangu ngazi ya mapendekezo ya Mpango huo mwezi Februari, 2016 na kupitisha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2016/2017 - 2020/2021 Aprili, 2016. Nashukuru pia kwa fursa hii ya leo ya kuwasilisha Hotuba ya Hali ya Uchumi 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wasaidizi wake wakuu; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa, Waziri Mkuu kwa uongozi wao mahiri pamoja na juhudi za dhati wanazoziweka katika kuiendeleza Tanzania ili iweze kufikia kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati mwaka 2025. Aidha, uongozi wao umedhihirisha dhamira ya wazi katika kupambana na ufisadi na ubadhirifu wa mali za umma. Juhudi hizi zinapaswa kuungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo kwa maoni na ushauri wao. Maelekezo na ushauri waliotupatia wakati wa kujadili mapendekezo ya Mpango pamoja na maoni ya Waheshimiwa Wabunge mwezi Februari, 2016 yametusaidia katika kuandaa hotuba hii na kuboresha Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango ninaouwasilisha hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017, yamezingatia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 mpaka 2020/2021 ambao ulizinduliwa jana. Pia yamezingatia sera na mikakati mbalimbali ya maendeleo ya kisekta, kikanda na Umoja wa Afrika, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na Hotuba ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ya kuzindua Bunge la Kumi na Moja. Aidha, maandalizi hayo yamezingatia maoni ya wadau mbalimbali zikiwemo Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na michango ya Waheshimiwa Wabunge walioitoa katika Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 ni mwaka wa kipekee kwa nchi yetu, Afrika na maendeleo ya kidunia kwa ujumla kwa sababu zifuatazo:-

Serikali ya Awamu ya Tano yenye kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu itaanza kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano pamoja na Mpango wake wa Kwanza wa Maendeleo wa mwaka mmoja 2016/2017; Mpango wa kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2011/2012 mpaka 2015/2016 ambao utafikia ukomo wake tarehe 30 Juni 2016; pia kuanza utekelezaji wa Ajenda ya Afrika ya 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ninayoiwasilisha imegawanyika katika maeneo makuu manne. Eneo la kwanza, ni maelezo kuhusu hali ya uchumi wa dunia na mwenendo wa uchumi wa Taifa kwa mwaka 2015. Eneo la pili, ni muhtasari wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2015/2016. Tatu, ni muhtasari wa mwelekeo wa uchumi wa Taifa kwa mwaka 2015/2017 na nne, ni maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mwenendo wa hali ya uchumi wa dunia 2015. Mwaka 2015 uchumi wa pato la dunia ulikuwa kwa asilimia 3.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimi 3.4 mwaka 2014. Hata hivyo, mwenendo huu wa ukuaji wa uchumi unatofautiana kati ya nchi zilizoendelea na

zinazoendelea. Ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea uliimarika kufikia asilimia 1.9 mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 1.8 mwaka 2014. Ongezeko hilo linatokana na uwepo wa bei za chini za nishati, kuimarika kwa soko la nyumba na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande kwa nchi zinazoendelea kasi ya ukuaji wa uchumi ilikuwa kwa asilimia nne mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.6 mwaka 2014. Hali hiyo ilitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi kwa nchi za China, Urusi, Brazil, Afrika Kusini kufuatia kuporomoka kwa bei ya bidhaa na mazao katika soko la dunia pamoja na masharti magumu ya upatikanaji wa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa mfumuko wa bei kwa mtumiaji wa mwisho duniani kwa mwaka 2015 uliendelea kupungua kutokana na kushuka kwa bei ya mafuta, kupungua kwa bei ya bidhaa na mahitaji ya bidhaa. Mfumuko wa bei kwa mtumiaji wa mwisho duniani ulipungua na kuwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kasi ya ongezeko la bei kwa nchi zilizoendelea ilipungua kutoka wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2014 hadi wastani wa asilimia 0.3 mwaka 2015. Hata hivyo, kasi ya mfumuko wa bei ya mtumiaji wa mwisho kwa kundi la nchi zinazoendelea iliendelea kubaki katika wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2015 kama ilivyokuwa mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa Taifa. Pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia saba mwaka 2015 sawa na kiwango cha ukuaji cha mwaka 2014. Ukuaji huu wa uchumi ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme kwa ajili ya matumizi ya shughuli mbalimbali ikiwemo uzalishaji wa viwandani, kuongezeka kwa uzalishaji wa saruji na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, shughuli za kiuchumi zilizokua kwa viwango vikubwa zilikuwa ni pamoja na ujenzi asilimia 16.8 na uchimbaji wa madini na mawe asilimia 9.1. Aidha, kilimo ambayo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi na kinaajiri zaidi ya asilimia 70 ya watu wote nchini kiliendelea kukua kwa kasi ndogo ya asilimia 2.3 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4 mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa shughuli za kilimo ambao hujumuisha mazao, ufugaji, misitu na uvuvi katika pato la Taifa ulikuwa asilimia 29 mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 28.9 mwaka 2014. Shughuli za viwanda na ujenzi zilichangia asilimia 24.3 katika pato la Taifa mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 23.2 mwaka 2014. Vilevile shughuli za utoaji huduma zilichangia

asilimia 40 katika pato la Taifa mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 40.9 mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, pato la wastani la kila mtu. Katika mwaka 2015 Tanzania ilikadiriwa kuwa na idadi ya watu milioni 47.3 na pato la Taifa lilikuwa shilingi bilioni 90,863.68. Aidha, wastani wa pato la kila mtu lilikuwa shilingi milioni 1,918,928 mwaka 2015 ikilinganishwa na shilingi 1,730,405 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 10.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, pato la wastani kwa kila mtu katika dola za kimarekani lilipungua kutoka dola za Kimarekani 4,047 mwaka 2014 hadi dola za Kimarekani 966.5 mwaka 2015 kutokana na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. Hivyo, ni dhahiri kuwa bado kunahitajika msukumo zaidi wa kuongeza ukuaji wa pato la Taifa ili kufikia lengo la Dira ya Maendeleo ya Taifa la kufikia wastani wa dola za Kimarekani 3,000 kwa kila mtu na kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati itakapofika mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa bei. Wastani wa mfumuko wa bei katika mwaka 2015 ulikuwa asilimia 5.6 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2014. Kupungua kwa mfumuko wa bei nchini kulichangiwa kwa kiwango kikubwa na kushuka kwa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia hapa nchini na utekelezaji madhubuti wa sera za bajeti na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za kuondoa umaskini. Katika kipindi cha 2015/2016, Serikali iliendelea kuratibu na kufuatilia hali ya umaskini nchini ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango wa kwanza wa maendeleo wa miaka mitano na MKUKUTA wa pili. Matokeo ya tathmini hiyo yameainishwa katika taarifa za utekelezaji wa mpango huo na MKUKUTA wa pili kwa kipindi cha miaka mitano 2010 - 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizo zilisambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge wakati nikiwasilisha mapendekezo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kwenye semina ya Waheshimiwa Wabunge mwezi Februari 2016. Tathmini hiyo imesaidia katika kubainisha vipaumbele vya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao pia umejumuisha masuala ya kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukua kwa pato la wastani la Mtanzania kutoka sh. 770,464.3 mwaka 2010 na kufikia sh. 1,918,928 mwaka 2015; kuongezeka kwa kasi ya kupungua kwa umaskini wa mahitaji ya msingi ambapo kati ya mwaka 2007 na 2012 umaskini ulipungua kwa asilimia 6.2 kutoka asilimia 34.4 hadi asilimia 28.2 ikilinganishwa na kupungua kwa kiwango cha asilimia 4.6 katika kipindi cha miaka 15 yaani kutoka asilimia 39 mwaka 1992 hadi kufikia asilimia 34.4 mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya hali ya umaskini kimaeneo iliyofanyika kwa kutumia takwimu za Sensa ya Watu ya mwaka 2012 na Utafiti wa Hali ya Kipato na Matumizi katika Kaya mwaka 2012 inaonesha matokeo chanya na kutofautiana kimkoa na kiwilaya. Mikoa mitano yenye ahueni ya umaskini wa kipato ni Dar es Salaam asilimia 5.2, Kilimanjaro asilimia 14.3, Arusha asilimia 14.7, Pwani asilimia 14.7 na Manyara asilimia 18.3. Mikoa mitano yenye umaskini mkubwa wa kipato ni Kigoma asilimia 48.9, Geita asilimia 43.7, Kagera asilimia 39.3, Singida asilimia 38.2 na Mwanza asilimia 35.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwilaya umaskini mkubwa upo katika Wilaya ya Kakonko Mkoani Kigoma na Biharamulo Mkoani Kagera ambapo takriban asilimia 60 ya idadi ya watu katika wilaya hizo wapo chini ya mstari wa umaskini na mahitaji ya msingi. Hii ina maana kuwa maeneo ya vijijini hususan pembezoni bado Watanzania wengi wanaishi katika lindi la umaskini na uwezo wao wa kupata mahitaji ya msingi ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nguvu kazi na ajira. Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi kwa mwaka 2014 ulionyesha kuwa nguvu kazi ya Taifa ilikuwa watu 25,750,116 sawa na asilimia 57 ya watu wote Tanzania Bara. Kati ya hao, wanawake walikuwa 13.3 sawa na asilimia 52, wanaume walikuwa milioni 12.3 sawa na asilimia 48. Vilevile utafiti huo ulionesha kuwa kati ya nguvu kazi iliyokuwepo, watu wenye uwezo wa kufanya kazi walikuwa milioni 22.3 na watu wasio na uwezo wa kufanya kazi walikuwa milioni 3.4. Aidha, sababu za watu wasio na uwezo wa kufanya kazi zilikuwa ni pamoja na ulemavu na ugonjwa wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi walioajiriwa walikuwa 20,030,139 na wasioajiriwa walikuwa watu 2,291,785. Kati ya walioajiriwa, wanawake walikuwa 9.8 sawa na asilimia 49.4 na wanaume walikuwa 10.1 sawa na asilimia 50.6. Watu wenye ajira Jijini Dar es Salaam walikuwa milioni 1.9 sawa na asilimia 9.6 na katika maeneo mengine ya mijini walikuwa milioni 5.1 sawa na asilimia 25.6 na maeneo ya vijijini walikuwa watu milioni 12.9 sawa na asilimia 64.8. Kutokana na utafiti huo ilibainika kuwa idadi kubwa ya kundi la watu walioajiriwa lilikuwa na umri kati ya miaka 35 na 64 ambayo ni asilimia 42.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti huo umeonesha kuwa vilevile kuna asilimia 77.8 ya nguvu kazi yote ya Taifa imeajiriwa au imejiajiri. Uwiano huo wa ajira na nguvu kazi unapima uwezo wa nchi kutoa ajira. Uwiano ulikuwa mkubwa maeneo ya vijijini ambapo ni asilimia 82.2 wakati Jiji la Dar es Salaam lilikuwa na uwiano mdogo wa asilimia 59.8. Aidha, wanaume walikuwa na uwiano mkubwa, asilimia 82.1 ukilinganisha na wanawake asilimia 73.8. Vilevile, uwiano ulikuwa mkubwa kwa kundi la watu wenye umri wa miaka 35-64 sawa

na asilimia 87.2 na mdogo zaidi kwenye kundi la miaka 65 na zaidi ambayo ni asilimia 56.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa afya, Utafiti wa Hali ya Afya ya Mama na Mtoto uliofanyika mwaka 2015 unaonesha vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja vimepungua kufikia 43 mwaka 2015 kutoka 51 mwaka 2010 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai. Vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano vimepungua kufikia 67 mwaka 2015 kutoka 81 mwaka 2010 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa damu kwa watoto chini ya miaka mitano umepungua kutoka asilimia 59 mwaka 2010 hadi 47 mwaka 2015. Aidha, kiwango cha upungufu wa chakula kwa watoto chini ya miaka mitano kimepungua kutoka asilimia nane mwaka 2010 na kufikia asilimia 34 mwaka 2015. Pia umri wa Mtanzania wa kuishi umeongezeka kutoka wastani wa miaka 51 mwaka 2001 hadi miaka 61 mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti huo pia unaonesha kuwa wastani wa idadi ya watoto kwa kila mama imepungua kutoka watoto 5.4 mwaka 2010 hadi watoto 5.2 mwaka 2015. Idadi wa wasichana wanaopata watoto katika umri wa kati ya miaka 15 na 19 imeongezeka kufikia asilimia 27 mwaka 2015 kutoka asilimia 23 mwaka 2010. Kuongezeka kwa wasichana wanaoanza kupata watoto katika umri mdogo (miaka 15 – 19) si dalili nzuri kwani inaashiria kuongezeka kwa utegemezi na kudumaza jitihada za kuondoa umaskini katika jamii yetu. Hivyo, ni muhimu Serikali, wazazi na wadau wote kushirikiana katika kuhakikisha watoto wengi wa kike wanapata elimu kuanzia shule za awali hadi sekondari na katika vyuo vya ufundi na elimu ya juu ili jitihada za kupambana na umaskini katika maeneo ya vijijini ziweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio hayo kwa pamoja yamechangia kupandisha Kipimo cha Maendeleo ya Binadamu *(Human Development Index)* kutoka 0.48 mwaka 2014 hadi 0.52 mwaka 2015. Vilevile yanaonesha kuwa kukua kwa uchumi kumechangia kasi ya kupungua kwa umaskini wa kipato na usio wa kipato ijapokuwa si kwa kasi iliyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuzaji rasilimali. Ukuzaji wa rasilimali umeongezeka kwa asilimia 5.4 kufikia shilingi milioni 25.3 mwaka 2015 kutoka shilingi milioni 24.0 mwaka 2014. Hata hivyo, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2007 ulipungua kwa asilimia moja na kufikia shilingi milioni 13.9 mwaka 2015 kutoka shilingi milioni 14.1 mwaka 2014. Uwiano wa ukuzaji rasilimali na pato la Taifa ulikuwa asilimia 27.9 mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 30.2 mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya nje. Mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma nje uliendelea kuimarika mwaka 2015 kama ilivyokuwa mwaka 2014, hususan kufuatia kupungua kwa thamani ya uagizaji wa mafuta ya petroli sambamba na kuongezeka kwa mapato ya mauzo ya bidhaa na huduma nje. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilikuwa dola za Kimarekani milioni 9,450 ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 8,717.4 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 8.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo asilia hususan bidhaa za viwandani. Kwa upande mwingine thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ilipungua kwa asilimia 7.8 kutoka dola za Kimarekani 13,586.5 mwaka 2014 hadi dola za Kimarekani milioni 12,528.2 mwaka 2015. Mwenendo huu ulichangia kuimarika kwa urari wa malipo ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Kimarekani milioni 1,063.3 mwaka 2015 ikilinganishwa na ziada ya dola za Kimarekani milioni 727.3 mwaka 2014 sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 46.2. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma za mawasiliano, usafirishaji na usafiri hususan biashara ya utalii na kupungua kwa malipo ya huduma za usafirishaji na huduma nyingine za kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2015 nchi zinazofanya biashara na Tanzania kwa kiwango kikubwa zilikuwa kama ilivyokuwa mwaka 2014. Nchi ambazo Tanzania iliagiza bidhaa zake kwa kiwango kikubwa zilikuwa ni Saud Arabia, China, India na Umoja wa Falme za Kiarabu ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 55.5 ya bidhaa zote zilizoagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya bidhaa zilizoagizwa na Tanzania kutoka Saud Arabia ni bidhaa za mafuta ya petroli wakati mitambo na bidhaa za kielektroniki hususan simu za mkononi ziliagizwa kutoka China. Aidha, Tanzania iliagiza magari, makaa ya mawe, juice na matunda kutoka India na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho nchi ambazo Tanzania iliuza bidhaa zake kwa kiwango kikubwa zilikuwa ni India, Kenya, Afrika ya Kusini na China ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 53.7 ya bidhaa zote zilizouzwa nje. Bidhaa zilizouzwa China na India ni pamoja na mbegu za mafuta, vito vya thamani, bidhaa za plastiki, dhahabu, mazao ya samaki na korosho. Kwa upande mwingine, bidhaa zilizouzwa Kenya ni chai, mahindi, maharage, vyandarua, mbogamboga na nafaka. Aidha, dhahabu, madini ya shaba, kahawa na chai ni baadhi ya bidhaa zilizouzwa Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya fedha, nikianza na thamani ya fedha ya Tanzania. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani ilishuka kwa wastani wa asilimia 16.8 mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 3.3 mwaka 2014. Dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi za Tanzania 1,985.4 mwaka 2015 ikilinganishwa na shilingi 1,652.5 mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuporomoka kwa thamani ya shilingi hususan katika robo ya nne (Oktoba - Desemba 2015) kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuimarika kwa dola ya Marekani, kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha za kigeni kwa ajili ya bajeti ya Serikali pamoja na mapato kidogo ya fedha za kigeni yasiyokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, amana katika benki za biashara. Amana katika benki za biashara ziliongezeka kwa asilimia 18.4 mwaka 2015 na kufikia shilingi bilioni 19,149.4 kutoka shilingi bilioni 16,177.8 mwaka 2014. Kati ya hizo, sekta binafsi ilichangia shilingi bilioni 18,292.5 ambazo ni sawa na asilimia 95.5 ya amana zote. Aidha, amana za fedha za kigeni na amana za akiba na za muda maalum zilichangia sehemu kubwa ya amana zote kwenye benki za biashara mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwiano wa amana za fedha za kigeni katika amana zote uliongezeka na kufikia asilimia 32.9 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 28.8 mwaka 2014. Aidha, uwiano wa amana za akiba na za muda maalum ulikuwa wastani wa asilimia 32.4 mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya benki za biashara kwa shughuli za kiuchumi. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 24.8 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 19.4 mwaka 2014. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kupungua kwa ukuaji wa madai rasmi kwa Serikali. Madai rasmi kwa Serikali Kuu yalikua kwa asilimia 33.8 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 42.9 mwaka 2014. Aidha, thamani ya mikopo iliyotolewa kwa sekta binafsi ilikuwa sawa na asilimia 17.3 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 15.6 katika mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa mikopo kwenye shughuli za uchukuzi na mawasiliano, mikopo kwa watu binafsi na shughuli za viwandani uliongezeka mwaka 2015 ikilinganishwa na mwaka 2014. Katika kipindi hicho, sehemu kubwa ya mikopo ilielekezwa kwenye shughuli za biashara ambazo zilipata wastani wa asilimia 20.2 ya mikopo yote ikifuatiwa na shughuli za watu binafsi (asilimia 18.0).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa viwango vya riba. Viwango vya riba za amana na za mikopo viliongezeka mwaka 2015 ikilinganishwa na viwango vya mwaka 2014. Riba ya mikopo kwa ujumla iliongezeka kutoka wastani wa asilimia 15.75 Desemba, 2014 hadi wastani wa asilimia 16.41

Desemba, 2015. Riba za amana za muda maalum ziliongezeka kutoka wastani wa asilimia 8.76 Desemba, 2014 hadi wastani wa asilimia 9.22 Desemba, 2015. Kiwango cha riba za amana za mwaka mmoja kiliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 11.08 Desemba, 2015 kutoka wastani wa asilimia 10.66 Desemba, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, riba ya mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kutoka wastani wa asilimia 14.8 Desemba, 2014 hadi wastani wa asilimia 14.22 Desemba, 2015. Kutokana na mwendo huu, tofauti kati ya riba za amana na za mikopo za mwaka mmoja ilipungua kutoka wastani wa asilimia 4.14 Desemba, 2014 hadi wastani wa asilimia 3.14 Desemba, 2015. Kwa upande mwingine riba katika soko la fedha baina ya benki zilipungua na kuwa wastani wa asilimia 7.29 Desemba, 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 11.82 Desemba, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, riba kwenye dhamana za Serikali zilikuwa wastani wa asilimia 18.25 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 15.73 mwaka 2014. Aidha, mauzo ya dhamana za Serikali yalipungua kwa asilimia 8.5 kutoka mauzo yenye thamani ya shilingi bilioni 3,535.7 mwaka 2014 hadi shilingi bilioni 3,235.3 mwaka 2015. Mauzo ya hati fungani mwaka 2015 yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 924.6 kutoka shilingi bilioni 916.7 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 0.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato na matumizi ya Serikali. Katika mwaka 2015/2016, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 22.49 kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Katika mwaka 2015/2016, Serikali ililenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi bilioni 13.47 sawa na asilimia 14.3 ya Pato la Taifa. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, makusanyo ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 11,481.4 sawa na asilimia 99 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 11,550.8 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 10,170.1 sawa na asilimia 100 ya lengo na mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 967.2 sawa na asilimia 105 ya lengo. Vilevile mapato ya halmashauri yalikuwa shilingi bilioni 344.1 sawa na asilimia 79 ya lengo kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015/2016, Serikali ilikadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 22,495.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 16,576.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 5,909.1 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 16,856.9 sawa na asilimia 90 ya lengo katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 13,647.1 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3,209.8 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa sekta binafsi. Uwekezaji wa moja kwa moja nchini kutoka nje umeendelea kuongezeka ambapo katika kipindi cha miaka mitano iliyopita thamani ya uwekezaji wa moja kwa moja nchini iliongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni 1,229 mwaka 2011 hadi dola za Kimarekani milioni 2,142 mwaka 2014. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa mazingira ya kufanya biashara nchini pamoja na sera na sheria imara za kuvutia uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Urahisi wa Kufanya Biashara ya Benki ya Dunia ya mwaka 2015, Tanzania ilipanda kwa nafasi moja katika vigezo vya urahisi wa kufanya biashara kwa kushika nafasi ya 139 kati ya nchi 189 duniani ikilinganishwa na nafasi ya 140 mwaka 2014, hali hii hairidhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, pamoja na jitihada zilizoanza za kuboresha taratibu za upatikanaji wa vibali vya ujenzi na huduma za biashara kupitia vituo vya pamoja vya utoaji huduma mipakani ni muhimu kuongeza nguvu zaidi katika kushughulikia kero za uwekezaji na za wafanyabiashara hapa nchini hususan kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika, kuharakisha utoaji wa maamuzi, kuboresha mfumo wa kodi na sera ili viwe vya kutabirika na kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina ya Hali ya Uchumi wa Taifa yapo katika kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2015/2016. Katika mwaka 2015/2016, Serikali ilitenga shilingi trilioni 5.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa shilingi trilioni 4.2 na fedha za nje zilikuwa shilingi trilioni 1.6. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri ni shilingi bilioni 739.4 ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 595 na fedha za nje ni shilingi bilioni 144.4. Kwa upande wa Wizara, Taasisi, Wakala na Idara zinazojitegemea zilitengewa shilingi trilioni 5.1 ambapo fedha za ndani ni shilingi trilioni 3.65 na fedha za nje ni shilingi trilioni 1.51.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa hadi Aprili, 2016 ni shilingi trilioni 3.2, kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi trilioni 2.8 na fedha za nje ni shilingi bilioni 398.8. Fedha hizo za maendeleo zilizotolewa ni sawa na asilimia 65 ya lengo la shilingi trilioni 4.92 hadi Aprili, 2016. Fedha za ndani zilizotolewa ni sawa na asilimia 79 ya lengo la shilingi trilioni 3.53 na fedha za nje zilizotolewa ni sawa na asilimia 29 tu ya lengo la shilingi trilioni 1.38.

Miradi iliyokamilika mwaka 2015/2016. Kwa kuwa taarifa za mafanikio ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na changamoto zake zilishaelezwa kwa kina katika hotuba za kisekta zilizotangulia, naomba nitaje baadhi tu ya miradi

ya maendeleo iliyokamilika kama kielelezo cha mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa 2015/2016.

(i) Ujenzi wa madaraja ya Kigamboni, Maligisu, Nangoo, Mbutu na Ruhekei katika barabara kuu; *(Makofi)*

(i) Ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam (kilomita 542); *(Makofi)*

(ii) Ujenzi wa mitambo ya kuchakata gesi katika maeneo ya Madimba na Songosongo; *(Makofi)*

(iii) Ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi vya Somanga – Fungu na Kinyerezi; *(Makofi)*

(iv) Usimikaji wa mitambo minne ya kufua umeme Kinyerezi I yenye uwezo wa kuzalisha *MW* 150 na kuanza uzalishaji wa umeme; *(Makofi)*

(v) Awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini na hivyo kuunganisha wateja 61,023 wa awali kati ya wateja 250,000; *(Makofi)*

(vi) Kukamilika kwa awamu ya Pili ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (kilomita 25,954) na kusambazwa katika mikoa 24 Tanzania Bara; *(Makofi)*

(vii) Kukamilika kwa mradi wa Maji wa Ruvu Chini (Pwani); na *(Makofi)*

(viii) Kukamilika kwa miradi mipya 1,160 ya maji ya vijiji 10 katika vijiji 1,206 yenye vituo 28,499 vya kuchotea maji katika Halmashauri 148. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine katika maeneo ya kipaumbele ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo yapo katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017, Sura ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto na hatua zilizochukuliwa. Katika mwaka 2015/2016, kumejitokeza changamoto mbalimbali katika kutekeleza mpango ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi, ulipaji wa fidia kwa wakati, taratibu na gharama za ununuzi wa umma, madeni ya wakandarasi hususan ya ujenzi wa barabara, upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji, utegemezi wa bajeti ya maendeleo, ushiriki mdogo wa sekta binafsi, mazingira

yasiyowezeshi katika uwekezaji na uendeshaji biashara na uhaba wa miundombinu ya kuwezesha utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto hizo, ikiwemo kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha hasa kwa ajili ya miradi ya Matokeo Makubwa Sasa na miradi ya Kitaifa ya kimkakati, kuendelea kuimarisha miundombinu wezeshi katika maeneo ya miradi ya maendeleo na kupunguza madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya viwanda nchini. Mchango wa sekta ya uzalishaji viwandani katika pato la Taifa kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita ni wastani wa asilimia saba ambapo uliongezeka kutoka asilimia 6.6 mwaka 2005 hadi asilimia 7.3 mwaka 2015. Kwa mujibu wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 Tanzania ina jumla ya viwanda 50,656 ambavyo vipo katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivyo vinajumuisha viwanda vya kati na vikubwa 1,769 sawa na asilimia 3.5 ambavyo vinaajiri wafanyakazi 10 na kuendelea na viwanda vidogo 48,887 sawa na asilimia 96.5, ambavyo vinaajiri mfanyakazi mmoja hadi wafanyakazi tisa. Takribani ajira 231,176 zimetengenezwa kutokana na viwanda hapa nchini ambapo viwanda vikubwa na vya kati, vimetoa ajira 107,732 na viwanda vidogo vilitoa ajira 123,364.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikoa inayoongoza kwa idadi kubwa ya viwanda ni Dar es Salaam ambayo ina viwanda 516 sawa na asilimia 29.2, Arusha ina viwanda 144 sawa na asimilia 8.1, Shinyanga viwanda 101 sawa na asilimia 5.7, Kilimanjaro viwanda 96 sawa na asilimia 5.4 na Mwanza viwanda 88 sawa na asilimia 5.0.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile aina ya viwanda vingi vilivyopo nchini ni vya uzalishaji wa vyakula ambavyo viko viwanda 20,228 sawa na asilimia 39.9, mavazi viwanda 13,758 sawa na asilimia 27.2, viwanda vya samani 7,071 sawa na asilimia 14. Hata hivyo, zipo fursa zaidi katika viwanda vingine ambavyo utafiti ulionesha viwanda vyake viko vichache nchini kama vile nguo 817, TEHAMA vitatu, mashine na vifaa 30, madawa tisa, ngozi 216, kemikali 102 na vifaa vya umeme 269.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubinafsishaji wa viwanda. Katika kukidhi mahitaji ya soko huria na ushindani wa kibiashara, viwanda 106 vilibinafsishwa kwa lengo la kuongeza ufanisi, uzalishaji, ajira, kupunguza uagizaji wa bidhaa nchini na kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi. Kati ya viwanda vilivyobinafsishwa, uzalishaji katika viwanda 34 umekuwa wa ufanisi na hivyo kuongeza ajira na mapato ya kodi kwa Serikali. Aidha, viwanda 33 vinaendeshwa kwa hasara na

viwanda 39 vilivyokuwa vinazalisha bidhaa mbalimbali kama ngozi, chuma, korosho, zana za kilimo, sabuni, mafuta ya kupikia vimefungwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa zinazokabili viwanda vilivyobinafsishwa ni pamoja na mtaji, teknolojia, malighafi na upatikanaji wa umeme wa uhakika, maji na masoko. Aidha, baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa vilitumika kama dhamana ya kupata mikopo ya benki na kugharamia shughuli nyingine badala ya uendelezaji wa viwanda na hivyo kuwa na madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya kuendeleza viwanda nchini. Katika kutekeleza kwa vitendo dhima ya ujenzi wa uchumi wa viwanda, mpango huu pamoja na mambo mengine utajikita katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuendeleza viwanda vikubwa, vya kati, vidogo na vile vilivyobinafsishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kulipa fidia kwa maeneo maalum ya uwekezaji na kuweka miundombinu wezeshi itakayovutia sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vikubwa; kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini ili kuinua nafasi ya Tanzania katika ushindani wa kibiashara; kuendelea kuboresha miundombinu ya msingi kuwezesha maendeleo ya viwanda nchini hasa miradi ya nishati ya umeme, maji, barabara, reli na bandari na kuboresha sekta ya fedha ili iweze kutoa mitaji ya kuendeleza viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine ni pamoja na kusimamia kikamilifu uingizwaji wa bidhaa zinazozalishwa na viwanda hapa nchini; kuendeleza miundombinu ya *SIDO* ili kuvutia viwanda vidogo; kuweka mikakati madhubuti ya kuwainua wajasiriamali wadogo na wa kati ili waweze kuzalisha kwa ufanisi; kuboresha mazingira ya biashara nchini ikiwa ni pamoja kufuta kodi na tozo ambazo ni vikwazo kwa wajasiriamali wadogo; kuanzisha kongane za viwanda (*industrial clusters)* za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi kupitia elimu na mafunzo ya kuendesha na kuendeleza viwanda, ujasiriamali na uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutathmini kwa kina viwanda vyote vilivyobinafsishwa ili kuandaa mikakati ya kuviendeleza; kupitia mikataba yote ya ubinafsishaji na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria; kufufua viwanda vilivyobinafsishwa na kuviendeleza kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na kuchukua hatua kuhusu uagizwaji wa bidhaa zinazozalishwa na viwanda hapa nchini ili ziweze kukua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu hali ya viwanda nchini yapo katika kitabu cha Mpango Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017, Sura ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa uchumi 2016. Katika mwaka 2016/2017, shabaha na malengo ya uchumi jumla na bajeti ni kama ifuatavyo:-

(i) Pato halisi la Taifa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2016 toka asilimia 7.0 mwaka 2015;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 5.0 na asilimia 8.0 mwaka 2016;

(iii) Mapato ya ndani ukijumuisha mapato ya Halmashauri kufikia asilimia 14.8 ya pato la Taifa mwaka wa 2015/2016 na kuendelea kuongezeka kufikia asilimia 16.9 ya pato la Taifa mwaka 2016/2017;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.8 ya pato la Taifa mwaka 2016/2017 kutoka asimilia 12.6 ya pato la Taifa mwaka 2015/2016;

(v) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 23.2 ya pato la Taifa mwaka 2015/2016 hadi asilimia 27 mwaka 2016/2017;

(vi) Nakisi ya bajeti inakadiriwa kuwa asilimia 4.5 ya pato la Taifa mwaka 2016/2017 kutoka makadirio ya bajeti ya asilimia 4.2 mwaka 2015/2016;

(vii) Nakisi katika urari wa malipo ya kawaida kuwa asilimia 7.9 ya pato la Taifa mwaka 2015/2016 na kupungua hadi asilimia 7.5 mwaka 2016/2017; na

(viii) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne ifikapo mwezi Juni, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017: Maeneo ya kipaumbele. Miradi ya maendeleo ya kipaumbele katika mwaka 2016/2017 imegawanyika katika makundi manne. Kwanza, ni viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda. Pili, ni kufungamanisha maendeleo ya uchumi na rasilimali watu. Tatu, mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji na nne, ni usimamizi wa utekelezaji wa mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ifuatayo:-

Mradi wa Magadi Soda, Bonde la Engaruka, Arusha; mradi wa kufufua kiwanda cha *General Tyre,* Arusha; uendelezaji wa viwanda vidogo vya *SIDO* katika maeneo ya viwanda (*industrial park)* ya Mwanza, Dar es Salaam, Mbeya na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi itakayotekelezwa katika eneo la kufungamanisha maendeleo ya uchumi na rasilimali watu ni pamoja na ifuatayo:-

Kuimarisha mifumo, majengo na miundombinu mingine katika shule za awali, msingi na sekondari; upanuzi na ujenzi wa vyuo vikuu; ukarabati, upanuzi na ujenzi wa vyuo vya ualimu; ukarabati na upanuzi wa ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi; mradi wa kuboresha hospitali za rufaa; Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*; Hospitali ya Magonjwa ya Kuambukiza Kibong'oto; kuanzisha programu ya uzalishaji ajira na programu ya maendeleo ya ujuzi; na mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji, Serikali itaendelea kutekeleza miradi iliyoanza kutekelezwa katika kipindi cha Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ikiwa ni pamoja na miradi katika maeneo yafuatayo:-

Nishati ikiwemo mradi wa *Liquified Natural Gas;* kilimo cha mazao; mifugo; uvuvi; misitu; maji; miundombinu ya reli na barabara hususan barabara ya Kidahwe – Nyakanazi; barabara ya Masasi – Newala – Mtwara; barabara ya Mbinga - Mbamba Bay na barabara ya Tabora – Ipole – Koga - Mpanda; bandari hususan bandari ya Dar es Salaam; Bagamoyo na Mtwara; usafiri wa anga na usafiri wa majini na TEHAMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali itaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango kwa lengo la kurekebisha upungufu uliojitokeza katika utekelezaji wa mipango na programu mbalimbali za maendeleo. Dhamira ya Serikali ni kuongeza kasi katika kutanzua vikwazo vya utekelezaji na kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango kwa kurekebisha taratibu zitakazosaidia na kuongeza ufanisi wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017 umeainisha miradi mikubwa ya kielelezo ambayo itapewa msisitizo katika utekelezaji wake**.** Miradi hii ni mahsusi kwa

maana ya ukubwa wa uwekezaji na matokeo tarajiwa. Miradi hiyo ni pamoja na ifuatayo:-

Mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma; mradi wa chuma Liganga; ujenzi wa reli mpya ya Kati Dar es Salaam – Kigoma na Tabora – Mwanza na matawi yake Isaka mpaka Kigali/Keza – Musongati na Kaliua - Mpanda kwa kiwango cha *standard gauge;* uboreshaji wa usafiri katika maziwa makuu ikiwa ni pamoja na ununuzi wa meli moja mpya ya usafirishaji wa abiria na mizigo katika Ziwa Victoria na ukarabati wa meli ya *MV Victoria*, *MV* Butiama na *MV* Liemba; na kuimarisha Shirika la Ndege la Taifa *(ATCL)* ikijumuisha ununuzi wa ndege tatu mpya moja ikiwa ni *Bombardier CS300* yenye uwezo wa kubeba abiria 100 - 150 na ndege mbili *Bombardier Q400* zenye uwezo wa kubeba abiria 67 - 88 kila moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya kushirikisha sekta binafsi. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017, utategemea zaidi ushiriki mkubwa wa sekta binafsi. Hivyo, Serikali imeweka mikakati ya kujenga na kuboresha miundombinu wezeshi; kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara na kuhamasisha ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada mahsusi za Serikali katika eneo hili ni pamoja na kuongeza kasi ya kulipa fidia katika Maeneo Maalum ya Uwekezaji *(EPZs* na *SEZs);* Benki ya Rasilimali Tanzania kuongeza utoaji wa mikopo katika sekta mbalimbali kutoka shilingi bilioni 538.7 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 726.9 mwaka 2016; kuiwezesha Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili iweze kupanua huduma zake ziwafikie wananchi; na kuwezesha Kituo cha Uwekezaji Tanzania kuwa na ardhi yenye hati miliki kwa ajili ya kuikodisha kwa wawekezaji wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu utahusisha utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kwa njia ya ubia ili kuendelea kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi. Miongoni mwa miradi itakayotekelezwa kwa ubia ni pamoja na ujenzi wa Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini; miradi ya Chuma - Liganga na Makaa ya Mawe – Mchuchuma; na mradi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro *Express Way*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu miradi ya kipaumbele yapo katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Sura ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugharamiaji wa Mpango. Serikali imetenga shilingi trilioni 11.8 sawa na asilimia 40 ya bajeti yote ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, fedha za ndani ni shilingi trilioni 8.7 sawa na asilimia 74 ya bajeti ya maendeleo na fedha za nje ni shilingi trilioni 3.1 sawa na asilimia 26 ya bajeti ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta binafsi inatarajiwa kuwekeza kiwango kikubwa cha fedha ili kuanzisha na kuendeleza viwanda ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango. Kwa ujumla, fedha za maendeleo zimeelekezwa zaidi katika miradi inayolenga kuendeleza viwanda kama vile uchukuzi, ujenzi, nishati, kilimo, maji, elimu na afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu ugharamiaji wa Mpango yapo kwenye Kitabu cha Mpango, Sura ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa. Wizara na taasisi za umma zinahusika moja kwa moja katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo katika maeneo yao na kutoa taarifa za utekelezaji kwa kila robo mwaka na mwaka mzima. Taarifa za ufuatiliaji na tathmini za miradi ya maendeleo zitawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaratibu ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo itakayotekelezwa katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zitakuwa na jukumu la kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya Kitaifa ya kimkakati na ya sekta binafsi kwa lengo la kubaini changamoto zinazokabili miradi hiyo na kuzitafutia ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa yako katika Kitabu cha Mpango, Sura ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Kabla ya kumaliza hotuba yangu, napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Wakuu wa Idara za Serikali na Taasisi zinazojitegemea kwa ushirikiano wao wakati wote wa maandalizi ya kutayarisha Taarifa ya Hali ya Uchumi 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Servacius Likwelile kwa kusimamia vizuri kazi za kila siku na maandalizi ya Taarifa ya Hali ya Uchumi 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/2017 na hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana katika hali ya uchumi na utekelezaji wa Mpango yamechangiwa na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wakiwemo nchi marafiki, washirika wa maendeleo, sekta binafsi na

wananchi wote. Kwa niaba ya Serikali, nawashukuru wadau hao kwa michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Hotuba hii na vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi, 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/2017 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango *www.mof.go.tz* na *www.mipango.go.tz*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge wapokee, wakubali kujadili na kupitisha Taarifa hii ya Hali ya Uchumi 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono lakini inaendelea mpaka baadaye tutakapoanza mjadala baada ya kusomwa kwa bajeti ya Serikali.

HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA UCHUMI 2015 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2016/17

UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17. Pamoja na hotuba hii nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17. Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango ninayowasilisha ndio msingi wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuendelea kushiriki Mkutano wa Tatu wa Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukiwa na afya njema, amani na utulivu. Napenda kutumia nafasi hii pia kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha majadiliano ya Mpango wa Maendeleo kwa umakini na umahiri mkubwa tangu ngazi ya mapendekezo ya Mpango huo Februari, 2016 na kupitisha Mpango

wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21, Aprili 2016. Nashukuru pia kwa fursa hii ya leo ya kuwasilisha hotuba ya Hali ya Uchumi 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17.

3. Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wasaidizi wake wakuu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu, kwa uongozi wao mahiri pamoja na juhudi za dhati wanazoweka katika kuiendeleza Tanzania ili iweze kufikia kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati mwaka 2025. Aidha, uongozi wao umedhihirisha dhamira ya wazi katika kupambana na ufisadi na ubadhirifu wa mali za umma. Juhudi hizi zinapaswa kuungwa mkono na Waheshimiwa wabunge na Wananchi wote kwa ujumla.

4. Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo kwa maoni na ushauri wao. Maelekezo na ushauri waliotupatia wakati wa kujadili Mapendekezo ya Mpango pamoja na maoni ya Waheshimiwa Wabunge Februari, 2016 yametusaidia katika kuandaa hotuba hii na kuboresha taarifa za Hali ya Uchumi na Mpango ninaowasilisha leo.

5. Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 yamezingatia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21) uliozinduliwa jana. Pia, yamezingatia sera na mikakati mbalimbali ya maendeleo ya kisekta, kikanda (EAC na SADC) na Umoja wa Afrika; Malengo ya Maendeleo Endelevu, 2030; Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015; na Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuzindua Bunge la 11. Aidha, maandalizi hayo yamezingatia maoni ya wadau mbalimbali zikiwemo Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na michango ya Waheshimiwa Wabunge waliyoitoa katika Mkutano wa Pili wa Bunge la 11.

6. Mheshimiwa Spika, mwaka 2016 ni mwaka wa kipekee kwa nchi yetu, Afrika na maendeleo ya kidunia kwa ujumla kwa sababu zifuatazo: Serikali ya Awamu ya Tano yenye kauli mbiu ya HAPA KAZI TU kuanza kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) pamoja na Mpango wake wa kwanza wa maendeleo wa mwaka mmoja 2016/17; Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) kufikia ukomo wake tarehe 30

Juni, 2016; kuanza utekelezaji wa Agenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

7. Mheshimiwa Spika, hotuba ninayowasilisha imegawanyika katika maeneo makuu manne (4): kwanza ni maelezo kuhusu Hali ya Uchumi wa Dunia na Mwenendo wa Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2015; pili ni Muhtasari wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2015/16; tatu ni Muhtasari wa Mwelekeo wa Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016/17 na nne ni Maeneo ya Kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17.

MWENENDO WA HALI YA UCHUMI 2015

Uchumi wa Dunia

8. Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 ukuaji wa Pato la Dunia ulikuwa asilimia 3.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4 mwaka 2014. Hata hivyo, mwenendo huu wa ukuaji wa uchumi unatofautiana kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea. Ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea uliimarika kufikia asilimia 1.9 mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 1.8 mwaka 2014. Ongezeko hilo lilitokana na uwepo wa bei za chini za nishati, kuimarika kwa soko la nyumba na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha. Kwa upande wa nchi zinazoendelea, kasi ya ukuaji wa uchumi ilikuwa asilimia 4.0 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.6 mwaka 2014. Hali hiyo ilitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi kwa nchi za China, Urusi, Brazil na Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara kufuatia kuporomoka kwa bei za bidhaa na mazao katika soko la Dunia pamoja na masharti magumu ya upatikanaji wa mikopo.

9. Mheshimiwa Spika, mwenendo wa mfumuko wa bei kwa mtumiaji wa mwisho Duniani kwa mwaka 2015 uliendelea kupungua kutokana na kushuka kwa bei ya mafuta, kupungua kwa bei za bidhaa na mahitaji ya bidhaa. Mfumuko wa bei kwa mtumiaji wa mwisho Duniani ulipungua na kuwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2014. Aidha, kasi ya ongezeko la bei kwa nchi zilizoendelea ilipungua kutoka wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2014 hadi wastani wa asilimia 0.3 mwaka 2015. Hata hivyo, kasi ya mfumuko wa bei ya mtumiaji wa mwisho kwa kundi la nchi zinazoendelea iliendelea kubaki katika wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2015 kama ilivyokuwa mwaka 2014.

Uchumi wa Taifa

Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

10. Mheshimiwa Spika, Pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 7.0 mwaka 2015 sawa na kiwango cha ukuaji cha mwaka 2014. Ukuaji huu wa uchumi ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme kwa ajili ya matumizi ya shughuli mbalimbali ikiwemo uzalishaji viwandani; kuongezeka kwa uzalishaji wa saruji; na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi. Katika kipindi hicho, shughuli za kiuchumi zilizokua kwa viwango vikubwa zilikuwa ni pamoja na: ujenzi asilimia 16.8; habari na mawasiliano (asilimia 12.1); fedha na bima (asilimia 11.8); na uchimbaji madini na mawe (asilimia 9.1). Aidha, kilimo ambacho ndiyo uti wa mgongo wa uchumi na kinaajiri zaidi ya asilimia 70 ya watu wote nchini kiliendelea kukua kwa kasi ndogo ya asilimia 2.3 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4 mwaka 2014.

Mchango katika Pato la Taifa

11. Mheshimiwa Spika, mchango wa shughuli za **kilimo** ambao hujumuisha mazao, ufugaji, misitu na uvuvi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 29.0 mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 28.9 mwaka 2014. Shughuli za **viwanda na ujenzi** zilizochangia asilimia 24.3 katika Pato la Taifa mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 23.2 mwaka 2014. Vile vile, shughuli za utoaji **huduma** (ikijumuisha biashara na matengenezo, usafirishaji na uhifadhi mizigo, malazi, habari na mawasiliano, fedha na bima, upangishaji majumba, elimu na afya) zilizochangia asilimia 40.0 katika pato la Taifa mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 40.9 mwaka 2014.

Pato la Wastani la kila mtu

12. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015, Tanzania ilikadiriwa kuwa na idadi ya watu 47,351,275 na Pato la Taifa lilikuwa shilingi bilioni 90,863.68. Aidha, wastani wa Pato la kila mtu lilikuwa shilingi 1,918,928 mwaka 2015 ikilinganishwa na shilingi 1,730,405 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Hata hivyo, Pato la wastani kwa kila mtu katika dola za Kimarekani lilipungua kutoka dola za Kimarekani 1,047 mwaka 2014 hadi dola za Kimarekani 966.5 mwaka 2015 kutokana na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. Hivyo, ni dhahiri kuwa bado kunahitajika msukumo zaidi wa kuongeza ukuaji wa Pato la Taifa ili kufikia lengo aa Dira ya Maendeleo ya Taifa la kufikia wastani wa Dola za Kimarekani 3,000 kwa kila mtu na kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

Mwenendo wa Bei

13. Mheshimiwa Spika, wastani wa mfumuko wa bei katika mwaka 2015 ulikuwa asilimia 5.6 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2014. Kupungua kwa mfumuko wa bei nchini kulichangiwa kwa kiwango kikubwa na kushuka kwa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia na hapa nchini na utekelezaji madhubuti wa sera za bajeti na fedha.

Jitihada za Kuondoa Umaskini

14. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2015/16, Serikali iliendelea kuratibu na kufuatilia hali ya umaskini nchini ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano na MKUKUTA-II. Matokeo ya tathmini hiyo yameainishwa katika Taarifa za Utekelezaji wa Mpango huo na MKUKUTA-II kwa kipindi cha Miaka Mitano (2010-2015). Taarifa hizo zilisambazwa kwa waheshimiwa wabunge wakati nikiwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) kwenye semina ya Waheshimiwa Wabunge mwezi Februari, 2016. Tathmini hiyo imesaidia katika kubainisha vipaumbele vya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao pia umejumuisha masuala ya kupambana na umaskini.

15. Mheshimiwa Spika, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukua kwa **pato la wastani** la mtanzania kutoka Shilingi 770,464.3 mwaka 2010 kufikia shilingi 1,918,928 mwaka 2015; kuongezeka kwa kasi ya kupungua kwa umaskini wa mahitaji ya msingi ambapo kati ya mwaka 2007 na 2012 umaskini ulipungua kwa asilimia 6.2, kutoka 34.4 hadi 28.2, ikilinganishwa na kupungua kwa kiwango cha asilimia 4.6 katika kipindi cha miaka 15, yaani kutoka asilimia 39 mwaka 1992 hadi kufikia 34.4 mwaka 2007.

16. Mheshimiwa Spika, tathmini ya **hali ya umaskini** kimaeneo iliyofanyika kwa kutumia takwimu za Sensa ya Watu ya mwaka 2012 na Utafiti wa Hali ya Kipato na Matumizi katika Kaya ya mwaka 2012 inaonesha matokeo chanya na kutofautiana kimkoa na kiwilaya. Mikoa 5 yenye ahueni ya umaskini wa kipato ni Dar es Salaam (asilimia 5.2), Kilimanjaro (asilimia 14.3), Arusha (asilimia 14.7), Pwani (asilimia 14.7) na Manyara (asilimia 18.3). Mikoa 5 yenye umaskini mkubwa wa kipato ni Kigoma (asilimia 48.9), Geita (asilimia 43.7), Kagera (asilimia 39.3), Singida (asilimia 38.2), na Mwanza (asilimia 35.3). Kiwilaya, umaskini mkubwa upo katika wilaya ya Kakonko (Kigoma) na Biharamulo (Kagera) ambapo takriban asilimia 60 ya idadi ya watu katika wilaya hizo wapo chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi. Hii ina maana kuwa maeneo ya

vijijini hususan pembezoni bado watanzania wengi wanaishi katika lindi la umaskini na uwezo wao wa kupata mahitaji ya msingi ni mdogo.

Nguvu Kazi na Ajira

17. Mheshimiwa Spika, Utafiti wa Watu Wenye **Uwezo wa Kufanya Kazi** wa mwaka 2014 ulionesha kuwa nguvu kazi ya Taifa ilikuwa watu 25,750,116, sawa na asilimia 57 ya watu wote Tanzania Bara. Kati ya hao, wanawake walikuwa 13,390,678 (sawa na asilimia 52) na wanaume walikuwa 12,359,438 (sawa na asilimia 48). Vile vile, utafiti huo ulionesha kuwa, kati ya nguvukazi iliyokuwepo, watu wenye uwezo wa kufanya kazi walikuwa watu 22,321,924 na watu wasio na uwezo wa kufanya kazi walikuwa watu 3,428,192. Aidha, sababu za watu wasio na uwezo wa kufanya kazi zilikuwa ni pamoja na ulemavu na ugonjwa wa muda mrefu.

18. Mheshimiwa Spika, kati ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi, walioajiriwa walikuwa watu 20,030,139 na wasioajiriwa walikuwa watu 2,291,785. Kati ya walioajiriwa, wanawake walikuwa 9,886,739 (sawa na asilimia 49.4) na wanaume walikuwa 10,143,400 (sawa na asilimia 50.6). Watu wenye ajira katika jiji la Dar es Salaam walikuwa 1,927,367 sawa na asilimia 9.6 na katika maeneo mengine ya mijini walikuwa watu 5,131,422, (sawa na asilimia 25.6) na maeneo ya vijijini walikuwa watu 12,971,350, (sawa na asilimia 64.8). Kutokana na utafiti huo, ilibainika kuwa idadi kubwa ya kundi la watu walioajiriwa lilikuwa na umri kati ya miaka 35 hadi 64 (asilimia 42.5).

19. Mheshimiwa Spika, utafiti huo umeonesha vile vile kuwa, asilimia 77.8 ya **nguvukazi** yote ya Taifa imeajiriwa au imejiajiri. Uwiano huu wa ajira na nguvu kazi unapima uwezo wa nchi kutoa ajira. Uwiano ulikuwa mkubwa maeneo ya vijijini (asilimia 82.2), wakati jiji la Dar es Salaam lilikuwa na uwiano mdogo zaidi (asilimia 59.8). Aidha, wanaume walikuwa na uwiano mkubwa (asilimia 82.1) ukilinganisha na wanawake (asilimia 73.8). Vile vile, uwiano ulikuwa mkubwa kwa kundi la watu wenye umri wa miaka 35 - 64 (asilimia 87.2) na mdogo zaidi kwenye kundi la miaka 65 na zaidi (asilimia 56.4).

Afya

20. Mheshimiwa Spika, utafiti wa **Hali ya Afya ya Mama na Mtoto** uliofanyika 2015 unaonesha vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja, vimepungua kufikia 43 mwaka 2015 kutoka 51 mwaka 2010 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai. Vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka 5 vimepungua kufikia 67 mwaka 2015 kutoka 81 mwaka 2010 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai. Upungufu wa damu kwa watoto chini ya miaka 5 umepungua toka asilimia 59 mwaka 2010 hadi 47 mwaka 2015. Aidha, kiwango cha upungufu wa chakula kwa watoto chini ya miaka 5

kimepungua kutoka asilimia 8 mwaka 2010 na kufikia asilimia 34 mwaka 2015. Pia umri wa mtanzania wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 51 mwaka 2001 hadi miaka 61 mwaka 2012.

21. Mheshimiwa Spika, utafiti huo pia unaonesha kuwa wastani wa **idadi ya watoto kwa kila mama** imepungua kutoka watoto 5.4 mwaka 2010 hadi 5.2 mwaka 2015. Idadi ya wasichana wanaopata watoto katika umri wa miaka 15 – 19 imeongezeka kufikia asilimia 27 mwaka 2015 kutoka asilimia 23 mwaka 2010. Kuongezeka kwa wasichana wanaoanza kupata watoto katika umri mdogo, yaani miaka 15 – 19 si dalili nzuri kwani inaashiria kuongezeka kwa utegemezi na kudumaza jitihada za kuondoa umaskini katika jamii. Hivyo ni muhimu Serikali, wazazi na wadau wote kushirikiana katika kuhakikisha watoto wengi wa kike wanapata elimu kuanzia shule za awali hadi sekondari na katika vyuo vya ufundi na elimu ya juu ili jitihada za kupambana na umasikini hasa katika maeneo ya vijijini zifanikiwe.

22. Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo kwa pamoja yamechangia kupandisha Kipimo cha Maendeleo ya Binadamu (Human Development Index - HDI) kutoka 0.48 mwaka 2014 hadi 0.52 mwaka 2015. Vile vile, yanaonesha kuwa, kukua kwa uchumi kumechangia kasi ya kupungua kwa umaskini wa kipato na usio wa kipato, ijapokuwa siyo kwa kasi iliyotarajiwa.

Ukuzaji Rasilimali

23. Mheshimiwa Spika, ukuzaji rasilimali uliongezeka kwa asilimia 5.4 kufikia shilingi milioni 25,328,568 mwaka 2015 kutoka shilingi milioni 24,019,720 mwaka 2014. Hata hivyo, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2007 ulipungua kwa asilimia 1.0 na kufikia shilingi milioni 13,996,865 mwaka 2015 kutoka shilingi milioni 14,140,777 mwaka 2014. Uwiano wa ukuzaji rasilimali na Pato la Taifa ulikuwa asilimia 27.9 mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 30.2 mwaka 2014.

Sekta ya Nje

24. Mheshimiwa Spika, mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma nje uliendelea kuimarika mwaka 2015 kama ilivyokuwa mwaka 2014 hususan kufuatia kupungua kwa thamani ya uagizaji wa mafuta ya petroli sambamba na kuongezeka kwa mapato ya mauzo ya bidhaa na huduma nje. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilikuwa dola za Kimarekani milioni 9,450.0 ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 8,717.4 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 8.4. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo asilia hususan bidhaa za viwandani. Kwa upande mwingine, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka

nje ilipungua kwa asilimia 7.8 kutoka dola za Kimarekani milioni 13,586.5 mwaka 2014 hadi dola za Kimarekani milioni 12,528.2 mwaka 2015. Mwenendo huu ulichangia kuimarika kwa urari wa malipo ya kawaida.

25. Mheshimiwa Spika, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Kimarekani milioni 1,063.3 mwaka 2015 ikilinganishwa na ziada ya dola za Kimarekani milioni 727.3 mwaka 2014, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 46.2. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma za mawasiliano, usafirishaji na usafiri hususan biashara ya utalii na kupungua kwa malipo ya huduma za usafirishaji na huduma nyingine za kibiashara.

26. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015, nchi zinazofanya biashara na Tanzania kwa kiwango kikubwa zilikuwa kama ilivyokuwa katika mwaka 2014. Nchi ambazo Tanzania iliagiza bidhaa zake kwa kiwango kikubwa zilikuwa Saudi Arabia, China, India na Umoja wa Falme za Kiarabu ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 55.5 ya bidhaa zote zilizoagizwa kutoka nje. Sehemu kubwa ya bidhaa zilizoagizwa na Tanzania kutoka Saudi Arabia ni bidhaa za mafuta ya petroli wakati mitambo na bidhaa za kielektroniki hususan simu za mkononi ziliagizwa kutoka China. Aidha, Tanzania iliagiza magari, makaa ya mawe, juisi na matunda kutoka India na Afrika Kusini.

27. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, nchi ambazo Tanzania iliuza bidhaa zake kwa kiwango kikubwa zilikuwa ni India, Kenya, Afrika Kusini na China ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 53.7 ya bidhaa zote zilizouzwa nje. Bidhaa zilizouzwa China na India ni pamoja na mbegu za mafuta, vito vya thamani, bidhaa za plastiki, dhahabu, mazao ya samaki na korosho. Kwa upande mwingine, bidhaa zilizouzwa Kenya ni chai, mahindi, maharage, vyandarua, mboga mboga na nafaka. Aidha, dhahabu, madini ya shaba, kahawa na chai ni baadhi ya bidhaa zilizouzwa Afrika Kusini.

Sekta ya Fedha

Thamani ya Fedha ya Tanzania

28. Mheshimiwa Spika, thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani ilishuka kwa wastani wa asilimia 16.8 mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 3.3 mwaka 2014. Dola moja ya Kimarekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi za Tanzania 1,985.4 mwaka 2015 ikilinganishwa na shilingi 1,652.5 mwaka 2014. Kuporomoka kwa thamani ya shilingi hususan katika robo ya nne (Oktoba – Desemba 2015) ya mwaka 2015 kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuimarika kwa dola ya Kimarekani, kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha za kigeni kwa ajili ya bajeti ya

Serikali pamoja na mapato kidogo ya fedha za kigeni yasiyokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma.

Amana katika Benki za Biashara

29. Mheshimiwa Spika, amana katika benki za biashara ziliongezeka kwa asilimia 18.4 mwaka 2015 na kufikia shilingi bilioni 19,149.4 kutoka shilingi bilioni 16,177.8 mwaka 2014. Kati ya hizo, Sekta Binafsi ilichangia shilingi bilioni 18,292.5 ambazo ni sawa na asilimia 95.5 ya amana zote. Amana za fedha za kigeni na amana za akiba na za muda maalum zilichangia sehemu kubwa ya amana zote kwenye benki za biashara mwaka 2015. Uwiano wa amana za fedha za kigeni katika amana zote uliongezeka na kufikia asilimia 32.9 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 28.8 mwaka 2014. Aidha, uwiano wa amana za akiba na za muda maalum ulikuwa wastani wa asilimia 32.4 mwaka 2015.

Mikopo ya Benki za Biashara kwa Shughuli za Kiuchumi

30. Mheshimiwa Spika, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 24.8 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 19.4 mwaka 2014. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kupungua kwa ukuaji wa madai rasmi kwa Serikali. Madai rasmi kwa Serikali Kuu yalikua kwa asilimia 33.8 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 42.9 mwaka 2014. Aidha, thamani ya mikopo iliyotolewa kwa sekta binafsi ilikuwa sawa na asilimia 17.3 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 15.6 katika mwaka 2014. Ukuaji wa mikopo kwenye shughuli za uchukuzi na mawasiliano; mikopo kwa watu binafsi; na kwenye shughuli za viwandani uliongezeka mwaka 2015 ikilinganishwa na mwaka 2014. Katika kipindi hicho, sehemu kubwa ya mikopo ilielekezwa katika shughuli za biashara ambazo zilipata wastani wa asilimia 20.2 ya mikopo yote ikifuatiwa na shughuli za watu binafsi (asilimia 18.0).

Mwenendo wa Viwango vya Riba

31. Mheshimiwa Spika, viwango vya riba za amana na za mikopo viliongezeka mwaka 2015 ikilinganishwa na viwango vya mwaka 2014. Riba ya mikopo kwa ujumla iliongezeka kutoka wastani wa asilimia15.75 Desemba 2014 hadi wastani wa asilimia 16.41 Desemba 2015. Riba za amana za muda maalum ziliongezeka kutoka wastani wa asilimia 8.76 Desemba 2014 hadi wastani wa asilimia 9.22 Desemba 2015.

32. Mheshimiwa Spika, kiwango cha riba za amana za mwaka mmoja kiliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 11.08 Desemba 2015 kutoka wastani wa asilimia 10.66 Desemba 2014. Hata hivyo, riba ya mikopo ya

mwaka mmoja ilipungua kutoka wastani wa asilimia 14.80 Desemba 2014 hadi wastani wa asilimia 14.22 Desemba 2015. Kutokana na mwenendo huu, tofauti kati ya riba za amana na za mikopo za mwaka mmoja ilipungua kutoka wastani wa asilimia 4.14 Desemba 2014 hadi wastani wa asilimia 3.14 Desemba 2015. Kwa upande mwingine, riba katika soko la fedha baina ya mabenki zilipungua na kuwa wastani wa asilimia 7.29 Desemba 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 11.82 Desemba 2014.

33. Mheshimiwa Spika, riba kwenye dhamana za Serikali zilikuwa wastani wa asilimia 18.25 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 15.73 mwaka 2014. Aidha, mauzo ya dhamana za Serikali yalipungua kwa asilimia 8.5 kutoka mauzo yenye thamani ya shilingi bilioni 3,535.7 mwaka 2014 hadi shilingi bilioni 3,235.3 mwaka 2015. Mauzo ya hatifungani kwa mwaka 2015 yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 924.6 kutoka shilingi bilioni 916.7 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 0.9.

Mapato na Matumizi ya Serikali

34. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 22,495.5 kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Katika mwaka 2015/16 Serikali iliilenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi bilioni 13,475.6 sawa na asilimia 14.3 ya Pato la Taifa. Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Aprili 2016, makusanyo ya ndani (ikijumuisha ya Halmashauri) yalikuwa shilingi bilioni 11,481.4 sawa na asilimia 99 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 11,550.8 katika kipindi hicho. Mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 10,170.1 sawa na asilimia 100 ya lengo na mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 967.2 sawa na asilimia 105 ya lengo. Vile vile, mapato ya Halmashauri yalikuwa shilingi bilioni 344.1 sawa na asilimia 79 ya lengo kwa kipindi hicho.

35. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Serikali ilikadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 22,495.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 16,576.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 5,909.1 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Aprili 2016, Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 16,856.9 sawa na asilimia 90 ya lengo katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 13,647.1 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3,209.8 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Uendelezaji wa Sekta Binafsi Uwekezaji Vitega Uchumi Nchini

36. Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa moja kwa moja nchini kutoka nje umeendelea kuongezeka ambapo katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, thamani ya uwekezaji wa moja kwa moja nchini iliongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni 1,229 mwaka 2011 hadi dola za Kimarekani milioni 2,142 mwaka 2014. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa mazingira ya kufanya biashara nchini pamoja na sera na sheria imara za kuvutia uwekezaji nchini.

Urahisi wa Kufanya Biashara Nchini

37. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Urahisi wa Kufanya Biashara ya Benki ya Dunia ya mwaka 2015, Tanzania ilipanda kwa nafasi moja katika vigezo vya urahisi wa kufanya biashara kwa kushika nafasi ya 139 kati ya nchi 189 Duniani ikilinganishwa na nafasi ya 140 mwaka 2014. Hali hii hairidhishi. Hivyo, pamoja na jitihada zilizoanza za kuboresha taratibu za upatikanaji wa vibali vya ujenzi na huduma za biashara kupitia vituo vya pamoja vya utoaji huduma mipakani, ni muhimu kuongeza nguvu zaidi katika kushughulikia kero za uwekezaji na wafanyabiashara hapa nchini, hususan kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika, kuharakisha utoaji wa maamuzi, kuboresha mfumo wa kodi na sera ili viwe vya kutabirika na pia kupambana na rushwa.

38. Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina ya Hali ya Uchumi wa Taifa yapo katika **kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2015**.

UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2015/16

Utekelezaji wa bajeti ya Maendeleo 2015/16

39. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Serikali ilitenga shilingi bilioni 5,909.1 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 4,246.9 na fedha za nje ni shilingi bilioni 1,662.2. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri ni shilingi bilioni 739.4 ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 595.0 na fedha za nje ni shilingi bilioni 144.4. Kwa upande wa Wizara, Taasisi, Wakala na Idara zinazojitegemea zilitengewa shilingi bilioni 5,169.7 ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 3,651.9 na fedha za nje ni shilingi bilioni 1,517.8.

40. Mheshimiwa Spika, fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa hadi Aprili 2016 ni shilingi bilioni 3,209.8. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 2,819.9 na fedha za nje ni shilingi bilioni 398.841. Fedha hizo

za maendeleo zilizotolewa ni sawa na asilimia 65 ya lengo la shilingi bilioni 4,922.5 hadi Aprili 2016. Fedha za ndani zilizotolewa ni sawa na asilimia 79 ya lengo la shilingi bilioni 3,537.4 na fedha za nje zilizotolewa ni sawa na asilimia 29 ya lengo la shilingi bilioni 1,385.2.

Miradi iliyokamilika mwaka 2015/16

41. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa taarifa za mafanikio ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na changamoto zake zilishaelezwa kwa kina katika hotuba za kisekta zilizotangulia, naomba sasa nitaje baadhi ya miradi ya maendeleo iliyokamilika kama kielelezo cha mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2015/16:-

(i) Ujenzi wa madaraja ya Kigamboni, Maligisu, Nangoo, Mbutu na Ruhekei katika barabara kuu;

(ii) Ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam (km 542);

(iii) Ujenzi wa mitambo ya kuchakata gesi katika maeneo ya Madimba na Songosongo;

(iv) Ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi vya Somanga – Fungu na Kinyerezi;

(v) Usimikaji wa mitambo minne ya kufua umeme Kinyerezi I yenye uwezo wa kuzalisha MW 150 na kuanza uzalishaji wa umeme;

(vi) Awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini (REA Turnkey Phase II) na hivyo kuunganisha wateja 61,023 wa awali kati ya wateja 250,000;

(vii) Kukamilika kwa awamu ya Pili ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (km 25,954) na kusambazwa katika mikoa 24 Tanzania Bara;

(viii) Kukamilika kwa mradi wa Maji wa Ruvu Chini (Pwani); na

(ix) Kukamilika kwa miradi mipya 1,160 ya maji ya vijiji 10 katika vijiji 1,206 yenye vituo 28,499 vya kuchotea maji katika Halmashauri 148.

42. Mheshimiwa Spika, miradi mingine katika maeneo ya kipaumbele (miundombinu, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu; utalii, huduma za kifedha na Biashara) ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

43. Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo yapo katika Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 (**Sura ya Pili**).

Changamoto na Hatua zilizochukuliwa

44. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, kumejitokeza changamoto mbalimbali katika kutekeleza Mpango ikiwa ni pamoja na: upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi; ulipaji fidia kwa wakati; taratibu na gharama za ununuzi wa umma; madeni ya wakandarasi, hususan ya ujenzi wa barabara; upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji; utegemezi wa bajeti ya maendeleo; ushiriki mdogo wa sekta binafsi; mazingira yasiyo wezeshi kwa uwekezaji na uendeshaji biashara; na uhaba wa miundombinu (barabara, maji na umeme) ya kuwezesha utekelezaji wa miradi.

45. Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto hizo ikiwemo:- kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha, hususan fedha za miradi ya Matokeo Makubwa Sasa na miradi ya Kitaifa ya Kimkakati; kuendelea kuimarisha miundombinu wezeshi katika maeneo ya miradi ya maendeleo; na kupunguza madeni.

Hali ya Viwanda Nchini

46. Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta ya uzalishaji viwandani katika Pato la Taifa kwa kipindi cha mwongo mmoja uliopita ni wastani wa asilimia 7 ambapo uliongezeka kutoka asilimia 6.6 mwaka 2005 hadi asilimia 7.3 mwaka 2015. Kwa mujibu wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013, Tanzania ina jumla ya viwanda 50,656 ambavyo vipo katika mikoa mbalimbali nchini. Viwanda hivyo vinajumuisha viwanda vya kati na vikubwa 1,769 sawa na asilimia 3.5 ambavyo vinaajiri wafanyakazi 10 na kuendelea, na viwanda vidogo 48,887 sawa na asilimia 96.5 ambavyo vinaajiri wafanyakazi 1 hadi 9. Takriban ajira 231,176 zimetengenezwa kutokana na viwanda hapa nchini, ambapo viwanda vikubwa na vya kati vimetoa ajira 107,732 na viwanda vidogo ajira 123,364.

47. Mheshimiwa Spika, mikoa inayoongoza kwa idadi kubwa ya viwanda ni Dar es Salaam 516 (asilimia 29.2), Arusha 144 (asilimia 8.1), Shinyanga 101 (asilimia 5.7), Kilimanjaro 96 (asilimia 5.4) na Mwanza

88 (asilimia 5.0). Vilevile, aina ya viwanda vingi vilivyopo nchini ni vya uzalishaji wa vyakula 20,228 (asilimia 39.9), mavazi (kanga na vitenge) 13,758 (asilimia 27.2) na samani 7,071 (asilimia 14.0). Hata hivyo, zipo fursa zaidi katika viwanda vingine ambavyo utafiti ulionesha viwanda vyake vipo vichache nchini kama vile nguo 817, TEHAMA 3, mashine na vifaa 30, madawa 9, ngozi 216, kemikali 102 na vifaa vya umeme 269.

Ubinafsishwaji wa Viwanda

48. Mheshimiwa Spika, katika kukidhi mahitaji ya soko huria na ushindani wa kibiashara viwanda 106 vilibinafsishwa kwa lengo la kuongeza ufanisi, uzalishaji, ajira, kupunguza uagizaji wa bidhaa nchini na kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi. Kati ya viwanda vilivyobinafsishwa, uzalishaji katika viwanda 34 umekuwa wa ufanisi na hivyo kuongeza ajira na mapato ya kodi kwa Serikali. Aidha, viwanda 33 vinaendeshwa kwa hasara na viwanda 39 vilivyokuwa vinazalisha bidhaa mbalimbali kama vile ngozi, chuma, korosho, zana za kilimo, sabuni na mafuta ya kupikia vimefungwa kabisa. Changamoto kubwa zinazovikabili viwanda vilivyobinafsishwa ni pamoja na mtaji, teknolojia, malighafi na upatikanaji wa umeme wa uhakika, maji na masoko. Aidha, baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa vilitumika kama dhamana ya kupata mikopo ya benki, na kugharamia shughuli nyingine badala ya uendelezaji viwanda na hivyo kuwa na madeni.

Mikakati ya Kuendeleza Viwanda Nchini

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kwa vitendo dhima ya ujenzi wa uchumi wa viwanda, Mpango huu pamoja na mambo mengine utajikita katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuendeleza viwanda vikubwa, vya kati, vidogo na vile vilivyobinafsishwa.

49. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kulipa fidia kwa maeneo maalum ya uwekezaji na kuweka miundombinu wezeshi itakayovutia Sekta Binafsi kuwekeza katika viwanda vikubwa; kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini ili kuinua nafasi ya Tanzania katika ushindani wa kibiashara; kuendelea kuboresha miundombinu ya msingi kuwezesha maendeleo ya viwanda nchini hususan, miradi ya nishati ya umeme, maji, barabara, reli na bandari; na kuboresha sekta ya fedha ili iweze kutoa mitaji ya kuendeleza viwanda.

50. Mheshimiwa Spika, Mikakati mingine ni pamoja na: kusimamia kikamilifu uingizwaji wa bidhaa zinazozalishwa na viwanda hapa nchini; kuendeleza miundombinu ya SIDO ili kuvutia viwanda vidogo; kuweka mikakati madhubuti ya kuwainua wajasiriamali wadogo na wa kati ili waweze kuzalisha kwa ufanisi; kuboresha mazingira ya biashara nchini ikiwa ni pamoja

na kufuta kodi na tozo ambazo ni vikwazo kwa wajasiriamali wadogo; kuanzisha kongane za viwanda (Industrial Clusters) za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu; na kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi kupitia elimu na mafunzo ya kuendesha na kuendeleza viwanda, ujasiriamali na uwekezaji.

51. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutathmini kwa kina viwanda vyote vilivyobinafsishwa ili kuandaa mikakati ya kuviendeleza; kupitia mikataba yote ya ubinafsishaji na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria; kufufua viwanda vilivyobinafsishwa na kuviendeleza kwa utaratibu wa Ubia kati ya sekta ya umma na Sekta Binafsi; na kuchukua hatua kuhusu uagizwaji wa bidhaa zinazozalishwa na viwanda hapa nchini ili viweze kukua zaidi.

52. Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu Hali ya Viwanda nchini yapo katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 (**Sura ya Tatu**).

MWELEKO WA UCHUMI 2016

53. Katika mwaka 2016/17, shabaha na malengo ya uchumi jumla na bajeti ni kama ifuatavyo:-

(i) Pato Halisi la Taifa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2016 kutoka 7.0 mwaka 2015;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 5.0 na asilimia 8.0 mwaka 2016;

(iii) Mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya halmashauri kufikia asilimia 14.8 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16, na kuendelea kuongezeka kufikia asilimia 16.9 ya Pato la Taifa mwaka 2016/17;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.8 ya Pato la Taifa mwaka 2016/17 kutoka asilimia 12.6 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16;

(v) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 23.2 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16 hadi asilimia 27.0 mwaka 2016/17;

(vi) Nakisi ya bajeti inakadiriwa kuwa asilimia 4.5 ya Pato la Taifa mwaka 2016/17 kutoka makadirio ya bajeti ya asilimia 4.2 mwaka 2015/16;

(vii) Nakisi katika urari wa malipo ya kawaida kuwa asilimia 7.9 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16 na kupungua hadi asilimia 7.5 mwaka 2016/17; na

(viii) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne ifikapo Juni 2017.

MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2016/17

Maeneo ya Kipaumbele 2016/17

54. Mheshimiwa Spika, Miradi ya maendeleo ya kipaumbele katika mwaka 2016/17 imegawanyika katika makundi manne (4) yafuatayo: Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda; Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Rasilimali Watu; Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji; na Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango.

55. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda** miradi itakayotekelezwa ni pamoja na: mradi wa Magadi Soda – Bonde la Engaruka, Arusha; mradi wa kufufua Kiwanda cha General Tyre, Arusha; uendelezaji wa viwanda vidogo – SIDO katika maeneo ya viwanda (Industrial Park) ya Mwanza, Dar es Salaam, Mbeya na Morogoro.

56. Mheshimiwa Spika, miradi itakayotekelezwa katika eneo la **Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Rasilimali Watu** ni pamoja na**:** Kuimarisha mifumo, majengo na miundombinu mingine katika shule za awali, msingi na sekondari; upanuzi na ujenzi wa vyuo vikuu; ukarabati, upanuzi na ujenzi wa vyuo vya ualimu; na ukarabati, upanuzi na ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi; mradi wa kuboresha hospitali za rufaa; Taasisi ya Saratani Ocean Road; na hospitali ya magonjwa ya kuambukiza Kibong'oto; na kuanzisha Progamu ya kuzalisha Ajira na Programu ya Maendeleo ya Ujuzi; Mazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

57. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji,** Serikali itaendelea kutekeleza miradi iliyoanza kutekelezwa katika kipindi cha Mpango wa kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), ikiwa ni pamoja na miradi katika maeneo yafuatayo: nishati (ikiwemo mradi wa Liquified Natural Gas); kilimo cha mazao; mifugo; uvuvi; misitu; maji; miundombinu ya reli na barabara hususan: Kidahwe – Nyakanazi, Masasi – Newala - Mtwara, Mbinga - Mbamba Bay na Tabora – Ipole – Koga - Mpanda; bandari hususan ya

Dar es Salaam, Bagamoyo na Mtwara; usafiri wa anga; usafiri wa majini na TEHAMA.

58. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Serikali itaimarisha **Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango** kwa lengo la kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa mipango na programu mbalimbali za maendeleo. Dhamira ya Serikali ni kuongeza kasi katika kutanzua vikwazo vya utekelezaji na kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango kwa kurekebisha taratibu zitakazosaidia na kuongeza ufanisi wa utekelezaji.

59. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 umeainisha **Miradi Mikubwa ya Kielelezo** ambayo itapewa msisitizo katika utekelezaji wake**.** Miradi hii ni mahsusi kwa maana ya ukubwa wa uwekezaji na matokeo tarajiwa. Miradi hiyo ni pamoja na: mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma; mradi wa chuma Liganga; ujenzi wa reli mpya ya Kati Dar – Kigoma na Tabora – Mwanza na matawi yake Isaka – Kigali/Keza – Musongati na Kaliua - Mpanda kwa kiwango cha standard gauge; uboreshaji wa usafiri katika maziwa makuu ikiwa ni pamoja na ununuzi wa meli moja mpya ya usafirishaji wa abiria na mizigo katika Ziwa Victoria na ukarabati wa meli za MV Victoria, MV Butiama na MV Liemba na kuimarisha Shirika la Ndege la Taifa (ATCL) ikijumuisha ununuzi wa ndege tatu (3) mpya moja (1) ikiwa ni *Bombardier CS300* yenye uwezo wa kubeba abiria 100 – 150 na ndege mbili (2) *Bombardier Q400* zenye uwezo wa kubeba abiria 67 – 88 kila moja.

Mikakati ya Kushirikisha Sekta Binafsi 2016/17

60. Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 utategemea zaidi ushiriki mkubwa wa Sekta Binafsi. Hivyo, Serikali imeweka mikakati ya kujenga na kuboresha miundombinu wezeshi, kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, kuhamasisha ubia kati ya Sekta Binafsi na sekta ya umma. Jitihada mahsusi za Serikali katika eneo hili ni pamoja na: kuongeza kasi ya kulipa fidia katika Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZs na SEZs); Benki ya Rasilimali Tanzania kuongeza utoaji wa mikopo katika sekta mbalimbali kutoka shilingi bilioni 538.7 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 726.9 mwaka 2016; kuiwezesha Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili iweze kupanua huduma zake ziwafikie wananchi na kuwezesha Kituo cha Uwekezaji Tanzania kuwa na ardhi yenye hati miliki kwa ajili ya kuikodisha kwa wawekezaji wa nje.

61. Mheshimiwa Spika, Mpango huu utahusisha utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kwa njia ya ubia ili kuendelea kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi. Miongoni mwa miradi itakayotekelezwa kwa ubia ni

pamoja na ujenzi wa Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini, miradi ya Chuma - Liganga na makaa ya mawe - Mchuchuma; na mradi wa barabara wa Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Express Way.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu Miradi ya Kipaumbele yapo katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 (**Sura ya Nne**).

Ugharamiaji wa Mpango 2016/17

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 Serikali imetenga shilingi bilioni 11,820.503 sawa na asilimia 40 ya bajeti yote ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, fedha za ndani ni shilingi bilioni 8,702.697 sawa na asilimia 74 ya bajeti ya maendeleo na fedha za nje shilingi bilioni 3,117.805 sawa na asilimia 26 ya bajeti ya maendeleo. Sekta binafsi inatarajiwa kuwekeza kiwango kikubwa cha fedha ili kuanzisha na kuendeleza viwanda ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango. Kwa ujumla fedha za maendeleo zimeelekezwa zaidi katika miradi inayolenga kuendeleza viwanda kama vile uchukuzi, ujenzi, nishati, kilimo, maji, elimu na afya.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu Ugharamiaji wa Mpango yapo katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 (**Sura ya Tano**).

Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara na Taasisi za umma zinahusika moja kwa moja katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo katika maeneo yao na kuandaa taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka na mwaka mzima. Taarifa za ufuatiliaji na tathmini za miradi ya maendeleo zitawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaratibu ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo itakayotekelezwa katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zitakuwa na jukumu la kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya Kitaifa ya Kimkakati na ya Sekta Binafsi kwa lengo la kubaini changamoto zinazokabili miradi hiyo na kuzitafutia ufumbuzi.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji taarifa yapo katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 (**Sura ya Sita**).

SHUKRANI

67. Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango Mhe. Dr. Ashatu Kijaji (Mb), Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Wakuu wa Idara za Serikali na Taasisi zinazojitegemea kwa ushirikiano wao wakati wote wa maandalizi ya kutayarisha Taarifa ya Hali ya Uchumi 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/17. Vile vile, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Servacius B. Likwelile kwa kusimamia vizuri kazi za kila siku na maandalizi ya Taarifa ya Hali ya Uchumi 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 na hotuba hii.

68. Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika hali ya uchumi na utekelezaji wa Mpango yamechangiwa na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wakiwemo nchi marafiki, washirika wa maendeleo, sekta binafsi na wananchi wote. Kwa niaba ya Serikali, ninawashukuru wadau hao kwa michango yao.

HITIMISHO

69. Mheshimiwa Spika, hotuba hii na vitabu vya Taarifa ya Hali ya uchumi 2015, na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango www.mof.go.tz na www.mipango. go.tz

70. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa Waheshimiwa Wabunge wapokee, kujadili na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17.

71. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa shughuli zetu za asubuhi lakini ninalo tangazo moja hapa, litatoka ofisi ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba kesho Alhamisi, tarehe 9 Juni, 2016 kutakuwa na kikao cha pamoja kati ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wanaotoka Tanzania. Kikao hicho kitaanza saaa nne asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Wabunge wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 6.02 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu!

(Hapa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni waliondoka Ukumbini)

MBUNGE FULANI: Wahini bwana!

MBUNGE FULANI: Toka haraka wahi, wahi, wahi, wahi!

MBUNGE FULANI: Nenda mkasaini! *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Posho-*oriented,* wahi!

NAIBU SPIKA: Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILLAH – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Pamoja na hotuba hii, nawasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina makadirio ya Bajeti. Kitabu cha Kwanza ni Makadirio ya Mapato; Kitabu cha Pili ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara za Serikali Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali; Kitabu cha Tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Kitabu cha Nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2016 pamoja na Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2016, ambayo ni sehemu ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa baraka na amani anayoendelea kuijalia nchi yetu na pia kwa kuniruhusu kusimama hapa mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017. Aidha, kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu wa Rais na mwanamama wa kwanza kushika nafasi hiyo katika historia ya nchi yetu. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Ruangwa kuwa Mbunge wao na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Spika pamoja na wewe, Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge letu Tukufu. Kadhalika, natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mohamed Othman Chande, Jaji Mkuu wa Tanzania, kwa kuongoza mhimili wa Mahakama kwa weledi mkubwa. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu pia niwashukuru sana Waheshimiwa wenza wa viongozi wetu wa Kitaifa: Mama Janet Magufuli, Bwana Ameir Hafidh Ameir (mume wa Mheshimiwa Makamu wa Rais), Mama Mwanamwema Shein, Mama Mary Majaliwa, Mama Fatuma Ramadhani Mganga (Mke wa Mheshimiwa Spika), Bwana James Andilile (Mume wa Mheshimiwa Naibu Spika) na Mama Saada El-Maamry Othman (Mke wa Mheshimiwa Jaji Mkuu). Ninawashukuru kwa kuwasaidia na kuwatunza viongozi wetu vizuri, ahsante kwenu wote na Mungu awabariki. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine natoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kuwa Mbunge na Waziri wa Fedha na Mipango. Natambua kwamba wananchi wa Tanzania wananidai!

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 29 Februari, 1968, Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwasilisha hati ya madai kama ifuatavyo, nanukuu:-

"Tunadai nini basi kwa wale wenzetu waliojaliwa kupata elimu? Tunadai huduma kwa wananchi na huduma ambayo ukubwa wake utalingana na kiasi cha elimu waliyoipata." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, napenda kumuahidi tena Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kwamba nitaibeba dhamana hii kwa bidii na uadilifu ili kulipa deni langu kwa nchi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwenu na kuwa sehemu ya Bunge hili. Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa dhamana kubwa tuliyopewa na Mheshimiwa Rais ya kuwatumikia Watanzania. Nampongeza pia Dkt. Thomas Kashilillah, Katibu wa Bunge, Bw. Hussein Kattanga, Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kuratibu vyema shughuli za Bunge na Mahakama kwa mtiririko huo. Napenda pia kumpongeza Profesa Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri anayoifanya ya kukagua na kutoa taarifa za matumizi ya fedha za umma kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kwa kuchambua kwa kina bajeti za Mafungu yote na kutoa mapendekezo na ushauri. Aidha, napenda kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati za Kisekta kwa ushauri na mapendekezo waliyoyatoa wakati wakichambua rasimu ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Mbunge na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2016 na Muswada wa Sheria ya Matumizi wa mwaka 2016 ambayo ni sehemu ya Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge wa Jimbo la Kondoa kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango na pia namshukuru kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kumshukuru Dkt. Servacius B. Likwelile, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa uratibu na usimamizi mzuri wa maandalizi ya Bajeti hii. Kadhalika, nawashukuru Naibu

Makatibu Wakuu; Gavana wa Benki Kuu; Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; Msajili wa Hazina; Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu; Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; Wakuu wa Idara, Vitengo na watumishi wote wa Wizara na taasisi zake kwa kazi kubwa waliyoifanya kukamilisha Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii imezingatia mawazo na mapendekezo ya wadau mbalimbali wakiwemo wenye viwanda, wafanyabiashara na wengine wengi. Nawashukuru wote kwa mawazo na ushauri wao. Kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Wataalam na Ushauri wa Masuala ya Kodi *(Task Force)* na Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Kodi *(Think Tank)* kwa ushauri wao mzuri walionipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kukamilisha shukrani hizi, napenda kutoa shukrani maalum, kwanza kwa Profesa Benno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania. Huyu ni mwalimu wangu na mfano bora wa maisha yangu kikazi. Amenilea kitaaluma na kikazi tangu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Benki ya Dunia na ameendelea kunishauri katika utumishi wangu Serikalini. Namshukuru sana kwa uzalendo na unyenyekevu wake na namtakia kheri na afya njema yeye na familia yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia napenda kutoa shukrani maalum kwa rafiki yangu mpenzi, mke wangu Mbonimpaye kwa kunitunza vizuri, lakini hasa kwa kuniombea msaada wa Mungu siku zote akishirikiana na watoto wetu, wanafamilia wengine na marafiki zetu. Ahsanteni na amani iwe kwenu!

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru Viongozi wa Dini mbalimbali na Watanzania wote ambao waliitikia rai ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kumwombea na wanatuombea sana na sisi wasaidizi wake ili tujitoe na kuwatumikia Watanzania na hasa maskini, kwa bidii na unyenyekevu. Mungu awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, nawashukuru sana wananchi wa Kijiji cha Kasumo, Wilaya ya Buhigwe nilikozaliwa, pamoja na wananchi wa Kasulu na wa Mkoa wa Kigoma kwa ujumla. Ahsanteni kwa kunilea na kwa mapenzi yenu mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii inawasilisha Bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yenye kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu. Serikali inaleta bajeti hii kwa dhamira ya kweli ya kutekeleza ahadi zake zilizopo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 – 2020, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 - 2020/2021 na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ili kukidhi kiu na matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo makuu ya kiuchumi ya bajeti hii ni mawili. Kwanza ni kutatua matatizo yanayowakabili wananchi ili kuleta matumaini mapya ya maisha mazuri zaidi kwa wananchi wetu na hasa wa kipato cha chini. Lengo hili litahusisha kufanya mabadiliko makubwa katika utendaji Serikalini, hususan kurejesha nidhamu ya kazi na uwajibikaji na kuondokana na ufanyaji kazi kwa mazoea. Pia kuimarisha uadilifu na usimamizi wa matumizi ya mali za umma na rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, ni kujenga uchumi wa kipato cha kati kiuhalisia kwa kusimamia kwa umakini utulivu wa uchumi na uendelezaji wa viwanda vitakavyoongeza ajira, hasa kwa vijana wetu nchini na kuongeza tija kwenye kilimo ili kuongeza kipato katika sekta hii inayotegemewa na wananchi wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais akifungua Bunge hili tarehe 20 Novemba, 2015, alibainisha maeneo yanayolalamikiwa sana na wananchi na alielekeza Wizara, Ofisi na Taasisi husika zijipange ipasavyo kutatua malalamiko hayo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tena kwamba, mkazo mkuu wa bajeti hii ni kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kutatua kero za wananchi. Aidha, Serikali itatekeleza azma ya kuendeleza viwanda ambavyo ndio msingi wa uchumi endelevu utakaowezesha Taifa letu kufikia hadhi ya kipato cha kati na hali bora ya maisha ya wananchi walio wengi ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli mbiu ya Bajeti ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2016/2017 ni *kuongeza uzalishaji viwandani ili kupanua fursa za ajira* kwa Kiingereza ni *Industrial growth for job creation*. Kwa msingi huo, Bajeti ya maendeleo ya mwaka 2016/2017 imeongezwa kwa kiasi kikubwa na kufikia asilimia 40 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia! Bajeti ya maendeleo ya mwaka 2016/2017 imeongezwa kwa kiasi kikubwa na kufikia asilimia 40 ya bajeti yote. Tofauti na miaka yote ya nyuma ambapo ilikuwa wastani wa asilimia 25, hii haijawahi kutokea. Bajeti hii pia inalenga kujenga mazingira mazuri ya kufanya biashara na kuwekeza ili kuvutia ushiriki wa wawekezaji wa ndani na wa nje katika kuendeleza viwanda na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nieleze kwa ufupi sana mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa fedha 2015/2016. Katika kipindi cha miezi kumi ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2015/2016, Serikali imefanikiwa kutekeleza shughuli muhimu za bajeti licha ya kukabiliwa na changamoto kadhaa. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa

makusanyo ya kodi kufikia wastani wa Shilingi trilioni 1.02 kwa mwezi mwaka 2015/2016 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi bilioni 904 kwa mwezi mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tulifanikisha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 kwa kutumia fedha za ndani bila ya kupata msaada wowote kutoka kwa wadau wa maendeleo kama ilivyozoeleka kwa chaguzi zilizopita, lakini pia tumeanza utekelezaji wa elimu ya msingi bila malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo, zimejitokeza changamoto kadhaa zikiwemo za ukwepaji kodi unaohusisha wafanyabiashara na watumishi wasio waadilifu, uelewa mdogo wa Sheria mpya za Kodi ya Ongezeko la Thamani, mwitikio mdogo wa wafanyabiashara katika matumizi ya mashine za kielektroniki *(EFDs),* pamoja na wananchi kutodai stakabadhi zitokanazo na mashine hizo katika ununuzi wa bidhaa na huduma. Pia mazingira magumu ya ukusanyaji kodi katika sekta isiyo rasmi, uwepo wa wafanyakazi na wanafunzi hewa na kuwepo kwa mahitaji makubwa yasiyowiana na uwezo wa mapato, yakiwemo mahitaji ya kuboresha miundombinu, hususan ya maji, reli, bandari, viwanja vya ndege na barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo juu ya usimamizi wa deni la Taifa. Serikali imeendelea kusimamia deni la Taifa kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ya 134. Hadi Machi, 2016 deni la Taifa lilikuwa Dola za Kimarekani bilioni 20.94 ikilinganishwa na dola za kimarekani bilioni 19.69 Juni 2015, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 6.34. Kati ya kiasi hicho deni la Serikali lilikuwa Dola za Kimarekani bilioni 17.93 na deni la nje la sekta binafsi lilikuwa Dola za Kimarekani bilioni 3.01.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, deni la Serikali liliongezeka kwa asilimia 6.01 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani bilioni 16.92 Juni, 2015. Ongezeko hilo lilitokana na mikopo ya ndani na nje kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Baadhi ya miradi iliyoendelea kutekelezwa kutokana na mikopo hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara na madaraja nchini, mradi wa kimkakati wa kuboresha Majiji, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa mpaka Shinyanga, mabasi yaendayo haraka, ujenzi wa bomba la gesi na mitambo ya kusafisha gesi, upanuzi wa uwanja wa ndege wa Dar es Salaam na mradi wa maji Ruvu Chini na Ruvu Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuendelea kuongezeka kwa deni la Taifa bado ni himilivu na hii inathibitishwa na tathmini ya uhimilivu wa deni la Taifa *(debt sustainability assessment)* iliyofanyika mwezi Septemba, 2015, ambayo ilionesha kuwa deni hilo ni himilivu katika kipindi cha muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017. Shabaha za uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2016/17 ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, pato halisi la Taifa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2016, kutoka asilimia saba mwaka 2015. Pili, kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei katika wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia tano na asilimia nane mwaka 2016. Tatu, mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri kufikia asilimia 14.8 ya pato la Taifa mwaka wa 2015/2016 na kuendelea kuongezeka kufikia asilimia 16.9 ya pato la Taifa mwaka 2016/2017. Nne, mapato ya kodi kufiikia asilimia 13.8 ya pato la Taifa mwaka 2016/2017 kutoka asilimia 12.6 ya pato la Taifa mwaka 2015/2016. Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 23.2 ya pato la Taifa mwaka 2015/2016 hadi asilimia 27 mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakisi ya bajeti inakadiriwa kuwa asilimia 4.5 ya Pato la Taifa mwaka 2016/2017 kutoka makadirio ya bajeti ya asilimia 4.2 mwaka 2015/2016. Nakisi katika urari wa mapato ya kawaida kuwa asilimia 7.9 ya Pato la Taifa mwaka 2015/2016 na kupungua hadi asilimia 7.5 mwaka 2016/2017 na kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa za huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne mwezi Juni, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo haya yatafikiwa kwa kutegemea misingi ya bajeti ifuatayo:-

Kwanza, ni kuendelea kuwepo kwa amani, usalama, utulivu na utengamano nchini kikanda na duniani. Pili, ni utulivu wa bei za mafuta ya *petrol* katika Soko la Dunia. Tatu, kuweko kwa hali nzuri ya hewa nchini na katika nchi jirani. Nne, kuendelea kuimarika kwa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya Jamii kama vile Pato la Taifa, biashara ya nje, ujazi wa fedha mapato matumizi na huduma za jamii. Tano, ni kuimarika kwa sera za fedha na za bajeti zitakazosaidia kupunguza mfumuko wa bei na tofauti kati ya riba za amana na za mikopo. Sita, kuendelea kuimarika na kutengemaa kwa uchumi wa dunia; na saba, ni ushirika wa sekta binafsi katika uchumi utakaoongezeka hususani uwekezaji katika viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera za Mapato mwaka 2016/2017 zimejielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kusimamia kikamilifu matumizi ya vifaa na mifumo ya ki-*electronic* katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato. Mbili, kuendelea kupanua wigo wa walipa kodi ikiwa ni pamoja na kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iweze kuingia katika mfumo wa kodi. Tatu, kuimarisha ufuatiliaji wa mapato yanayokusanywa na Taasisi na Mamlaka

mbalimbali za Serikali. Nne, kuendelea kuchukua hatua za kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija; na tano, kuendelea kuimarisha usimamizi na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara bandarini, kwenye viwanja vya ndege na maeneo ya mipakani ili kuhakikisha kodi stahiki inakusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa misamaha ya kodi, Serikali itaendelea kudhibiti utoaji misamaha ya kodi kwa taasisi za kidini na wawekezaji ili kuhakikisha inakuwa na tija kwa Taifa. Katika kutekeleza hili Serikali itafanya marekebisho ya sheria husika ili kuondoa matumizi mabaya ya misamaha ya kodi. Pamoja na mambo mengine marekebisho hayo yatalenga kuwataka wanufaikaji kulipa kodi kwa bidhaa watakazoingiza na baadaye kuwasilisha maombi ya kurejeshewa kodi hiyo baada ya uhakiki kufanyika. *(Makofi)*

Kwa upande wa mapato yasiyo ya kodi, kuanzia mwaka 2016/2017 usimamizi wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi utakuwa chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. Uamuzi wa kuipatia *TRA* jukumu hili unatokana na uzoefu na mifumo ya ukusanyaji wa mapato iliyopo nchi nzima, lakini pia mafanikio na uzoefu wa nchi nyingine. Serikali itaendelea kusimamia kikamilifu matumizi ya vifaa na mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na utaratibu wa kuziruhusu baadhi ya Taasisi za Serikali kutumia mfumo wa kubakiza maduhuli yaani *retention*. Utaratibu huu umekuwa ukipunguza mapato kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kuzinufaisha taasisi chache, hivyo kuanzia mwaka 2016/2017 Serikali itafuta utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia sasa mapato yote yatakusanywa na kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kila Fungu litapewa fedha kulingana na bajeti yake. Wizara ya Fedha na Mipango kwa upande wake itahakikisha kwamba fedha kutoka Mfuko Mkuu zinagawiwa kwa mafungu mbalimbali bila kuchelewa kulingana na mapato yaliyokusanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera za Matumizi. Katika mwaka 2016/2017, Serikali itaendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu pamoja na miongozo mbalimbali. Lengo Kuu ni kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuziba mianya ya uvujaji wa fedha za umma na kuelekeza kiasi kikubwa cha mapato kwenye Miradi ya Maendeleo. Ili kutimiza hili Serikali itachukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na zifuatazo:-

Kwanza, ni kuhakikisha malipo kwa Wazabuni na watoa huduma yanafanyika kwa kuwasilisha hati za ununuzi *(LPOs)* ambazo zinatokana na *Integrated Financial Management System*. Pia kuwasilisha Bungeni kwa hati ya

dharura katika Bunge hili, marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma. Mheshimiwa Naibu Spika nitarudia, kuwasilisha Bungeni hati ya dharura katika Bunge hili kuhusu marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ili kuziba mianya ya upotevu wa fedha katika ununuzi wa umma na kuhakikisha ununuzi unawiana na thamani ya fedha itakayotumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kudhibiti matumizi ya Taasisi za Serikali yasiyo na tija na kufanya tathmini ya gharama za uendeshaji ili kuchukua hatua stahiki kwa maendeleo ya nchi. Vile vile, kuendelea na zoezi la kuunganisha Halmashauri zote nchini kwenye mfumo wa malipo ya kibenki ili kuongeza udhibiti wa matumizi ya fedha za umma na kuhakikisha kwamba malipo yanafika kwa wakati. Kuhakikisha kwamba Mashirika ya Umma yaliyoundwa kwa lengo la kujiendesha kibiashara yanajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali na pia kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya matumizi ya fedha za umma hususani katika miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze kuhusu kuongeza uzalishaji viwandani. Kama nilivyoeleza awali kauli mbiu ya bajeti ya mwaka 2016/2017 ni kuongeza uzalishaji viwandani ili kupanua fursa za ajira. Katika kufikia azma hii Serikali imelenga kutekeleza mikakati mbalimbali itakayochochea uwekezaji katika viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kufanya uthamini wa ardhi na mali na kulipa fidia kwa maeneo maalum ya uwekezaji yaliyotengwa nchini. Kugharamia tafiti za viwanda kupitia taasisi za *TILDO*, *TEMDO*, *KAMATECH* na *COSTECH*, kuendeleza miundombinu ya viwanda vidogo kupitia SIDO kuanzisha Kongane za viwanda *industrial clusters* na kuwezesha upatikanaji wa teknolojia rahisi na nafuu kwa ajili ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 50.9 katika Fungu 44 na Fungu 46 ambazo pamoja na mambo mengine zitagharamia utekelezaji wa maeneo niliyoainisha hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais wakati wa hotuba ya ufunguzi wa Bunge lako Tukufu Serikali itahakikisha viwanda vilivyopo vinafanya kazi na katika mwaka 2016/2017, Serikali itakamilisha tathmini ya viwanda vilivyobinafsishwa ili kuweka mikakati ya namna bora ya kuviendeleza. Baadhi ya viwanda hivyo ni viwanda vya nguo, viwanda vya mazao ya mifugo, viwanda vya kusindika mazao yakiwemo mazao ya mpira, korosho, tumbaku, miwa na mpunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu hilo fedha za maendeleo zimetengwa katika mafungu mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza mashamba na kuimarisha uzalishaji wa mazao ya kilimo na ya mifugo. Pamoja na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi katika viwanda, Serikali itachukua hatua stahiki dhidi ya wawekezaji waliokiuka masharti ya mikataba ya mauzo ya viwanda walivyobinafsishiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mazingira ya uwekezaji wa viwanda Serikali imetenga fedha za kuboresha miundombinu ya uwekezaji hususani umeme maji, barabara, bandari na reli. Aidha, Serikali imedhamiria kuondoa urasimu usio wa lazima na kuharakisha utoaji wa maamuzi ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi katika viwanda. Vilevile zipo hatua mahsusi za kodi zinazopendekezwa katika bajeti hii ambazo zina lengo la kushawishi na kuhimiza uwekezaji wa sekta binafsi katika viwanda. Serikali pia itaimarisha upatikanaji wa mikopo ya uendelezaji wa viwanda kupitia Benki ya Rasilimali pamoja na taasisi nyingine za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Balozi zetu na *Diaspora* itaimarisha Diplomasia ya Uchumi katika nchi mbalimbali hasa zile zilizoendelea pamoja na nchi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi ikiwemo Jamhuri ya Watu wa China, India, Korea Kusini, Afrika Kusini na Brazil ili kushawishi wawekezaji kuja kuwekeza Tanzania na hivyo kufanikisha azma ya Serikali ya kuwa na uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji nchini ambayo yatahamasisha kampuni za kigeni zilizoko hapa nchini kuwa Mabalozi wetu na kuvutia kampuni nyingine za nje huko wanakotoka ili waje kuwekeza hapa nchini. Hivyo kama nilivyoeleza awali jukumu la kuboresha mazingira ya uwekezaji litapewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za kutatua kero za wananchi. Bajeti hii inajikita kutatua kero katika maeneo yaliyolalamikiwa na wananchi kama nilivyoeleza hapo awali. Baadhi ya hatua za kibajeti na kiutawala zitakazochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa upande wa utoaji rushwa katika utoaji wa huduma. Katika kukabiliana na rushwa na ufisadi Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 2.5 ili kuwezesha uanzishwaji wa Mahakama ya Mafisadi. Narudia Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.5 ili kuwezesha uanzishwaji wa Mahakama ya Mafisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 72.3 katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za TAKUKURU ili kuiwezesha Taasisi hii kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Vile vile

katika bajeti ya 2016/2017, Serikali imetenga Shilingi bilioni 44.7 kwa ajili ya kuiwezesha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kukagua na kudhibiti matumizi ya fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za kuzuia upotevu wa mapato. Serikali itadhibiti upotevu wa mapato kwa kuimarisha ufuatiliaji wa mara kwa mara katika maeneo mbalimbali ya biashara, bandarini, viwanja vya ndege na mipakani, kuwajengea uwezo watumishi ili waweze kufanya kaguzi za kitaalam hasa katika sekta za madini, maliasili, ardhi, mafuta na gesi asilia. Kuhimiza matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi pamoja na kupunguza misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawapongeza wafanyabiashara walioitika matakwa ya sheria ya usimamizi wa kodi ambayo inamtaka kila mfanyabiashara isipokuwa wale ambao wametangazwa rasmi na Kamishna wa Mamlaka ya Mapato kutotumia mashine za *EFD* kutoa risiti kila anapouza bidhaa au huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kuna baadhi ya wafanyabiashara ambao wanakaidi matakwa haya ya kutumia mashine hizo. Napenda kuwasihi wafanyabiashara hao kuanza mara moja kutumia mashine hizo vinginevyo watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwanyang'anya leseni zao za biashara na hawataruhusiwa kufanya biashara hapa nchini kwa kipindi kisichopungua miaka miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa upande wa Serikali ili kuwa na usimamizi mzuri wa fedha za Serikali na kuhakikisha kwamba zinatumika kama ilivyokusudiwa; kwa Mamlaka niliyopewa chini ya Sheria ya Fedha za Umma pamoja na kanuni zake malipo yote lazima yaambatanishwe na ankara za madai au stakabadhi *(tax invoice)* zilizotolewa na mashine za *EFD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo kuanzia tarehe 1 Julai, 2016 ni marufuku kwa Wizara, Taasisi, Wakala za Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya biashara na Wazabuni na Wafanyabiashara wengine ambao hawatumii mashine za kielektroniki *(EFD)*. Aidha, malipo yatakayofanywa bila stakabadhi au ankara zisizokuwa za mashine za *EFD* ni lazima ziambatanishwe na ushahidi kuwa mfanyabiashara husika ametangazwa rasmi na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kutotumia mashine za *EFD*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za kudhibiti matumizi; Serikali itaendelea kuchukua hatua za kupunguza na kudhibiti matumizi bila kuathiri ubora wa huduma zinazotolewa na hivyo kuhakikisha uwepo wa ufanisi katika matumizi ya Serikali. Baadhi ya hatua hizo zimeainishwa katika mwongozo wa kutayarisha

mpango na bajeti wa mwaka 2016/2017 niliouwasilisha hapa Bungeni Februari, 2016, na miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhakikisha mikutano yote ikiwa ni pamoja na mikutano ya Bodi, mafunzo na semina inatumia kumbi za Serikali na za Taasisi za Umma. Kutoa kipaumbele kwa Taasisi za Umma katika kutoa huduma kwa Serikali kama vile bima, usafirishaji wa barua, mizigo na vifurushi, matangazo na usafiri ili mradi ziwe ni shindani, hatutaki kulea uzembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, narudia, kutoa kipaumbele kwa Taasisi za Umma katika kutoa huduma za Serikali kama vile bima, usafirishaji wa barua, mizigo na vifurushi, matangazo na usafiri, lakini pia kudhibiti matumizi ya umeme, simu na maji, ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara, kudhibiti ulipaji wa mishahara kwa Watumishi ili kuepuka malipo yasiyostahili. Aidha, Serikali itaendelea kufanya sensa ya watumishi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kudhibiti utoaji wa mikopo ya elimu ya juu ili kuepuka utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wasiostahili. Kuendelea kufanya ununuzi wa magari kwa pamoja na bidhaa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji ili kupata unafuu wa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kudhibiti gharama za uendeshaji wa magari ikiwa ni pamoja na matengenezo, mafuta na vilainishi. Kupunguza na kuondoa matumizi yasiyo na tija katika maeneo mbalimbali ikiwemo maadhimisho na sherehe za Kitaifa, matamasha, machapisho na safari za ndani na nje zisizo na tija. Tisa, ni kuhimiza matumizi ya nakala laini *(soft copy)* za machapisho mbalimbali hususani yanayozidi kurasa hamsini ili kupunguza gharama za uchapishaji na kutunza mazingira. Mwisho, ni kudhibiti matumizi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yasiyowiana na majukumu yao ya msingi na yasiyo na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kero nyingine ambayo wananchi wetu walilalamika sana ni katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. Azma kuu ya Serikali ni kuimarisha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, kwa mtazamo wa kibiashara, kukuza viwanda na kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na sekta hii. Hata hivyo bado sekta hii inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo kodi na tozo za mazao zisizo na tija, uhaba wa pembejeo, vifaa duni, masoko, na uhaba wa maafisa ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imetenga jumla ya Shilingi trilioni 1.56, sawa na asilimia 4.9 ya bajeti yote ukiondoa deni la Taifa, kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji, zikiwemo ununuzi wa pembejeo, kuboresha upatikanaji

wa masoko, kuongeza upatikanaji wa zana bora za kisasa za kilimo, ufugaji na uvuvi na kuongeza maafisa ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kupunguza ama kuondoa kabisa ushuru na kodi mbalimbali za mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi zisizo na tija. Nitaeleza hatua mahususi muda mfupi ujao. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania itaendelea kutoa mikopo ya riba nafuu na masharti yanayozingatia hali halisi ya kilimo ili kusaidia kuleta mapinduzi ya kilimo kutoka kilimo cha kijungujiko *(subsistence farming)* kwenda kilimo cha kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Benki ya Kilimo itaendelea kutangaza na kupanua huduma zake kwa wananchi mikoani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Migogoro ya Ardhi. Serikali itaendelea na juhudi za kutatua migogoro katika sekta ya ardhi ikiwemo migogoro kati ya wakulima na wafugaji, vijiji na hifadhi, wananchi na wawekezaji, uvunjaji wa sheria za ardhi na umiliki wa mashamba pori. Katika kukabiliana na migogoro hiyo, Serikali imtenga Shilingi bilioni tano kwa ajili ya Mfuko wa Fidia ya Ardhi, Shilingi bilioni 13 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa umilikishwaji wa ardhi na Shilingi bilioni 8.8 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya upimaji wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imetenga Shilingi bilioni 33.4 kwa ajili ya programu ya kuwezesha umilikishaji wa ardhi na uwekaji wa kumbukumbu utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu. Vile vile Serikali itaendelea kushajili migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini na kutafuta ufumbuzi kulingana na mazingira ya eneo husika ili kupunguza migogoro baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma zisizoridhisha za usafiri na usafirishaji. Serikali itaendelea kukabiliana na kero zinazotokana na uchakavu wa miundombinu ya reli, barabara, bandari na viwanja vya ndege. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga Shilingi trillion 5.47 sawa na asilimia 25.4 ya bajeti yote ukiondoa deni la Taifa kwa ajili ya miradi ya ujenzi na uchukuzi. Baadhi ya maeneo yanayohusika ni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni ujenzi wa miundombinu ya barabara. Kiasi cha Shilingi trilioni 2.18 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hasa zenye kufungua fursa za kiuchumi na kukarabati zile zilizoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uchukuzi Serikali imetenga shilingi trilioni 2.49 kwa ajili ya kuanza kujenga Reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge*; lakini pia kwa ajili ya ununuzi wa ndege tatu mpya za abiria, ununuzi wa meli mpya Ziwa Victoria, ukarabati wa Meli katika Ziwa Victoria na

Ziwa Tanganyika, uboreshaji wa miundombinu ya bandari na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege. Aidha, kiasi cha Shilingi bilioni 161.4 kimetengwa katika Mfuko wa Reli kwa ajili ya ununuzi wa mabehewa na vichwa vya treni pamoja na ukarabati wa reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa umeme Serikali imetenga jumla ya Shilingi trilioni 1.13 sawa na asilimia 5.3 ya bajeti yote, bila kujumuisha deni la Taifa ili kugharamia upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa ajili ya matumizi ya majumbani na viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya miradi itakayotekelezwa ni pamoja na kuongeza kasi ya usambazaji wa Umeme Vijijini, kupitia *REA* na kukamilisha miradi ya umeme inayoendelea ikiwemo kuongeza mitambo mingine yenye uwezo wa kufua *megawatt* 185 katika Mradi wa *Kinyerezi One* na *Kinyerezi Two*. Serikali itahakikisha kuwa Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* linakuwa na uwezo wa kifedha ili lijiendeshe lenyewe na kuwa na ushindani katika uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo nafuu ili kupunguza gharama kwa wazalishaji na walaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji duni wa huduma za afya, maji na elimu. Kuna changamoto nyingi katika maeneo haya, ikiwemo kukosekana na upatikanaji wa uhakiki wa maji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya majumbani na viwandani, lakini huduma bora za afya. Aidha, kuna changamoto za ubora wa elimu na upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa wakati. Bajeti ya 2016/2017 imejielekeza katika kutatua changamoto hizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa upande wa elimu. Sekta ya Elimu imetengewa jumla ya Shilingi trilioni 4.77 sawa na asilimia 22.1 ya bajeti yote bila kujumuisha deni la Taifa. Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za elimu zikiwemo elimu ya msingi bila malipo, gharama za uendeshaji wa shule ikiwemo chakula, ununuzi wa vitabu na mitihani, mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu katika ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa afya. Kwa kutambua umuhimu wa huduma bora za afya kwa wananchi, Serikali imetenga jumla ya Shilingi trilioni 1.99 sawa na asilimia 9.2 ya bajeti yote bila kujumuisha deni la Taifa kwa ajili ya Sekta ya Afya. Baadhi ya maeneo yanayohusika ni pamoja na ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi *(reagents)* ambayo yametengewa Shilingi bilioni 180.5, lakini pia ulipaji wa deni la Bohari Kuu ya Dawa ya *(MSD)*, tumetenga Shilingi bilioni 71 na uboreshaji wa miundombinu ya kutolewa huduma za afya katika ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maji, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi trilioni 1.02, sawa na asilimia 4.8 ya bajeti yote bila kujumuisha deni la Taifa kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama nchini. Baadhi ya shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji, mijini na vijijini, ulipaji wa madeni ya wakandarasi na utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mazingira wezeshi kwa sekta binafsi. Kama nilivyokwishaeleza bajeti ijayo Serikali imedhamira kuboresha mazingira ya kufanya biashara ikiwa ni pamoja na kuwekeza kwenye miundombinu ya reli, barabara, bandari, maji na kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika ili kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika maeneo mbalimbali. Aidha, Serikali itaendelea kupitia kodi, tozo na ada mbalimbali ili kuzipunguza au kuziondoa zile ambazo zinalalamikiwa na wananchi na wawekezaji wa ndani ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa jitihada zitakazochukuliwa na Serikali katika kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi, ni pamoja na kuboresha huduma za upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kuimarisha soko la mitaji, kukuza utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi *(PPP)* na kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kuboresha miundombinu ya umeme usafirishaji, maji, usambazaji wa gesi asili, mfumo wa kodi, kuweka vivutio mbalimbali, kuondoa urasimu usio wa lazima na kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshaji kiuchumi makundi maalum, nikianza na maendeleo vijijini. Serikali ya Awamu ya Tano imeazimia kuwawezesha wananchi kiuchumi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015, ambapo Shilingi milioni 50 ziliahidiwa kwa kila kijiji ili kuwawezesha wananchi kuanzisha na kuendeleza shughuli za uzalishaji kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa *(SACCOS)* na vikundi vingine vya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza ahadi hii Serikali imetenga Shilingi bilioni 59 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu kwa awamu. Mpango huu utaanza kutekelezwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu mara baada ya kukamilisha utaratibu wa matumizi ya fedha hizo ili kuhakikisha kuwa fedha hizi zinatumika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vijana, wazee, wenye ulemavu, wanawake na watoto, Bajeti ya Mwaka 2016/2017. imezingatia mahitaji ya makundi haya hasa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga Shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya makazi ya wazee na mahabusu ya watoto na chakula dawa na mahitaji mengine ya watoto walio katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga asilimia tano ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri kwa ajili ya vijana. Aidha, Shilingi bilioni moja zimetengwa chini ya Fungu 65 kwa ajili ya kuendeleza vijana. Vile vile Shilingi bilioni tano zimetengwa katika Fungu 65 kwa ajili ya kuendeleza ujuzi kwa vijana ambao hawana ajira na wale walioko kwenye soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2016/2017, Serikali imetenga asilimia tano ya mapato ya ndani ya kila halmashauri kwa ajili ya kuwezesha vikundi vya maendeleo vya wanawake katika halmashauri husika. Vile vile Serikali imetenga Shilingi bilioni 1.95 kwa ajili ya uwezeshaji wa wanawake kiuchumi katika Fungu 53. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watu wenye ulemavu Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa vifaa vilivyotengenezwa mahususi kwa ajili yao vinasamehewa kodi ili viweze kupatikana kwa bei nafuu. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha shule maalum za watoto wenye ulemavu na kugharamia mahitaji yao ili kuwajengea mazingira mazuri zaidi ya kujifunzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wasanii, wabunifu na wana michezo. Katika mwaka 2016/2017; Serikali kupitia Fungu 96 imetenga jumla ya Shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya sanaa, ubunifu, utamaduni na michezo, ikiwa ni pamoja na kuratibu na kusimamia uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Ubunifu. Kusimamia urasimishaji wa shughuli za sanaa, kusimamia na kudhibiti filamu zitakazoingia sokoni bila kufuata utaratibu na kuratibu uendeshaji wa kazi za sanaa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wachimbaji wadogo wa madini. Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuwawezesha wachimbaji wadogo wa madini ili kuongeza tija na ufanisi katika shughuli zao na hivyo kuongeza ajira, kukuza kipato cha wachimbaji na wananchi wanaozunguka maeneo ya uchimbaji wa madini. Katika mwaka 2016/2017, Serikali inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

Kuwapatia ruzuku, mafunzo, kuwatengea maeneo maalum ya uchimbaji, kuimarisha soko pamoja na kuziwezesha taasisi zinazohusika na ukaguzi wa usalama wa migodi ili kupunguza ajali zinazoweza kuepukika. Kiasi cha fedha kilichotengwa kwa madhumuni haya katika Bajeti ya Mwaka 2016/2017 ni Shilingi milioni 900 kwa ajili ya ruzuku ya wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wafanyakazi. Ili kuboresha kipato cha wafanyakazi, siku ya Mei Mosi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza kiwango cha kodi ya mapato kwenye mishahara *(Pay As You Earn)* kipunguzwe kutoka

asilimia 11 hadi asilimia tisa (9) ili kupunguza makali ya maisha kwa wafanyakazi, agizo hilo litaanza kutekelezwa Julai, Mosi 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuanzia mwaka ujao wa fedha Serikali itaanza kuwasilisha mchango wa mwajiri wa asilimia 0.5 ya mshahara kwenye Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi ili watumishi wa umma wapatapo ajali mahali pa kazi waweze kulipwa na Mfuko. Kadhalika, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kuwezesha watumishi wake kujenga au kununua nyumba kupitia Bodi ya Mfuko wa Mkopo wa Nyumba kwa Watumishi wa Serikali pamoja na Watumishi *Housing Company*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya Ulinzi na Usalama. Serikali inavipongeza sana vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kujipambanua kwa nidhamu ya hali ya juu katika kazi zao. Hata hivyo, Serikali inawaelekeza Maafisa Masuhuli wa mafungu husika kujipambanua vivyo hivyo kwa nidhamu kama hiyo kwa matumizi ya fedha na mali za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa 2016/2017, utaratibu wa kutoa misamaha ya kodi kwenye maduka ya vyombo vya ulinzi na usalama utasitishwa na nitaeleza utaratibu mpya baadaye kidogo. Pia Serikali itaendelea kujenga nyumba za makazi kwa askari ili kukabiliana na uhaba wa makazi kwa askari nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nieleze maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato. Napenda kuwasilisha sasa mapendekezo ya hatua mpya za kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi. Ikiwa ni pamoja na kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada chini ya sheria mbalimbali za kuboresha taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali. Aidha, marekebisho haya yanalenga pamoja na mambo mengine, kuongeza mapato ya Serikali na kuchochea ukuaji wa uchumi hususani katika sekta ya viwanda, kilimo, usafirishaji na kukuza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *VAT,* Sura ya 148. Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye maharagwe ya soya baada ya kubaini kuwa mazao haya yalisahaulika kuingizwa kwenye orodha chini ya kifungu cha tatu cha jedwali la misamaha linalojumuisha mifugo, mazao ya kilimo, ambayo hayajasindikwa na chakula cha binadamu.

Pili, napendekeza kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye mbogamboga zote na mazao ya mifugo yakiwa hayajasindikwa kama inavyoonekana kwenye ushuru wa pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki,

Sura ya Pili, ya Tatu, ya Saba, ambayo ni matunda na karanga, Sura ya Nane nafaka, lakini pia Sura ya Kumi unga na nafaka na Sura ya Kumi na Moja mbegu za mazao. Hatua hii inakusudia kutoa msamaha wa kodi ya *VAT* kwenye mazao ya chakula ambayo hayajasindikwa ili kuwezesha upatikanaji wa lishe bora ya msingi kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Tatu, kuongeza vitamini na virutubishi kwenye orodha ya vifaa na madawa muhimu, yanayoidhinishwa na Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa ajili ya kupata msamaha wa kodi. Vitamini na virutubisho hivyo huongezwa kwenye vyakula ili kuboresha lishe kama njia mojawapo ya kuimarisha afya ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napendekeza kuongeza madawa ya kutibu maji yanayotumiwa na binadamu kwenye orodha ya vifaa na madawa muhimu yanayoidhinishwa na Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya kupata msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani, kwenye huduma za utalii, hususani kuongoza watalii, kuendesha watalii, utalii majini, kuangalia wanyama na ndege wa porini, kutembelea hifadhi na usafirishaji watalii ardhini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii inachukuliwa kama ilivyokusudiwa wakati wa kutunga Sheria mpya ya *VAT* ambayo ilianza kutumika Julai, 2015, lakini kwa kutambua kwamba mikataba iliyokuwepo wakati huo kati ya watoa huduma wa utalii na watalii waliokuwa wanakuja nchini ilikubalika kusubiri kukamilika kwa makubaliano hayo kwa mwaka unaomalizika. Huduma hizi pia zinatozwa kodi ya *VAT* katika nchi nyingine ikiwa ni pamoja na Kenya, Rwanda na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa zinazotengenezwa Tanzania Bara na kuuzwa Zanzibar zitatozwa kodi ya ongezeko la thamani upande wa Zanzibar na bidhaa zinazotengenezwa Zanzibar na kuuzwa Tanzania Bara zitatozwa kodi hiyo upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni kuondoa utaratibu uliokuwepo hapo awali wa kufanya marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani kwenda Zanzibar, kwa kuwa sheria ya kodi hiyo inayotumika sasa haina kifungu kinachoruhusu marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani kwenda Zanzibar kama ilivyokuwa kwenye sheria iliyofutwa. Kwa kuwa, kila upande wa Muungano una Sheria yake ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, kodi hii itatozwa sehemu ambako bidhaa au huduma itatumika *(destination principle)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo muhimu katika utozaji wa kodi ya ongezeko la thamani, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itakuwa inakusanya kodi hii kwa bidhaa zinazozalishwa Tanzania Bara na kupelekwa Zanzibar, vilevile Tanzania Bara itakuwa inakusanya kodi hii kwa bidhaa zinazozalishwa Zanzibar na kuletwa Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya marekebisho katika orodha ya misamaha ya bidhaa za *petrol* chini ya Kifungu cha 15 cha Jedwali la Misamaha ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014 ili kujumuisha bidhaa za lami zenye *HS Code* 27.13, 27.14, 27.15 ambazo hazikujumuishwa katika Jedwali hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye bima ya vyombo vya usafiri wa anga. Hatua hii inapendekezwa kwa kuzingatia kuwa sekta ya usafirishaji wa anga bado ni changa kuweza kuhimili ulipaji wa bima kwa vyombo hivyo vya usafiri. Hivyo, kuna umuhimu wa kuhamasisha ukuaji wa sekta hii ya usafiri wa anga na hatimaye kukuza utalii. Aidha, hatua hii itasaidia wawekezaji katika sekta ya usafiri wa anga kutumia bima za hapa nchini badala ya nje kwenye mikataba ya ukodishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napendekeza kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwenye ada za huduma za kibenki zinazotozwa na benki hizo ili kupanua wigo wa kodi isipokuwa riba kwenye mikopo. Hatua hizi za kodi ya ongezeko la thamani kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa jumla ya shilingi bilioni 136.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na marekebisho hayo kwenye kodi ya ongezeko la thamani Serikali itachukua hatua mbalimbali za kiutawala ndani ya mamlaka ya mapato ili kuboresha makusanyo ya kodi, hii ikiwa ni pamoja na kuanzisha *program* kabambe ya kufuatilia makusanyo na hivyo kupanua wigo wa kodi. Ili kutekeleza azma hii Serikali itafanya yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha kuwa daftari la usajili wa walipa kodi linahuishwa kila wakati na kuwa na taarifa sahihi za walipa kodi.

(ii) Kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wote wakubwa na wa kati hapa nchini wanapatiwa mashine za kielektroniki na kuzitumia kikamilifu.

(iii) Kuendelea kuimarisha ukaguzi wa hesabu za walipa kodi ili kuwezesha kodi stahiki kulipwa kwa wakati na kuanzisha ofisi mpya ya kusimamia mapato kwa ngazi za Wilaya katika mikoa ya kikodi kwenye Jiji la Dar es Salaam na vituo vipya vya huduma kwa walipa kodi kwa maeneo mbalimbali ya Majiji na Miji mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza pia kufanya mapitio ya Sheria ya Uwekezaji ili iendane na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa lengo la kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija. Hatua hizo za kiutawala zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 268.6. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa *(Excise Duty)* Sura ya 147.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kufanya marekebisho yafuatayo kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa *(Excise Duty)*:-

Kwanza, ni kufanya marekebisho ya viwango maalum vya kodi *(specific duty rates)* za baadhi ya bidhaa zisizo za *petrol* kwa kiwango cha mfumuko wa bei wa asilimia tano. Marekebisho haya ni kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa inayotaka yafanyike marekebisho ya viwango hivyo vya ushuru kulingana na mfumuko wa bei ili kuendana na thamani halisi ya fedha. Hata hivyo, marekebisho haya hayatafanyika kwenye maji ya kunywa yaliyosindikwa kwenye chupa. Mabadiliko ninayopendekeza ni kama ifuatavyo:-

(i) Ushuru wa vinywaji baridi kutoka shilingi 55 kwa lita hadi shilingi 58 kwa lita, ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda yaani *juice* iliyotengenezwa kwa matunda yanayozalishwa hapa nchini, kutoka sh. 10/= kwa lita hadi sh. 11/= kwa lita. Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda yaani juisi iliyotengenezwa kwa matunda ambayo hayazalishwi hapa nchini, kutoka sh. 200/= kwa lita hadi sh. 210/= kwa lita.

(ii) Ushuru wa bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa *unmalted* kama vile kibuku, kutoka sh. 409/= kwa lita hadi sh. 430/= kwa lita, ushuru wa bia nyingine kutoka sh. 694/= kwa lita hadi sh. 729/= kwa lita, ushuru wa bia zisizo na kilevi ikijumuisha vinywaji vya kuongeza nguvu kutoka sh. 508/= kwa lita hadi sh. 534/= kwa lita. Ushuru wa mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa ndani ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 75 kutoka sh. 192/= kwa lita hadi sh. 202/= kwa lita. Ushuru wa mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25 kutoka sh. 2,130/= kwa lita hadi sh. 2,237/= kwa lita, ushuru wa vinywaji vikali kutoka sh. 3,157/= kwa lita hadi sh. 3,315/= kwa lita.

(iii) Ushuru wa bidhaa kwenye maji yanayozalishwa viwandani hautaongezeka, sigara zisizo na kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 kutoka sh. 11,289/= hadi sh. 11,854/= kwa kila sigara 1,000, sigara zenye kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 kutoka sh. 26,689/= hadi sh. 28,024/= kwa sigara 1,000. Sigara nyingine zenye sifa tofauti na hizo nilizoziainisha kutoka sh. 48,285/= hadi sh. 50,700/= kwa kila sigara 1,000; tumbaku ambayo ipo tayari

kutengeneza sigara yaani *cut filler* kutoka sh. 24,388/= hadi sh. 25,608/= kwa kilo. Ushuru wa sigara unabaki kuwa asilimia 30.

(iv) Ushuru wa mafuta ya kulainisha mitambo kutoka sh. 665.50 kwa lita hadi sh. 699/= kwa lita. Ushuru wa *grease* za kulainisha mitambo kutoka senti 75 kwa kilo hadi senti 79 kwa kilo na ushuru wa gesi asili kutoka senti 43 kwa futi za ujazo hadi senti 45 kwa futi za ujazo. Kuongeza ushuru wa bidhaa *excise duty* unaotozwa kwenye samani zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zinazotambulika katika *HS Code* 94.01 na *HS Code* 94.03 kutoka asilimia 15 hadi asilimia 20 kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya samani zinazotengenezwa kwa kutumia mbao zinazozalishwa hapa nchini, kuongeza ajira na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ugumu uliojitokeza katika kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na mifuko ya *plastic,* Serikali imeamua kupiga marufuku utengenezaji, uuzaji, ununuzi na matumizi ya mifuko ya *plastic* yenye kipimo cha unene chini ya *microns* 50 na kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 10 kwenye ada zinazotozwa na watoa huduma wa simu katika kutuma na kupokea fedha badala ya ushuru huo kutozwa tu kwenye kutuma fedha pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utaratibu wa sasa baadhi ya kampuni wanazotoa huduma zimetumia mwanya na kuhamishia sehemu kubwa ya ada hiyo kwenye kupokea fedha na hivyo kuwa nje ya wigo wa kodi. Hatua hizi za ushuru wa bidhaa kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 63.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, napendekeza kufanya mabadiliko ya viwango vya kodi kama ifuatavyo:-

(i) Kuondoa msamaha wa kodi ya mapato kwenye malipo ya kiinua mgongo kitakacholipwa kwa Wabunge kila mwisho wa muhula wa miaka mitano ili kujenga msingi wa usawa na haki katika utozaji wa kodi kwa kila mtu anayestahili kulipa kodi. *(Makofi)*

(ii) Kutoza kodi ya mapato kwenye mapato yote yanayotokana na hisa kwenye makampuni, marekebisho hayo yatafanyika kwa kufuta aya ya (d) katika kifungu cha tatu (3) cha Sheria ya Mapato cha Sura ya 332 cha tafsiri ya maneno *investment assets* yaliyokuwa yanatoa msamaha wa kodi kwa wenye hisa chini ya asilimia 25 kwenye makampuni. Hatua hii itaongeza wigo wa kodi kwa ujumla wake na kupunguza misahama ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika..

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri kwa sababu tutapata nafasi ya mjadala hapo baadaye. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza:-

(iii) Kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato yatokanayo na ajira kutoka asilimia 11 hadi asilimia tisa na hatua hii inachukuliwa ikiwa ni sehemu ya dhamira ya Serikali ya muda mrefu ya kuwapunguzia mzigo wa kodi wafanyakazi hatua kwa hatua hadi kufikia kiwango cha tarakimu moja.

(iv) Napendekeza kutoza kodi ya zuio kwenye malipo yanayofanywa kwenye Mifuko ya Jamii yanayotokana na mapato ya uwekezaji ili kuweka misingi ya usawa na haki katika utozaji wa kodi. Hatua hii inalenga kuweka wajibu wa makampuni wa kutoza kodi ya zuio kwenye malipo yanayofanywa kwenye mifuko ya jamii kutokana na upangishaji na ukopeshaji.

(v) Kumpa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato *TRA* mamlaka ya kukadiria mapato yanayotokana na pango kwa kuweka kiwango cha ukomo wa chini wa thamani kulingana na hali halisi ya soko ili kutoza kodi kwenye mapato hayo. Hatua hizi za kodi ya mapato kwa pamoja zinatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa shilingi bilioni 71.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82 napendekeza kupunguza tozo ya kuendeleza ufundi stadi (*Skills Development Levy)* kutoka kiwango cha sasa cha asilimia tano hadi asilimia 4.5 ili kuwapatia nafuu ya mzigo wa tozo waajiri na kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiyari pasipo shuruti na hivyo kuongeza mapato ya Serikali katika muda wa kati. Hatua hii itapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 28.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Magari napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Magari, Kodi ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki, Sura 124, kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya marekebisho ya viwango vya usajili wa magari kutoka sh. 150,000/= hadi sh. 250,000/= kwa kila gari.

(ii) Kupandisha ada ya usajili wa namba binafsi za magari kutoka shilingi milioni tano hadi shilingi milioni 10 baada ya miaka mitatu ili kuhuisha viwango hivyo kulingana na thamani halisi ya fedha. Hatua hizi kwa pamoja zitaongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 26.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399; Sheria ya Kodi ya Majengo ya Mamlaka ya Miji, Sura 289; Sheria ya Fedha

za Serikali za Mitaa, Sura 290; Sheria ya Utawala wa Kodi ya mwaka 2015 na Sheria ya Rufani za Kodi, Sura 208.

Napendekeza kufanya marekebisho katika sheria hizo ili kuiwezesha *TRA* kukusanya kodi ya majengo ambavyo hivi sasa kodi hiyo inakusanywa na Halmashauri. Lengo la marekebisho hayo pamoja na mambo mengine ni:-

Kuiwezesha *TRA* kukadiria kodi ya majengo na kufanya uthamini wa majengo husika, mamlaka ya mapato kupewa uwezo wa kukusanya kodi ya majengo kwa kutumia utaratibu wake wa kawaida kupitia sheria za kodi, kuweka utaratibu wa namna ya kuhifadhi na kuwasilisha kodi za majengo itakayokusanywa na *TRA* kwenye Halmashauri husika, kuweka taratibu za kutatua migogoro itokanayo na ukusanyaji wa kodi ya majengo, kusimamiwa na sheria zinazotumika hivi sasa na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kusimamia migogoro hiyo na kufanya marekebisho katika misamaha ya kodi ya majengo ili majengo mengi zaidi yaingizwe kwenye mfumo wa utozwaji wa kodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sheria ya Msajili wa Hazina, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370 ili kuzitaka Wakala na Taasisi zote za usimamizi na udhibiti zilizo chini ya Msajili wa Hazina kuchangia asilimia 15 ya mapato yake ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali, Taasisi hizo zitatangazwa kwenye gazeti la Serikali. Aidha, napendekeza kuiondoa katika orodha hiyo Taasisi ya *AICC* na kuwekwa katika orodha ya Taasisi zinazotakiwa kutoa gawio *(dividend)* kwa Serikali kwa kuwa Taasisi hiyo inafanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya kikao cha maandalizi Jijini Arusha Tanzania kuanzia tarehe 2 hadi 5 Mei 2016. Katika kikao hicho walikubaliana kwa pamoja kufanya marekebisho ya viwango vya ushuru wa pamoja wa forodha yaani *EAC (Common External Tariff)* na kurekebisha Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya viwango vya ushuru wa pamoja wa forodha yaliyokubaliwa yalizingatia kwa sehemu kubwa katika kuendeleza uchumi wa viwanda kwenye ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(i) Tanzania kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye bidhaa ya saruji inayotambuliwa kwenye *HS Code* 23.29.00 kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hatua hii inalenga katika kuhamasisha na kulinda uzalishaji

wa saruji hapa nchini ambao umekuwa ukiongezeka dhidi ya ushindani wa bei ya saruji inayoingizwa nchini kutoka nje.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kuongeza ushuru wa forodha, tulikubaliana kuongeza kutoka asilimia sifuri (0) hadi asilimia 10 kwenye bidhaa za chuma yaani *flats rolled products of iron or non-alloy steel,* hatua hii inalenga katika kulinda uzalishaji wa bidhaa hizi hapa nchini.

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, tulikubaliana kutoza ushuru wa forodha kwa asilimia 25 badala ya 10 kwenye bidhaa za nondo yaani *(bars and rods of iron and steel)* lengo la hatua hii ni kulinda uzalishaji wa bidhaa za chuma zinazozalishwa na viwanda vya ndani dhidi ya ushindani wa bidhaa zisizo na ubora na bei ya chini kutoka nje ya nchi.

(iv) Kuendelea kutoza ushuru wa forodha wa asilimia sifuri badala ya 25 kwenye bidhaa za chuma *iron and steel products* ambazo ni muhimu katika ujenzi wa madaraja. *(Makofi)*

(v) Mheshimiwa Naibu Spika, tulikubaliana pia kuendelea kutoza ushuru wa forodha kwa asilimia 10 kwa mwaka mmoja badala ya 25 kwenye *automotive bolts and nuts.* Aidha, ushuru huu unapunguzwa kwa kuzingatia kwamba, malighafi zinazotumika kutengeneza bidhaa hizi hazizalishwi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(vi) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa wazalishaji wa *bolts and nuts* kwenye malighafi kwa kutoza kiwango cha asilimia sifuri (0) badala ya asilimia 10. Lengo ya hatua hii ni kuwawezesha wazalishaji kupata malighafi hizo kwa gharama nafuu kwa kuwa hazizalishwi katika ukanda wa Afrika mashariki.

(vii) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 badala ya kiwango cha sasa cha asilimia 10 kwenye nyavu za samaki zinazotumika. Hatua hii inazingatia kuwa kuna watengenezaji wengi wa nyavu za aina hii katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(viii) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 badala ya kiwango cha sasa cha asilimia 10 kwenye bidhaa za *oil* na *petrol filters and intake air filters* zinazotambulika kwenye *HS Code* 8321.31.00 na lengo la hatua hii ni kulinda uzalishaji wa bidhaa hizi zinazozalishwa na viwanda vya ndani dhidi ya bidhaa zisizo na ubora na za bei rahisi kutoka nje.

(ix) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha na kutoza asilimia sifuri (0) kwa utaratibu wa *duty remission* kwenye malighafi za kutengeneza *air filter* za magari kwa wazalishaji hapa nchini.

(x) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha na kutoza asilimia sifuri (0) kwa utaratibu wa *duty remission* kwenye malighafi za kutengeneza vibiriti vinavyotambulika, hatua hii imezingatia kwamba, hakuna misitu ya kutosha na yenye mbao za kukomaa zinazokidhi mahitaji ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(xi) Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kupunguza msamaha wa ushuru wa forodha hatua kwa hatua kwenye sukari *(sugar and sugar confectionery)* kutoka kiwango cha sasa ambacho waagizaji wa sukari wa viwandani hulipa asilimia 10. Kutokana na kupunguza msamaha huo waagizaji watalipa ushuru zaidi hatua kwa hatua. Upunguzaji huo wa msamaha utakuwa kama ifuatavyo:- Mwaka 2016/2017, kiwango kitakuwa asilimia 15, mwaka 2017/2018, kiwango kitakuwa asilimia 20, mwaka 2018/2019 kiwango kitakuwa asilimia 25. Hatua hii inachukuliwa kwa kuwa kiwango cha sasa cha asilimia 10 kinadidimiza viwanda vyetu vya ndani na pia ni chachu ya matumizi mabaya ya misamaha husika.

(xii) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa sasa kwa baadhi ya bidhaa za *aluminium milk cans* na hizi bidhaa zilizokamilika tayari kwa kutumika hivyo zinatakiwa kutozwa ushuru wa asilimia 25 unaostahili kwa bidhaa za namna hiyo. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa ndani wenye uwezo wa kuzalisha bidhaa hizi kwenye nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(xiii) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha na kutoza asilimia sifuri, malighafi zinazoingizwa na uzalishaji wa *aluminium cans* hatua hii inalenga katika kuhamasisha uzalishaji wa *aluminium cans* katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(xiv) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwenye ngano *(wheat grain)* kwa mwaka mmoja. Hatua hii imezingatia kwamba, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki hazina uwezo wa kuzalisha ngano ya aina hii na kuweza kujitosheleza mahitaji. Aidha, utoaji wa unafuu wa uzalishaji wa bidhaa na vyakula vinavyotumia ngano na kuimarisha utulivu wa bei za bidhaa za ngano.

(xv) Kuongeza kiwango maalum cha ushuru kwenye mitumba ya nguo na viatu kutoka kiwango cha sasa cha dola za Kimarekani 0.2 kwa kilo hadi dola 0.4 kwa kilo. Hatua hii imechukuliwa ili kudhibiti hatua kwa hatua uingizaji nchini wa nguo za mitumba ambazo zinaonekana kuwa siyo salama kwa afya za watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuzuia kabisa uingizaji wa bidhaa hizi baada ya miaka mitatu kuanzia sasa. Hata hivyo, nchi zimekubaliana kuweka mikakati ya kuimarisha na kuhamasisha uzalishaji wa nguo na viatu ndani ya Jumuiya ya

Afrika Mashariki ili kukidhi hayo mahitaji. Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji tayari imeandaa mkakati madhubuti wa kuendeleza sekta ya ngozi na nguo.

(xvi) Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kutoza ushuru wa bidhaa kwa asilimia 25 au kiwango maalum cha dola za Kimarekani 200 kutegemea na kiwango kipi ni kikubwa kwa kila tani moja ya ujazo kwenye bidhaa za chuma, *(iron and iron alloy steel)* kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda uzalishaji wa bidhaa za chuma zinazozalishwa na viwanda vya ndani dhidi ya ushindani wa bidhaa hizo na ubora kutoka nje ya nchi.

(xvii) Mheshimiwa Naibu Spika, tulikubaliana pia kuendelea kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 au kiwango maalum cha dola 200 kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwa mwaka mmoja kwa kila tani moja ya ujazo kwenye bidhaa za chuma *(flat road products of bars, roads, sections, angles, shapes and related products)*. Lengo la hatua hii ni kulinda uzalishaji wa bidhaa za chuma zitakazozalishwa na viwanda vya ndani dhidi ya ushindani wa bidhaa zisizo na ubora kutoka nje.

(xviii) Kuendelea kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 au kiwango maalum cha dola cha Kimarekani 200 kutegemea na kiwango kipi kikubwa kwa mwaka mmoja, kwa kila tani moja ya ujazo kwenye bidhaa za chuma (*steel reinforcement bars angels sections)*, lengo la hatua hii ni kulinda uzalishaji wa bidhaa za chuma zinazozalishwa na viwanda vya ndani.

(xix) Mheshimiwa Naibu Spika, tulikubaliana kutoza ushuru wa forodha kwa asilimia 10 badala ya asilimia sifuri kwenye mafuta ghafi ya kula (*crude edible oil)* kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga katika kuhamasisha kilimo cha mbegu za mafuta hapa nchini na kukuza viwanda vya kutengeneza mafuta ya kula. Aidha, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imeandaa mkakati maalum wa kuendeleza viwanda vya kuzalisha mafuta yanayotokana na mbegu zinazozalishwa hapa nchini na kutumia fursa za soko kubwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo nchi yetu ina nafasi ya kuweza kuongeza uzalishaji wa mbegu za mafuta. *(Makofi)*

(xx) Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutoza ushuru wa forodha ya asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa bidhaa za karatasi. Hatua hii inachukuliwa ili kulinda viwanda vya hapa nchini vinavyozalisha karatasi za aina hiyo na ajira.

(xxi) Kuendelea kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 au kiwango maalum cha dola 200 kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwa mwaka mmoja kwa kila tani moja ya ujazo kwa bidhaa za nondo. Lengo ni kulinda viwanda vya ndani kutokana na ushindani wa bidhaa hizo zinazoagizwa kutoka nje; na

(xxii) Kuendelea kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 au kiwango maalum cha dola za Kimarekani 200 kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwa mwaka mmoja kwa kila tani moja ya ujazo kwenye bidhaa za chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya pia marekebisho kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Customs Management Act* ya mwaka 2004) kama ifuatavyo:-

(1) Kufanya marekebisho ya Jedwali Namba Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambalo linatoa msamaha wa ushuru wa forodha ili kuongeza vifaa vya majokofu yanayotumika katika kuhifadhi maiti yanayotambuliwa chini ya *HS code* 8418.69.90 kwa matumizi ya hospitali na Mamlaka za Miji *(City Councils)*.

(2) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, linalotoa ushuru wa forodha ili kuongeza vifaa vinavyotumika kwenye hospitali kuteketeza na kuchoma uchafu (*Incinerator Equipment and material used in hospitals to burn waste)*.

(3) Kufanya marekebisho katika Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuondoa msamaha wa ushuru wa forodha unaotolewa kwenye sare za wafanyakazi wa hospitali. Msamaha huu unaondolewa kwa kuwa sare hizi zinaweza kuzalishwa katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(4) Kusamehe ushuru wa forodha kwa kutumia utaratibu wa *duty remission* kwa wazalishaji wa hapa nchini wa malighafi zinazotumika kutengeneza *betry* zinazofahamika kama *deep circle betries.* Hatua hii inalenga katika kuhamasisha uzalishaji wa viwanda vya ndani kwa kuwa *betry* hizi zinazoagizwa kutoka nchi za nje zimesamehewa ushuru katika Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(5) Kufanya marekebisha katika lile Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki, linalotoa msamaha wa ushuru wa forodha ili kujumuisha chupa zinazotumika katika kukusanya damu kwenye hospitali *(blood collection tubes);* na

(6) Kusamehe ushuru wa forodha kwa kutumia *duty remission* kwa malighafi zinazotumika kuzalisha vifaa vya nishati ya umeme wa jua *(solar equipments)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi za ushuru wa forodha kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato kwa kiasi cha shilingi bilioni 42.8. Napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo ya kisera na ya kiuandishi katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine ili ziwe sanjari na

azma ya kurahisisha utekelezaji wake, marekebisho haya yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na kuleta uwajibikaji katika utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Mahakama na Mfuko wa Bunge, napendekeza kufanya marekebisho yafuatayo:-

(i) Kurekebisha Kifungu cha 29(3) cha Sheria ya Utawala wa Bunge, Sura ya 115, ili kubainisha kuwa bajeti ya Mfuko wa Bunge itawasilishwa Bungeni na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Bunge. Hivi sasa sheria hii imeweka sharti kuwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha atawasilisha Bungeni bajeti ya Mfuko wa Bunge.

(ii) Kurekebisha kifungu cha 59(3) cha Sheria ya Utawala wa Mahakama, Sura 237 ili bajeti ya Mfuko wa Mahakama iwasilishwe Bungeni na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Mahakama. Kifungu hiki kwa sasa kimewekwa sharti kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kuwasilisha Bungeni bajeti ya Mfuko wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza pia kufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa, Idara zinazojitegemea na vitahuishwa kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi. Napendekeza kufuta baadhi ya ada na tozo ambazo zimeonekana kuwa ni kero kwa wananchi na vikwazo katika kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara hapa nchini. Tozo hizo na ada ninazopendekeza kufuta ni kama ifuatavyo:-

(i) Mamlaka ya Chakula na Dawa, tunafuta kibali cha kusafirisha chakula nje ya nchi kwa sh. 50,000/=; kushikilia dawa za binadamu na mifugo zinazotengenezwa na viwanda vya ndani kwa sh. 100,000/=; kurudufu cheti cha dawa za binadamu na mifugo zinazotengenezwa na viwanda vya ndani kwa dola za Kimarekani 50; kudurufu cheti cha dawa za binadamu na mifugo zinazotengenezwa na viwanda vya nje ya nchi kwa dola za Kimarekani 100; tathmini ya matangazo ya bidhaa zinazotengenezwa nchini kwa dola za Kimarekani 50; matangazo yanayofanyiwa tathmini fupi kwa bidhaa zinazotengenezwa nchini kwa dola za Kimarekani 25; kudurufu cheti cha usafi wa chakula, dawa na vifaa tiba vinavyotengenezwa nje ya nchi kwa dola za Kimarekani 100; kudurufu cheti cha vifaa tiba vinavyotengezwa ndani ya nchi kwa dola za Kimarekani 30; kudurufu cheti cha dawa zinazotengenezwa nchini kwa dola za Kimarekani 50; na kushikilia vitendanishi vinavyotengenezwa nje ya nchi katika *register* kwa dola za kimarekani 150.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kushikiria vipodozi vinavyotengenezwa ndani ya nchi katika *register* kwa sh. 30,000/=; ukaguzi wa kiwanda cha dawa cha ndani ya nchi kabla ya kusajiliwa kwa dola za Kimarekani 250; Wawakilishi wa makampuni ya dawa ya nje ya nchi kwa dola za Kimarekani 1000; malighafi za vipodozi zinazoingizwa nchini kwa sh. 50,000,000/=; malighafi za dawa zinazoingizwa nchini kwa sh. 100,000,000/=; kibali cha hospitali kununua dawa zenye madhara ya kulevya kutoka bohari kwa dawa ya sh. 10,000/=; ada ya uingizaji nchini wa dawa zenye madhara ya kulevya ya sh. 50,000/=; cheti cha kusafirisha bidhaa nje ya nchi kwa sh. 50,000/=; cheti cha utambuzi wa dawa inayosafirishwa nje ya nchi kwa sh. 50,000/=; ukaguzi wa kiwanda kidogo kipya cha kusindika chakula, kwa sh. 100,000/= na cheti cha kuteketeza bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapendekeza pia kuondoa ada ya cheti cha afya kwa ajili ya kusafirisha bidhaa nje ya nchi kwa sh. 50,000/= na kibali cha kufanya maonesho ya biashara ya bidhaa inayodhibitiwa kwa sh. 200,000/=.

(ii) Kwa upande wa Bodi za Mazao; korosho, pamba, chai, kahawa, tumbaku, tunapendekeza kufuta ushuru wa Chama Kikuu cha Ushirika, kama ilivyo kwa korosho ni sh. 20/= kwa kilo tunapendekeza zifutwe, ushuru wa kusafirisha korosho wa sh. 50/= kwa kilo, gharama za mtunza ghala sh. 10/= kwa kilo, kikosi kazi kwa ajili ya ufuatiliaji wa masuala mbalimbali ya kuchangia sh. 10/= kwa kilo na makato ya unyaufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, tutafuta mchango wa mwenge kwa kila kiwanda cha kuchambua pamba yaani sh. 450,000/=, ada ya vikao vya Halmashauri za Wilaya wanapojadili maombi mbalimbali ya wafanyabiashara wa pamba 250,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Bodi ya Chai, kodi ya moto na uokoaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ada ya leseni ya kusindika kahawa ya dola za Kimarekani 250. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba, hatua ninazopendekeza za kufuta tozo na ada nilizozifanya hizi ni za awali tu wakati Serikali inaendelea kufanya uchambuzi na tathmini ya kina kuhusu ada zinazotozwa na mashirika na taasisi na wakala mbalimbali, lakini tozo pia kwenye mazao yote makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi ni endelevu katika kuhakikisha kuwa tunaboresha mazingira ya kufanya biashara katika nchi yetu ili iweze kuwa katika nafasi nzuri ya kiushindani katika biashara ya kuvutia uwekezaji.

Tunalenga kuondoa kero kwa wananchi na kuwapa nafuu katika uendeshaji wa shughuli za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kurekebisha baadhi ya viwango vya ada na tozo mbalimbali zitakazoainishwa kwenye Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 na sheria nyingine kutangazwa kwenye gazeti la Serikali na Mawaziri wenye dhamana na ada na tozo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi na tozo kwenye bidhaa za mafuta ya *petrol*. Kwa muda sasa bei ya mafuta *petrol, diesel* na mafuta ya taa, imekuwa ikishuka katika soko la dunia hali ambayo imesaidia kuleta unafuu wa gharama katika shughuli za kiuchumi hususan kwa wananchi maskin maana bei za mafuta haya yanagusa kila mtu. Hivyo, Serikali imeamua kuwa ushuru wa barabara, ushuru wa *petrol* na ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya *petrol* utabaki kama ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia "Serikali imeamua kuwa ushuru wa barabara, ushuru wa *petrol* na ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya *petrol* utabaki kama ulivyo sasa" hivyo Mfuko wa Barabara, Mamlaka ya Usambazaji ya Umeme Vijijini, Mfuko wa Maji watumie fedha hizo vizuri kwa viwango vya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa misamaha ya kodi, ushuru wa bidhaa, kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa forodha kwa Majeshi ya Ulinzi na Usalama kupitia kwenye migahawa na maduka maalum yanayouza bidhaa mbalimbali kwa mahitaji ya Askari; Serikali imekuwa ikifanya hivyo lakini kumekuwa na changamoto ya kuwepo kwa matumizi yasiyofaa ya misamaha hiyo. Aidha, kutokana na hali hiyo ya upotevu wa mapato nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeondokana na utaratibu huu isipokuwa kwa Tanzania na Rwanda, ambazo zinatoa msamaha wa ushuru wa forodha kwa Majeshi ya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha Mawaziri wa Fedha kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali ya Tanzania na Serikali ya Rwanda ilitakiwa kuangalia njia mbadala ya kutoa unafuu wa gharama kwa Majeshi yake badala ya utaratibu wa kutoa misamaha. Ili kuendelea kutoa huduma kwa Majeshi hayo pasipo kupoteza mapato ya Serikali, napendekeza kuwapatia posho Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama na posho hiyo itakuwa ni zaidi, ni nyongeza kwa posho ya chakula ambayo inatolewa kwa Askari wetu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama ili waweze kujipatia mahitaji hayo wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ni kusitisha msamaha huo wa kodi kwa Majeshi ili kuondokana na uvujaji wa mapato, lakini wakati huo huo kuendelea kuwapatia Askari wetu mahitaji yao muhimu kwa utaratibu mzuri zaidi. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa motisha inayotolewa inawanufaisha walengwa yaani Askari badala ya wajanja wachache kuendelea kunufaika na misamaha hiyo. Serikali itajadiliana na Majeshi husika ili kuweza kuainisha viwango stahiki vya posho ambayo itatolewa kwa Askari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2016 isipokuwa pale ambapo imeelekezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sura ya bajeti kwa mwaka 2016/2017: Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni sh. 29,539,603,000,000. Kati ya fedha hizo, mapato ya ndani ya Serikali Kuu ni shilingi trilioni 17.79; mapato ya Halmashauri ni bilioni 665.4; misaada na mikopo kutoka nje ni shilingi trilioni 3.6; mikopo ya ndani na yenye masharti ya kibiashara itakuwa ni trilioni 7.47 ambayo inafanya jumla ya mapato yote kuwa sh. 29,539,603,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa matumizi: Matumizi ya kawaida yatakuwa sh. 17,719,100,000,000 na matumizi ya maendeleo yatakuwa sh. 11,820,503,000,000 na kufanya matumizi yote kuwa sh. 29,539,603,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; wananchi wetu wengi wamechoka na adha ya umaskini. Watanzania wanataka kipato cha kuweza kukidhi mahitaji yao ya msingi, Watanzania wanataka huduma bora zaidi hususani upatikanaji wa maji, elimu, afya, umeme na makazi. Akinamama wamechoka kutembea na ndoo za maji kichwani, watoto wetu shuleni wamechoka kukaa chini na kugombania matundu machache ya vyoo, vijana wetu wanataka ajira, kilio cha mauaji ya kikatili ya *Albino* ni fedheha kwa nchi yetu na wananchi bado wananyimwa haki zao kutokana na kukithiri kwa rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanataka nchi yenye neema, Watanzania wanataka Serikali inayofanya kazi kwa ufanisi, Watanzania wanataka mazingira safi na endelevu, Watanzania wanataka miundombinu na usafiri wa kisasa na salama, Watanzania wanataka Miji na Makazi yaliyopimwa na yaliyopangwa vizuri, pia Watanzania wanapenda amani, utulivu, utangamano na furaha. Hata hivyo, napenda nisisitize kuwa Tanzania hii mpya ambayo wote tunaitamani iko mikononi mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuwaambia Watanzania wenzangu siri ya maendeleo. Siri ya kuifikia Tanzania mpya ambayo tunaitamani. Kwanza maendeleo hayaji hivi hivi, maendeleo

yanataka dhamira na utashi, juhudi na maarifa, maendeleo yanataka vitendo siyo maneno, maendeleo yanataka pawepo dira ya kutuongoza tunakotaka kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikiwa lazima kuyafahamu vizuri mazingira tulipo, njia ya kupita na hususani fursa na hatari zilizo mbele yetu, maendeleo yanataka *focus* (mwelekeo), vipaumbele, malengo na viashiria vya hatua iliyofikiwa. Maendeleo yanahitaji nidhamu ya hali ya juu hususani katika matumizi ya rasilimali watu, fedha, muda, vitendea kazi na mali. Maendeleo yanataka usimamizi makini wa utekelezaji, hivyo maendeleo yanataka hatua kali za kumwajibisha yeyote anayekwamisha na kuhujumu juhudi zetu kwa kutotimiza wajibu kwa uzembe, rushwa, ubadhirifu, yafaa hawa washughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo yanahitaji kujinyima au kujitoa *(sacrifice)* na kwa maana hiyo, yafaa Watanzania tujitafakari juu ya kujengeka kwa utamaduni wa kuchangisha michango mingi ya sherehe za anasa na badala yake tujielekeze kusaidiana katika masuala ya maendeleo kama ada za shule, gharama za matibabu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, maendeleo ni mwendelezo wa hatua stahiki badala ya kurukia mambo mapya kabla ya kukamilisha yaliyoanza kutekelezwa *(consistency of action)*. Maendeleo yanapatikana kwa kufanya kazi kwa bidii *(hard work),* maendeleo hayatakuja kwa kucheza *pool table* na kunywa viroba muda wote, maendeleo yanapatikana kwa kuthubutu *(boldness)* na kujiamini *(self confidence)* na hatimaye kuamua kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu pia niseme juu ya utegemezi kwa misaada kutoka kwa Wahisani. Tangu uhuru, wafadhili wameendelea kutupatia misaada ambayo imetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa. Nitawashukuru hivi punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, pamoja na kuwa lengo la misaada ni kujazia uwezo wa Taifa kutekeleza miradi ya maendeleo au kukabiliana na maafa, ni vizuri Watanzania wenzangu tukaelewa kuwa, kwa upande mwingine, misaada inaweza kuwa sumu ya maendeleo, misaada inaweza kuwa uchochoro wa sera na miradi mibovu, inapoteza kujiamini na masharti yanayoambatana na misaada yanapunguza uhuru wa kujiamulia mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, misaada pia inaweza kuchochea rushwa na kuzorotesha jitihada za ndani hususani za ukusanyaji wa mapato. Mwanazuoni anayeitwa Sebastian Edward katika Kitabu chake kinachoitwa "*Toxic Aid* -

Economic Collapse and Recovery in Tanzania" cha mwaka 2014, amefichua huo ukweli ninaosema kwa maneno yafuatayo, naomba kunukuu:

"*After analysing in great depth Tanzania's history during its first two decades as an independent Nation, it is clear to me that the official aid community had a major responsibility in one of the most colossal collapses of a poor country in the history of the modern world. When one adds and subtracts everything - the misguided policies, the blunders, the growing corruption and the socially worthwhile projects - the balance is hugely negative. The inescapable conclusion of that exercise is that, during 1961 to 1981, aid was worse than ineffective; it was toxic!*". Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ni muhimu sana kama Taifa tutambue jambo hili na tufanye kila linalowezekana kupunguza utegemezi kwa misaada ya Wahisani kwa kulinda utulivu wa uchumi, kwa kujenga uwezo wetu wenyewe hususani wa kukuza sekta ya viwanda ili kupanua wigo wa kukusanya zaidi mapato ya ndani na kwa ufanisi zaidi. Ni muhimu sana tuweke msukumo zaidi wa kukuza na kuvutia uwekezaji wa ndani na nje pamoja na kuimarisha biashara katika mahusiano yetu na nchi rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho na muhimu sana ni kuwa, maendeleo endelevu yanapatikana kwa haraka katika mazingira ya amani na usalama. Hivyo ni lazima tunu ya amani katika nchi yetu ilindwe kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Watanzania, Mungu ametujalia rasilimali nyingi, Mama zetu walizaa na wanaendelea kuzaa watoto wenye akili timamu, tena wabunifu na wenye uwezo wa kutatua changamoto kuu na vikwazo vya maendeleo kwa Tanzania mpya. Hivyo, tukiongozwa na uzalendo, uchungu wa nchi hii na uthubutu wa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ni lazima sasa tudhamirie kuigeuza Tanzania kuwa nguvu kuu ya kiuchumi katika Kanda hii ya Afrika *(Economic Power House)* na tufanye hivyo katika kipindi cha miaka 10 ijayo. Tukiwa na nia moja inawezekana na hakika Mungu yuko upande wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwakumbusha viongozi wenzangu na wananchi kwa ujumla kuhusu umuhimu wa matumizi ya muda ambao ni rasilimali muhimu sana katika maendeleo ya Taifa letu. Watanzania wengi tunatumia muda vibaya kwa mambo yasiyokuwa na tija na hatuzingatii muda katika kutimiza majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Watumishi wa Umma kumekuwa na mazoea ya kutumia muda mrefu kwenye vikao na mikutano na kuacha majukumu ya msingi ya kuwahudumia wananchi. Vilevile wananchi na

hasa vijana ambao ndiyo nguvukazi ya Taifa wamekuwa wakitumia muda mwingi wa kufanya kazi, kufanya mambo yasiyokuwa na manufaa kwao binafsi na Taifa kwa ujumla, hususani unywaji wa pombe, kucheza *pool,* uzuraji, kamari, sinema za mitaani, kukaa vijiweni na kupoteza muda mwingi kwenye mitandao ya kijamii. Hivyo, natoa rai kwa Watanzania wote kuthamini matumizi mazuri ya muda kwa kufanya kazi kwa bidii ili kuchochea maendeleo yetu binafsi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapoelekea kumaliza hotuba hii napenda kusisitiza mambo yafuatayo ambayo yanalenga kuimarisha ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa matumizi ili kuweza kutekeleza bajeti hii niliyoisoma kama ilivyopangwa.

(i) Serikali itaongeza msukumo katika matumizi ya mashine za *EFD* ili kuhakikisha kuwa kila mfanyabiashara anatoa risiti za mashine ya *EFD* na wananchi wanadai risiti pale wanapofanya manunuzi ya bidhaa au huduma. Katika kutimiza azma hii, Wizara yangu itaunda kikosi maalum cha kufuatilia utekelezaji wa agizo hili katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, ili kuhakikisha wale wote watakaokiuka utaratibu huu wanachukuliwa hatua stahiki za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa rai kwa Viongozi wote hususani Waheshimiwa Mawaziri, Wabunge, Madiwani na Viongozi wa Dini kuwa mfano wa kuigwa kwa wananchi wetu, kwa kuhakikisha kuwa tunadai risiti za *EFD* pale tunaponunua bidhaa. Kila asiyetoa risiti na asiyedai risiti ajue anatenda kosa na anasaliti jitihada zetu za kuijenga Tanzania mpya. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri naomba ukae kidogo, naomba urudi kwenye kiti kidogo. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5), naongeza muda wa nusu saa mpaka Waziri atakapomaliza. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

(ii) Vituo vyote vya kuuzia mafuta ya *petrol* vinaagizwa kukamilisha ufungaji wa mashine za *EFD* kwenye *pump* za kuuzia mafuta hayo ikifikapo tarehe 1 Oktoba, 2016, ili kuhakikisha kuwa Serikali inakusanya kodi stahiki. Serikali itafanya ukaguzi kwenye vituo vyote vya mauzo ya mafuta hapa nchini na kuchukua hatua za kisheria kwa wale ambao watakaidi agizo hili.

(iii) Katika kudhibiti misamaha ya kodi inayotolewa kwa Wafanyabiashara, Watumishi wa Umma, Mashirika ya Dini na Taasisi Zisizo za Kiserikali kuanzia Julai Mosi, watalazimika kulipa kodi kwanza kwa bidhaa watakazoziagiza. Kodi hiyo itarejeshwa kwa wanufaikaji baada ya ukaguzi kufanyika na kujiridhisha kuwa bidhaa hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Serikali inawataka

wanufaika kuwasilisha maombi yao Wizara ya Fedha na Mipango kabla ya kuagiza bidhaa husika ili kupata kibali cha uagizwaji wa bidhaa hizo.

(iv) Maafisa Masuuli wote wanaagizwa kutumia vifaa na mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato unaofanywa na Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika na Taasisi za Umma ili kuongeza ufanisi na udhibiti wa upotevu wa mapato. Aidha, kodi na tozo hizo zitakazokusanywa zipelekwe benki ndani ya masaa 24.

(v) Kuanzia mwaka ujao wa fedha utaratibu wa kubakiza sehemu ya makusanyo yaani *retention* umefutwa. Taasisi zote zilizokuwa zikitumia Mfuko huu zitalazimika kuwasilisha mapato yote kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Utoaji wa fedha kutoka Hazina kwenda kwenye taasisi hizo utazingatia utaratibu wa kawaida kulingana na bajeti iliyoidhinishwa.

(vi) Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia agizo la Serikali la kupunguza matumizi yasiyo ya lazima katika maeneo yaliyoanishwa ikiwa ni pamoja na safari za nje ya nchi, mafunzo nje ya nchi, posho za vikao, warsha, makongamano, sherehe na maadhimisho ya Kitaifa, ununuzi wa samani, ununuzi wa uendeshwaji wa magari na kadhalika ili kupata fedha zaidi na kuzielekeza kwenye miradi ya maendeleo na kutatua kero za wananchi.

(vii) Waajiri wanatakiwa kuwasilisha kodi ya mapato ya Wafanyakazi *(pay as you earn)* pamoja na michango kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa wakati. Aidha, kwa wale wenye malimbikizo ya *pay as you earn* na michango wanaagizwa kuwasilisha malipo hayo kabla ya tarehe 31 Desemba, 2016 vinginevyo hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yao. Maafisa Masuuli, Wakuu wa Taasisi, Mashirika na Kampuni Binafsi wanaagizwa kusimamia utekelezwaji wa agizo hili.

(viii) Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutumia mfumo wa nakala laini *(soft copy)* katika kusambaza nyaraka mbalimbali za Serikali zinazozidi kurasa 50 isipokuwa kwa mafungu yanayotakiwa kusambaza nakala ngumu *(hard copy)* kutokana na matakwa ya kikanuni au ya kisheria. Hatua hii inalenga kupunguza matumizi makubwa ya gharama ya kuchapisha na kurudufu nyaraka hizo na kulinda mazingira.

(ix) Katika mwaka 2016/2017, madai yote yanayohusu huduma za umeme, maji na simu yatalipwa moja kwa moja *(centrally)* na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kutumia bajeti za mafungu husika. Maafisa Masuhuli wanaagizwa kulipa kwa wakati ankara za huduma za umeme, maji na simu ili kuepuka malimbikizo ya madai mapya.

(x) Maafisa Masuuli wanaagizwa kufanya ununuzi kwa kutumia hati za ununuzi *(LPO's)* zinazotokana na mfumo wa *Intergrated Financial Management System*. Aidha, Wazabuni na watoa huduma wanaelekezwa kuhakikisha wanapatiwa hati za ununuzi zinazotokana na mfumo wa *IFMS* hivyo kuanzia mwaka 2016/2017 hati za ununuzi zitakazotolewa nje ya utaratibu huu hazitatambuliwa kama hati halali za ununuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya utekelezaji wa bajeti niliyoiwasilisha yanategemea sana ushirikiano wa kila mmoja wetu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Bajeti ya 2016/2017 inategemea zaidi mapato ya ndani katika utekelezaji wake, hivyo kila Taasisi ya Serikali inahimizwa kutekeleza wajibu wake wa kusimamia ukusanyaji wa mapato ili kufikia lengo la mapato lililokusudiwa na hatimaye kutoa huduma bora kwa wananchi wetu. Naomba sote tushirikiane kwa pamoja na kila mmoja awajibike katika nafasi yake ili tujenge Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, nawashukuru kwa dhati wananchi wa Tanzania, hususan Wakulima, Wafugaji na Wavuvi, Wafanyabiashara, Watumishi wa Umma na walioko katika sekta binafsi. Pia *Diaspora* ambao wanafanyakazi kwa bidii kuchangia maendeleo ya uchumi wa Taifa, ninyi ndiyo nguzo na mhimili wa Taifa linalojitegemea. Serikali inawathamini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia vijana Taifa la kesho, wale waliopo shuleni na vyuoni someni kwa bidii ili mpate maarifa na ujuzi wa kuijenga nchi yenu na wale wengine tumieni nguvu zenu na ubunifu wenu katika kilimo cha mazao ya thamani kubwa, ufugaji na huduma ikiwa ni pamoja na tasnia za ubunifu, muziki, filamu, *comedy*, mitindo ambako bado kuna fursa tele za kujipatia kipato halali ili kukidhi mahitaji ya maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba kuwatambua na kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo wanaotarajia kuchangia bajeti ya Serikali kwa mwaka wa 2016/2017 kama ifuatavyo:-

Nchi za Canada, China, Denmark, Finland, Hispania, India, Ireland, Italy, Japan, Korea Kusini, Marekani, Norway, Poland, Sweden, Belgium, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Pia Taasisi mbalimbali za Kimataifa ikiwemo *Arab Bank for Economic Development in Africa (BADEA*), Benki ya Maendeleo Afrika (*ADB*), Benki ya Dunia (*World Bank*), *Global Fund*, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, *Organisation of the Petroleum Exporting Countries (OPEC Fund),* Saudi *Fund*, Kuwait *Fund* na Umoja wa Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha napenda kutambua uhusiano mzuri tulionao na Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* chini ya mpango wa ushauri wa kisera unaojulikana kama *Policy Support Instrument*. Rai yangu kwa marafiki zetu ni kuwa; endeleeni kutuunga mkono, hususan katika jitihada zetu za kujenga uchumi wa viwanda na kuvutia wawekezaji kutoka nchi zenu na kututafutia fursa za masoko ya bidhaa zetu. Mtimize ahadi zenu kwa wakati nasi tunawaahidi kutumia michango yenu kwa ufanisi na uwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hapa Kazi Tu! Mungu Ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, Mheshimiwa Waziri wa Fedha hongera sana, naona hoja yako imeungwa mkono na Wabunge wote, pamoja na wa Kambi Mbadala. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 106(1), tutaanza mjadala wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango siku ya Ijumaa. Kwa hiyo siku ya kesho tarehe 9 Juni, 2016, tutakuwa na fursa ya kusoma hotuba hii ili tuweze kuanza mjadala wetu siku ya Ijumaa. Kwa hivyo mfahamu tu kwambam siku ya kesho hatutakuwa na Bunge mpaka siku ya Ijumaa ili mpate nafasi ya kujisomea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilete kwenu matangazo kadhaa niliyonayo hapa mezani. Tangazo la kwanza linahusu wageni tulionao siku ya leo. Tunao Viongozi mbalimbali na nitaanza kuwatangaza kwa utaratibu ufuatao:-

Nitaanza na Mheshimiwa Balozi John William Herbert Kijazi ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi. Karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, tutaanza na Jenerali Davis Mwamunyange, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi; tunaye pia ndugu Rashid Othman ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa; tunaye Ndugu Abdulrahman Kaniki ambaye ni Naibu Inspekta Jenerali wa Polisi; tunaye Ndugu John Casmir Minja ambaye ni Kamishna Jenerali wa Magereza; tunaye Brigedia Jenerali Michael Isamuhyo ambaye ni Mkuu wa JKT; tunaye Ndugu Thobias Andengenye ambaye ni

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji; na tunaye Ndugu Victoria Lembeli ambaye ni Kaimu Kamishna Jenerali wa Uhamiaji. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Watendaji Wakuu Serikalini, tutaanza na Profesa Benno Ndulu ambaye ni Gavana wa Benki Kuu; tunaye pia Kamishna Valentino Mlowola, Mkurugenzi Mkuu TAKUKURU; tunaye pia Ndugu Alphayo Kidata, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; tunaye pia Ndugu Peter Shija ambaye ni Kaimu Mratibu Msaidizi wa Baraza la Usalama la Taifa. *(Makofi)*

Tunaye pia Dkt. Servacius Likwelile ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, karibu sana shemeji. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Julian Banzi Raphael ambaye ni Naibu Gavana wa Benki Kuu; tunaye pia Profesa Mussa Assad ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; tunaye pia Ndugu Cathlex Makawia ambaye ni Mwakilishi wa Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; tunaye pia Ndugu Florence Mwanri ambaye ni Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, kundi lingine la wageni ni la Viongozi Wastaafu waliopo Dodoma ambao kwa leo tunaye Mheshimiwa John Samwel Malecela ambaye ni Waziri Mkuu mstaafu. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni maalum ambao ni Mama Mbonimpaye Mpango ambaye ni mke wa Waziri wa Fedha na Mipango, karibu sana wifi yetu na mama yetu. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Benedict Likando ambaye ni Mkurugenzi wa *NCIS* – Zambia, tunaye pia Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka, mwakilishi wa Katibu Mkuu CCM. Tunaye pia Askofu Dkt. Eliud Isanja ambaye ni Askofu Mkuu wa *IEC* na Mchungaji Ismael Gabriel Maasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia jumla ya wawakilishi kumi na sita (16) wa Vyama mbalimbali vya Siasa vilivyosajiliwa kama ifuatavyo:-

Ndugu Fahmi Dovutwa, ambaye anatoka *UPDP;* Ndugu Rashid Rai ambaye ni wa *ASP;* Ndugu Abdul Mluya ambaye anatoka Chama cha *DP*; Ndugu Nancy Mrikaria ambaye anatoka *TLP*; Ndugu Yusuf Manyanga anayetoka SAU; tunaye Ndugu John Shibuda ambaye anatoka *TADSA;* tunaye pia Ndugu Hassan Kisyaga ambaye anatoka *NRA;* Ndugu Salum Kibanda ambaye anatoka Jahazi Asilia; Ndugu Renatus Muhabi anayetoka *CCK;* Ndugu Mlenda Kamara anayetoka *UMD;* Ndugu Donnie Mnyamani anayetoka *ADC;* Ndugu Tozi Matwanga anayetoka *NLD;* Ndugu Kisa Mussa anayetoka *APPT*

Maendeleo; Ndugu Mohamed Abdul anatoka Demokrasia Makini; Ndugu Makaja Ikoles anatoka *UDP*; na Ndugu Mwaka Mgimwa anayetoka CHAUSTA. Karibuni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Waheshimiwa Wabunge wanaoiwakilisha Tanzania kwenye Bunge la Afrika Mashariki, hawa wanaongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wasimame wote kwa pamoja. Karibuni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunao pia Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Mabalozi wanaoziwakilisha nchi mbalimbali hapa nchini wakiongozwa na Kaimu Mkuu wa Mabalozi Mheshimiwa Balozi Meja Jenerali Edzai Chimonyo ambaye pia ni Balozi Mkazi wa Jamhuri ya Watu wa Zimbabwe; Mabalozi wasimame kwa pamoja. *Can the Diplomats* – aah wameshaelewa! Karibuni sana wageni wetu. *Thank you for coming! (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia kundi lingine la Wakuu wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa wakiongozwa na Mratibu Mkazi Umoja wa Mataifa *UN Resident Coordinator* Ndugu Alvaro Rodrigues. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Washirika wa Maendeleo yaani *Development Partners* ambao wanaongozwa na Mwenyekiti wa Wahisani na Kiongozi Mkaazi wa Umoja wa Ulaya, Mheshimiwa Balozi Roland Van Der Geer. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Makatibu Wakuu 25 wanaoziwakilisha Wizara zao wakiongozwa na Ndugu Mussa Uledi ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge. Wasimame wote kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Watendaji kutoka Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zake wakiongozwa na Ndugu Dorothy Mwanyika ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Umma, wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Viongozi na Watendaji Waandamizi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa Ndugu Jordan Rugimbana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Viongozi wa Taasisi za Elimu ya Juu Dodoma ambao ni wafuatao:-

Askofu Donald Mtetemela, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu John; tunae pia Ndugu Constantine Lufulilo ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Mipango; tunaye pia Profesa Emmanuel Mjema ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Biashara *(CBE);* na Dkt. Mpambila Madale ambaye ni Kaimu Mkuu wa Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Viongozi wa Dini wa Mkoa wa Dodoma, tunaye Askofu wa Mkoa Kanisa la Anglikana, tunaye pia Askofu wa Mkoa wa Kanisa la KKKT. Tunaye pia Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Dodoma na pia tunaye Kaimu Sheikh wa Mkoa, BAKWATA. Karibuni sana Viongozi wetu wa Dini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wawakilishi wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Fedha zilizopo Dodoma Mashirika hayo na Taasisi hizo ni *NSSF, PPF, NMB, CRDB, NBC, TTCL*, Shirika la Posta na *BOT*, wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana! *(Makofi)*

Tunao pia Wazee wa Mkoa wa Dodoma ambao ni wafuatao:-

Mzee Samwel Kasori, Mzee Job Lusinde, Mzee Mohamed Makubeli, Mama Fatuma Mtaki, Mama Magreth Mwamoto, Mzee Stanslaus Nyange, Mzee Paulo Luhama, Mzee Pancras Ndejembi, Mzee David Mzuri, Mzee Christopher Mwaka na Mzee Peter Mavunde. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Kundi la mwisho ni la Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo, Ofisi ya Bunge. Wao wamekaa upande wangu wa kulia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo lingine la taarifa kuhusu Spika. Tangu juzi kumekuwa na taarifa zinazosambazwa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu hali ya Mheshimiwa Spika na kuzua hofu kwa wananchi kuhusu kiongozi wetu. Naomba nichukue fursa hii kuwafahamisha kuwa taarifa hizo ni za uzushi mkubwa na hazina ukweli wowote.

Waheshimiwa Wabunge, hali ya Mheshimiwa Spika ni njema kabisa na yupo nchini India ambako alikwenda kwa uchunguzi wa afya yake kufuatia maelekezo ya Daktari aliyokuwa amempa mwishoni mwa mwaka uliopita. Kwa hiyo, ameenda kwa sababu hizo!

Mheshimiwa Spika amekuwa akipata salamu mbalimbali kutoka kwa Viongozi wa Kitaifa na wananchi wanaomjulia hali na amekuwa akiwasiliana nao. Kwa hivyo, anaendelea vema, niwatoe hofu na ametuma salamu zake kwenu Waheshimiwa Wabunge na kuwatakia mfungo mwema wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Pia, Mheshimiwa Spika amewatakia kazi njema katika mjadala wa Bajeti ya Serikali inayosomwa leo na nawasihi wote tuendelee kumwombea ili afya yake izidi kuimarika haraka na aweze kurejea nchini. Hivyo,

nawaomba Watanzania wenye nia njema na Spika wetu waendelee kupuuza hizo taarifa na waendelee kumwombea ili aweze kurejea nyumbani mapema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni la kazi. Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)*, Wajumbe wa Kamati hiyo wanaombwa kukutana kesho Alhamisi tarehe 9 Juni, 2016, saa Tano asubuhi Ukumbi wa Msekwa C, tangazo limetoka kwa Mwenyekiti.

Pia Waheshimiwa Wabunge mnakumbushwa, tulitangaza asubuhi kwamba kesho kutakuwa na kikao cha pamoja kati ya Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge wanaotoka Tanzania wa Bunge la Afrika Mashariki, saa nne asubuhi Ukumbi wa Msekwa. *(Makofi)*

Waheshimwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, nisome mwongozo mmoja kwenu kabla sijaahirisha Bunge. Huu ni mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy kuhusu malipo ya posho kwa Wabunge wanaosusia mjadala wa Bunge la Bajeti kwa kutoka Ukumbini.

Waheshimiwa Wabunge, mnamo tarehe 6 Juni, 2016 katika Kikao cha 37 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge, Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy aliomba Mwongozo wa Spika, kuhusu Wabunge ambao wamekuwa wakisaini kwa utaratibu mpya wa kielektroniki (*biometric attendance register),* lakini baada ya hapo wanatoka ukumbini bila kushiriki mjadala wa Bunge la Bajeti unaoendelea.

Hoja ya Mheshimiwa Keissy ilikuwa ni kutaka kujua ni utaratibu gani utatumika kudhibiti vitendo hivi ili kuokoa fedha za Serikali zinazolipwa kama posho kwa Wabunge hao wanaosusia vikao vya Bunge la Bajeti. Mheshimiwa Keissy alieleza kuwa kwa wiki, Serikali inapoteza kiasi cha shilingi 42,760,000 kwa kuwalipa posho Wabunge hawa wasiohudhuria vikao vya Bunge. Baada ya kuombwa Mwongozo huo nilieleza kuwa nitalifuatilia suala hili kuona namna nzuri ya kulishughulikia.

Waheshimiwa Wabunge, vitendo vya Waheshimiwa Wabunge kujisajili na kisha kutoka ukumbini vimekuwa vikiendelea kwa muda mrefu mpaka sasa na jambo hilo limekuwa likipingwa na kukemewa vikali na baadhi ya Wabunge wanaobaki ukumbini. Wabunge hao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiomba Mwongozo wa Kiti kuhusu kukubalika au kutokubalika kwa vitendo hivyo.

Tarehe 27 Aprili mwaka 2016, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ambaye alihoji endapo ni haki na sahihi kwa Wabunge hao kupokea posho wakati hawashiriki kutimiza wajibu wao wa Kikatiba na Kisheria.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka mwongozo huu uliombwa wakati tukijadili hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani ilisema isingeshiriki lakini wote mtakumbuka kwamba walikuwepo humu ndani, hawakutoka nje. Nikijibu mwongozo huo nilieleza Bunge kuwa, Bunge lina jukumu zito la kujadili bajeti hivyo kila Mbunge anao wajibu wa kushiriki kikamilifu na kuchangia bajeti jambo ambalo naamini ndicho wananchi wanachokitazamia. Aidha, nilieleza kuwa inatakiwa uandaliwe utaratibu mahsusi utakaowezesha Waheshimiwa Wabunge kulipwa posho baada ya kutekeleza majukumu yao ipasavyo na siyo kujisajili pekee. *(Makofi)*

Mnamo tarehe 30 Mei, Mheshimiwa Dkt. Harrison Goerge Mwakyembe, Waziri wa Katiba na Sheria naye aliomba mwongozo kuhusu suala hilo hilo baada ya kutoridhishwa na vitendo vya Wabunge kujisajili na kisha kutoka nje ya ukumbi na kulipwa posho bila kufanya kazi. Mheshimiwa Mwakyembe alinukuu Ibara ya 26 ya Katiba ambayo inatoa nafasi kwa mtu yeyote kuhoji kuhusu vitendo vinavyofanywa kinyume na Katiba. Aidha, alisisitiza kwamba kila mtu anapaswa kupata ujira kulingana na kazi anazozifanya na hapo alinukuu Ibara ya 23(1).

Katika kujibu mwongozo wa Mheshimiwa Mwakyembe niliendelea kusisitiza kwamba Mbunge anatakiwa kulipwa mshahara au posho kutokana na kuhudhuria na kushiriki mijadala ya Bunge na kwa kuwa Wabunge ni Wawakilishi wa wananchi katika kusimamia Serikali, kutohudhuria Bungeni na kususia kutoa mchango wa mawazo ni kushindwa kutimiza wajibu wake wa Kibunge na kwamba siyo sahihi na halali kwa Mbunge kupokea posho na mshahara bila kufanya kazi.

Vilevile Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy kutokana na kutoridhishwa na tabia hiyo ya Wabunge aliwahi kuomba mwongozo katika jambo hilo katika Kikao cha Thelathini na Nne, siku ya tarehe 1 Juni, 2016 na kujibiwa. Alipoona jambo hilo linaendelea na Wabunge wanaotoka ukumbini hawazingatii maelekezo ya Kiti, mnamo tarehe 6 Juni, 2016 aliomba tena mwongozo ambao ndiyo huu ninaoutolea maelezo.

Waheshimiwa Wabunge, nimetafakari kwa kina kuhusu vitendo vya baadhi ya Wabunge kutia saini, kuingia ukumbini na kisha kutoka nje ya ukumbi na kuona kwamba endapo tabia hii itaachwa iendelee naamini itafika siku ambayo Wabunge wote kwa ujumla wetu tutajisajili kuingia ukumbini na kisha kutoka nje jambo ambalo litasababisha shughuli za Bunge kutotekelezeka na hivyo kukiuka masharti ya Katiba yanayolipa Bunge hili majukumu ya kutekeleza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inaeleza kwamba Kiti kinapaswa kuzingatia, pamoja na mambo mengine, maamuzi ya awali yaliyowahi kutolewa na Maspika wa Bunge. Katika suala hili lililoombewa mwongozo sawa na katika miongozo ya Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Mwakyembe, Bunge letu liliwahi kutoa mwongozo kwenye suala la Wabunge kuingia ukumbini na kisha kutoka nje na hivyo kutoshiriki kwenye shughuli zilizopangwa. Nimepitia maamuzi mbalimbali yaliyowahi kutolewa na Bunge letu yaani *Speaker's Rulings* kuhusiana na suala kama hili, hususan vitendo vya Wabunge kutoka ukumbini bila kutekeleza shughuli rasmi za Bunge.

Mnamo tarehe 8 Aprili, mwaka 2008 Wabunge wa Chama cha *CUF* walitoka Bungeni na kususia shughuli rasmi zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa kwa siku hiyo Bungeni. Kutokana na kitendo hicho cha Wabunge wa *CUF*, Kiti kilitoa uamuzi ufuatao: Nanukuu:

"Kwa sasa natamka tu kwamba, Wabunge waliotoka nje ya ukumbi kwa shughuli zisizokuwa rasmi kwa maana ya Bunge hili, basi hawastahili kulipwa posho zinazohusika kwa siku zote ambazo watakuwa nje mpaka hapo tutakapotangaza utaratibu mwingine, kwa sababu waliyokwenda kuyafanya wala hayahusiana na shughuli za Bunge letu".

Waheshimiwa Wanunge, napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwa mujibu wa Kanuni ya 146(1) ya Kanuni za Bunge, wajibu wa kwanza wa kila Mbunge ni kuhudhuria vikao vya Bunge na Kamati zake. Jambo hili linapaswa kuzingatiwa na kila mmoja wetu. Kitendo cha baadhi ya Wabunge kutoka nje mara baada ya kujisajili na hivyo kutohudhuria vikao ni ukiukaji wa Kanuni ya 146(1) inayomtaka kila Mbunge kutekeleza majukumu yake kwa kuhudhuria vikao vya Bunge na vikao vya Kamati.

Hivyo basi, kwa kuwa jambo hili halikubaliki na kwa kuwa, miongozo kadhaa imetolewa kuwasihi Waheshimiwa Wabunge wasitoke nje ya ukumbi wa Bunge, kwa shughuli zisizo rasmi, lakini vitendo hivyo vimekuwa vikiendelea na hivyo kuleta tafsiri mbaya ya chombo hiki na kuathiri mwenendo mzima wa shughuli za Bunge.

Kutokana na maelezo hayo pamoja na masharti ya Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naagiza kwamba Wabunge wote wanaojisajili na kisha kutoka ukumbini kwa kususia kushiriki mijadala ya Bunge hawastahili kulipwa posho kwa siku zote ambazo wamekuwa wakijisajili kuingia ukumbuni na kisha kutoka ukumbini. Huu ndiyo mwongozo wangu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, niwakumbushe kwamba, kesho hakutakuwa na shughuli za Bunge kwa sababu Wabunge wanapewa nafasi ya kusoma bajeti. Hivyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Ijumaa, tarehe 10, saa tatu Asubuhi.

(Saa 12. 25 Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 10 Juni, 2016, Saa Tatu Asubuhi)